

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 13 Mei, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI- KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA AFYA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI: Ahsante, Naibu Waziri wa Afya,

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, na ninamuita Mheshimiwa Grace Victor Tendega, swali lake litauliza na Mheshimiwa Esther Matiko.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 188

Fedha za Maendeleo kwa Halmashauri

MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. GRACE V. TENDEGA
aliuliza: -

Je, ni vigezo gani vinapaswa vifuatwe na halmashauri ili fedha za maendeleo ziweze kutolewa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa fedha za maendeleo zilizotengwa katika bajeti hutolewa kwa halmashauri kwa kuzingatia Waraka na Mwongozo wa Wizara ya Fedha na Mipango kila mwaka kwa kuzingatia maelekezo ya Kifungu Na. 5 cha Kanuni za Sheria ya Bajeti Sura 439, Kifungu cha 6 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Kifungu cha 12 cha Sheria ya Bajeti Sura 439.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vigezo hivyo ni pamoja na halmashauri kuwasilisha maombi ya fedha za utekelezaji ikionesha utayari wa kuanza kutekeleza mradi mara baada ya kupokea fedha. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kwanini sasa Serikali haina mikakati ya kuhakikisha kwamba halmashauri zenye vyanzo vidogo vya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mapato iweze kuwa inawapa fedha nyingi kuliko ambazo zinatengwa ukilinganisha na halmashauri nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwanini Serikali isitumie vigezo vya ukubwa wa eneo ili kuhakikisha kwamba inatoa fedha kulingana na kipaumbele, kulingana na ukubwa wa eneo husika, kuliko wanavyofanya sasa hivi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vyanzo ambavyo halmashauri wanakusanya kwa mapato ya ndani vinatofautiana katika halmashauri moja na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kwamba zile halmashauri zinazopata mapato kidogo ya ndani zipewe fedha zaidi. Ni kwamba suala hili linakwenda kuzingatia pia mara nyingi, ukiziona halmashauri hizi zenye mapato madogo ni halmashauri pia ambazo zina population ndogo lakini pia zina shughuli za kibashara ndogo zaidi ukilinganisha na halmashauri zenye mapato makubwa kwa sababu mapato yanatokana na shughuli za kiuchumi katika halmashauri husika.

Kwa hiyo, utaratibu wa kupeleka fedha unazingatia pia *population* ya eneo husika, lakini pia na shughuli zile, kwa mfano miradi ya kimkakati ambayo ilitakiwa kwenye kuwekezwa kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutaendelea kufanya tathmini kuona uwezekano wa kuongeza zaidi *package* za maendeleo kwa halmashauri zenye mapato madogo, ukilinganisha na halmashauri zenye mapato makubwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kuzingatia ukubwa wa eneo la kijigrafia, suala hili linategemeana na ukubwa lakini pia *population* kwa sababu fedha za maendeleo zinapelekwa kwa ajili ya kusaidia wananchi. Kuna halmashauri ambazo ni kubwa sana zina maeneo ya hifadhi za misitu na kadhalii. Kwa hiyo, ukiangalia tu ukubwa wa jiografia utapeleka fedha nyingi eneo ambalo lina *population* ndogo kwa sababu tu kuna ukubwa wa jiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunazingatia yote, ukubwa, *population* lakini pia na shughuli zingine za kimaendeleo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fedha za maendeleo kwenye halmashauri wakati mwingine imekuwa ikitoa fedha mwezi ambao unakaribia mwisho wa mwaka wa fedha kuisha.

Je, Serikali imetatua vipi changamoto hii ya kuchelewesha fedha kwenye halmashauri na baadaye kuzirudisha hazina?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, majibu kwa swali hilo muhimu sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zinapelekwa kwenye halmashauri zetu karibu na mwisho wa mwaka wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

fedha mara nyingi zimekuwa zikirejeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo mahususi yametolewa, kuhakikisha kwamba halmashauri ambazo zinapokea fedha karibu na mwisho wa mwaka wa fedha, ziandike barua kupitia ofisi ya Rais TAMISEMI, kwenda Wizara ya Fedha na Mipango, siku 15 kabla ya tarehe 30 ya mwaka husika, ili zile fedha zisirejeshwe ziendelee na miradi, kwa maana ya *quarter* ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, sasa namuita Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, aulize swali lake.

Na. 189

Kituo cha Afya Mapera Kutoa Huduma za Mionzi na Ultra Sound - Mbinga

MHE. BENAYA L. KAPINGA aliuliza: -

Je ni lini Kituo cha Afya Mapera kilichopo Mbinga Vijijini Kitaanza kutoa huduma za Mionzi na *Ultra sound*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI , OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Mapera kilipokea fedha Shilingi Milioni 400 mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya ukarabati mkubwa na upanuzi wa Kituo. Kituo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hicho kimekamilika na kuanza kutoa huduma za upasuaji toka Julai 2021 na jumla ya Wakinamama 114 wamekwisha pata huduma ya upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wananchi wa Kata ya Mapera wanapata huduma ya *X-Ray* kwenye Kituo cha Afya cha Maguu kilichopo kilometa tatu kutoka kwenye Kituo cha Afya Mapera. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga inashauriwa kutenga fedha kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga jengo la *X-ray* ili Serikali ikipatie Kituo hicho mashine ya *X-ray*. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijiji swali la nyongeza.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana na nishukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kituo hiki cha Mapela, ndio kituo pekee cha Serikali katika Halmashauri ya Mbinga Vijiji ambayo ina kata 29. Hicho kituo cha Maguo alichokitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ni kituo cha Mission, tu nashukuru wanatusaidia, sina hakika kama gharama zake zinalingana, sina hakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti nina maswali maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini Serikali itapeleka wahuduma wa afya, katika zahanati saba Kipolopolo, Lukiti, Kihuruku, matuta, Mwihayo, Ikwela na Lituru; zahanati hizi nimeuliza mwaka jana swali hapa. Lini zitafunguliwa maana wananchi wamejenga na wamekamilisha, lini sasa zitafunguliwa ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Halmasauri ya Mbinga, ina upungufu mkubwa wa watumishi, zaidi ya asilimia 80 hatuna watumishi. Je, katika mgao huu unaokuja, Serikali ipo tayari kuwaonea huruma na kutoa kipaombele katika halmashauri ya Wilaya ya Mbinga?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijiini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyezekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Mbinga Vijijiini ina kata 29 na ina kituo kimoja cha afya; lakini nimuhakikishie Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Hassan ameweka mkakati wa uhakika wa kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika kata za mkakati na tarafa za kimkakati. Tulishakuomba na ulishaleta hapa orodha ya kata ambazo zitajengewa vituo vya afya. Nikuhakikishie Serikali hii siku tutahakikisha tunajenga vituo vya afya katika Jimbo la Mbinga Vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, lakini pili, kuhusiana na watumishi kuhitajika katika zahanai saba; kwanza niwapongeze sana wananchi wa Mbinga Vijijiini kwa kutoa nguvu kujenga zahati saba ambazo zimekamilika, lakini na Serikali ilichangia. Nimpahakikishie kwamba tunakwenda kuzisajili zahanati hizi. Kwa upande wa ajira hizi ambazo zimetangazwa tutakwenda kutoa kipaumbele kikubwa kwenye halmashauri zote zenye upungufu mkubwa wa watumishi ikiwepo Halmashauri ya Mbinga Vijijiini. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya TAMISEMI, sasa namuita Mheshimiwa Jerry William Silaa, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu.

Na. 190

**Mikopo Inayotolewa na Halmashauri Kujumuisha
Wazee na Wanaume**

MHE. ELIBARIKI E. KINGU K.n.y MHE. JERRY W. SILAA
aliuliza:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuwaingiza Wazee na Wanaume kwenye mikopo inayotolewa na Serikali kuititia Halmashauri kwa kuwa sasa wameachwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa Mbunge wa Jimbo la Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria ya mikopo ya asilimia 10 na kanuni zake, mikopo hili inatolewa kwa ajili ya kuwezesha makundi maalum ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata mikopo yenye masharti nafuu. Makundi haya kwa kiasi kukubwa hayawezi kupata mikopo katika taasisi nyingine za fedha kwa sababu ya kukosa dhamana na uwezo mdogo wa kumudu riba ili waweze kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kujongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya utoaji na urejeshaji wa mikopo hili tangu kutungwa kwa sheria. Tathimini hili itawezesha kushauri namna bora ya utoaji wa mikopo pamoja na mapitio ya Sheria. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kingu swali la nyongeza.

MHE. ELIBARIKI E. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha hizi asilimia kumi zinazotolewa kama mikopo zinatokana na tozo pamoja na kodi ambazo wananchi kwa ujumla wengi wanashiriki kuzitoa na zinazokusanya katika halmashauri yetu;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuwapitia vijana wote mikopo bila kuwabagua, kama vile Serikali vijana wengi waliojiajiri katika sekta za uzalishaji, ujasiriamali, kilimo na boda boda,?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wanaume, kwa maana ya akina baba nao pia wamekuwa wakijishughulisha na shughuli za uzalishaji. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuwapatia nao mikopo bila kuwabagua?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Elibariki Kingu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba asilimia kumi inatokana na mapato ya ndani na inagusa makundi ya wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu. Na niseme dhahiri kwamba mikopo hii haina ubaguzi wowote kwa vijana, kwa wanawake, wala watu wenyewe ulemavu. Suala ambalo wanatakiwa kufanya kwa mujibu wa sheria na kanuni za asilimia kumi ni kuomba kupitia vikundi vyao vya ujasiriamali. Na vijana wote wanaomba kupitia vikundi na wakawa na sifa hizo hakuna anayebaguliwa, wote wanapewa mikopo hiyo katika mazingira ya halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunawapa fursa vijana wote wanawake na watu wenyewe ulemavu ili waweze kuijendeleza katika shughuli za kuijasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la wanaume, utoaji wa mikopo hii ni kwa mujibu wa sheria, na sheria yetu ambayo tulipitisha katika Bunge hili ilisema vijana, wanawake, na watu wenyewe ulemavu. Vijana ni umri wa chini wa miaka 35, lakini hoja ya msingi ni kwamba wanaume walio

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wengi ukilinganisha na makundi haya tayari wanauwezo wa kuwa dhamana, kwa maana ya ardhi, majengo na biashara ambazo zihawezza kutumika kama *collateral* kwenye mikopo ukilinganisha na makundi haya. Ndiyo maana tuliweka kipaumbele kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kwa sababu hawana *collaterals* zinazowawezesha kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kufanya tathmini kuona uwezekano wa kuingiza wanaume kwa kadri itakavyoona inafaa. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Naona mpo watatu hapo, Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa walemauvu hawa si wote wana uwezo wa kufanya shughuli za kibashara ama kuiwezesha kiuchumi lakini wanalelewa na babu zao, bibi zao ama baba zao ama wajomba zao ambao hawa-*qualify*katika hii asilimia kumi.

Je, Serikali haioni wakati umefika sasa wakuangalia wazazi ama walezi wanaoangalia walemauvu ambao wenyewe hawaijiwezi lakini wanaweza kuwezesha kwa ajili ya kuangalia?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna walemauvu ambao hawana uwezo wa kufanya shughuli hizo na wangehitaji kupata mikopo ili wajikwamue kiuchumi. Naomba tuchukue wazo la Mheshimiwa Mbunge, tukalifanyie tathmini na kuona

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uwezekano wa kuwapa mikopo hiyo wazazi au walezi wa hao wenye ulemavu ili waweze kuwasaidia. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond, nimekuona.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kutokana na majibu ya msingi ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri ameendelea kusisisitiza kwamba mikopo hiyo inatolewa kwa vikundi; na kwa kuwa hiyo dhana ya vikundi imekuwa ni mwiba sana kwa wale akina mama wa Kilimanjaro wanaotaka kuchukua mikopo hususan wale ambao wako katika ujasiriamali.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kurekebisha kipengele hicho ili mikopo hiyo itolewe kwa mtu mmoja mmoja?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kuipitia sheria na kanuni ya mikopo ya asilimia kumi. Katika kupitia kanuni hii tayari tumeshaanza kufanya tathmini kwa kina ili kuona maeneo gani yanahitaji kuboreshwa zaidi likiwemo suala la kuona uwezekano wa mtu mmoja kupata mkopo badala ya vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya tathmini hiyo, tutafanya maamuzi na kuona utaratibu sasa utakuwa wa aina gani. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Tunaendelea Wizara ya Kilimo, sasa namuita Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 191

Mchakato wa Kilimo cha Umwagiliaji Mto Luiche – Kigoma

MHE. KAVEJURU E. FELIX aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuanza Kilimo cha Umwagiliaji katika Bonde la Mto Luiche Mkoani Kigoma?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Luiche liliopo katika manispaa ya Kigoma Ujiji mkoa wa Kigoma. Bonde hilo linauwezo wa kumwagilia hekta 3,000 na kunufaisha wakulima wa vijiji vitatu vya Mahembe, Nyangofa na Kidawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa skimu hii utaanza mwaka wa fedha 2022/2023. Utekelezaji wa mradi huu unafadhiliwa na Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund for Arab Economic Development*) ambapo litajegwa bwawa lenye mita za ujazo milioni 70, ujenzi wa mfereji mkuu Kilomita 10 na mifumo ya umwagiliaji. Serikali imepata kibali (*No Objection*) kutoka kwa wafadhili mwezi Aprili, 2022 kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu na kutafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Luiche.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix Mbunge wa Buhigwe swalii la nyongeza.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru Serikali kwa majibu mazuri juu ya kilimo cha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

umwagiliaji katika Bonde la Mto Ruichi. Nina swali moja la nyongeza. Jimbo la Buhigwe lina skimu mbili, skimu ya Rukoyoyo na skimu ya Mugera ambazo nazo hazijawahi kupata msaada wowote kutoka Serikalini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuziendeleza skimu hizi za Rukoyoyo na Mugera zilizoko katika Wilaya ya Buhigwe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Anthony Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango mkakati, tulliweka Wizara ya Kilimo ni kuhakikisha skimu zote za umwagiliaji hapa nchini zinafanya kazi. Hivyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, ya kwamba katika bajeti yetu inayokuja itakayosomwa wiki ijayo wataona miradi mingi ambayo tumeainisha kwa ajili ya kuifufua, kuikarabati na kujenga upya ambapo pia naamini itagusa katika mikoa mingi ikiwemo Mkoa wa Kigoma. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swalii la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Serikali iliahidi kukamilisha miradi ya umwagiliaji ya skimu ya Karema na skimu ya Kabaki. Kupitia kwa Waziri aliyekuwpepo aliahidi kuwa atakamilisha hiyo miradi.

Je ni lini itakuja kukamilisha hiyo miradi miwili ndani ya Wilaya ya Tanganyika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kilimo, Mheshimiwa Mavunde, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, mimi nimefika na nilitoa pia ahadi hii mbele ya wananchi wake katika mkutano wa adhara ambao tuliuafanya pale kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti inayokuja ya mwaka 2022/23 miradi wa skimu hizi imeainishwa na itatekelezwa kupitia bajeti hiyo inayokuja. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuliipokea na tunaendelea na utekelezaji wa miradi hiyo.

MWENYEKITI: Asante, Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Serikali iliwekeza zaidi ya milioni 700 kwenye Bonde la Miogwezi lilioko kwenye Kijiji cha Igongo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, lakini mradi ule umesimama.

Je, Mheshimiwa Waziri huu nao ni kati ya miradi itakayotekelawa kwenye mwaka wa fedha 2022/2023?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi linaloendelea hivi sasa ambapo ni maelekezo wamepewa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika kuhakikisha kwamba miradi yote hii inafanya kazi. Tumewapa jukumu la kupitia miradi yote nchi nzima kujua *status* yake, tuone ipi inafanya kazi, ipi inahitaji

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

marekebisho na ipi inahitaji *over whole*, kwa maana ya kuanza upya katika mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika bajeti yetu ambayo tutaisoma wiki inayokuja tutaainisha miradi ambayo itatekelezwa na imani ni kwamba katika mradi aliosema tutaingiza katika utaratibu wa utekelezaji katika bajeti inayokuja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasunga swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika Kata ya Msia pana bwawa dogo ambalo lipo katika Kijiji cha Msia. Bwawa hili linaweza kutumika sana katika kilimo cha umwagiliaji hasa katika mashamba ya kahawa. Na kwa muda mrefu limekuwepo kwenye bajeti lakini Serikali hajaweweza kutekeleza. Ni lini Serikali itaanza kutekeleza lile bwawa ili liweze kutumika katika kilimo cha umwagiliaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hasunga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha ya kwamba ifikapo mwaka 2025 tumekuwa na eneo la umwagiliaji la hekta milioni moja na laki mbili yakiwa ni maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, ya kwamba katika kufikia azma hiyo ni lazima pia tutekeleze miradi mingi kadri iwezekanavyo ili wananchi wengi waweze kunufaika. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba bwawa alilolisema tutaelekeza wataalamu katika bwawa la pili pia kulipitia ili waje watushauri vizuri namna ya utekelezaji wake lakini ni jambo ambalo ndani ya wizara tunaona kwamba ni jambo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

muhimu na hivi sasa changamoto kubwa ni upatikanaji wa mabwawa yenyeye uhakika wa maji. Kama bwawa lipo tayari ni njia rahisi zaidi ya kuanza utekelezaji wa mradi. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge tutalisimamia hilo na mradi utatekelezeka.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Athnony Peter Mavunde kwa majibu. Sasa tunakwenda Wizara ya Habari, Mawasiliano, Teknoloja ya Habari namwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo aweze kuuliza swali lake.

Na. 192

Hitaji la Mawasiliano - Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Minara katika maeneo yasiyo na minara na kutatua matatizo ya mawasiliano katika maeneo yenyeye Minara?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Kundo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknoloja ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) inatekeleza miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata tatu za Ugalla, Itundu na Vumilia Wilayani Urambo ambapo ujenzi wa minara unaendelea na utakamilika ifikapo Julai 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imepanga kufikisha huduma za mawasiliano ya simu Kata za Kiloleni,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kasisi, Itundu na Uyogo katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 baada ya kubaini uwepo wa changamoto za mawasiliano katika baadhi ya maeneo ya vijiji katika kata hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hizo zimejumuishwa katika zabuni inayotarajiwा kutangazwa kabla ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 kukamilika kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali. Utekelezaji wa miradi hii ya usimikaji wa minara ya mawasiliano utahusisha uboreshaji wa mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa huduma za intaneti katika Kata za Songambele na Imlalamakoye asante.

MWENYEKITI: Asante, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta swali la nyongeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kwanza nimponeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini ye ye mwenyewe anaewa kwamba kuna kata tisa. Kwa hiyo ukiangalia idadi ya kata ambazo zinashughulikiwa bado nyingi zitakuwa na matatizo yale yale ambayo yanaendelea na kuwapa shida wananchi.

Je, Serikali, kutohana na umuhimu wa mawasiliano kwa upande wa kiuchumi na kijamii, inatoa tamko gani la kuwapa matumaini kata zile ambazo bado zina matatizo ya mawasiliano?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer Andrea Kundo*.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimponeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya wananchi wa Urambo, na kwa kweli

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ameonesha ushirikiano mkubwa pale ambapo Serikali inapohitaji msaada wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, ni kwamba tunatambua kabisa kwamba kuna changamoto ya mawasiliano katika Jimbo hili la Urambo ambapo jimbo hili lenye kata 18; na katika hizo kata 18 kata tisa ndizo ambazo zina changamoto, si kwamba hazina mawasiliano, zina changamoto. Kata hizo ni; Kata ya Uyumbu, Muungano, Vumilia, Busoke pamoja na Songambele. Kata zote hizo tunafahamu kabisa kwamba zina changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Serikali kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigital tayari tumeanza na kata tatu. kwa hiyo tunaamini kabisa kwamba tunapoenda katika utekelezaji wetu tukishakamilisha kata hizi tatu tunaamini hata zile kata sita ambazo zimebaki tutazifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.
(Makofii)

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa Oliver Semuguruka swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Changamoto kubwa inayokabili wananchi wa Ngara ya mawasiliano ya simu ni kuingiliana na nchi jirani za Rwanda na Burundi.

Ninataka kujua, ni nini mkakati wa Serikali ili kutatua changamoto hiyo?

MWENYEKITI: Asante kwa swali fupi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka Mbunge wa Viti Maalum Kagera kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kabisa kwamba ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge huyu ameendelea kuwa msumbufo kweli kweli kwa ajili ya kuhakikisha maeneo hayo yanatafutiwa ufumbuzi. Lakini vilevile natambua pia usumbufu ambao nimeendelea kuupata kutoka Mbunge wa Jimbo la Ngara Mheshimiwa Ndaisaba kwa sababu haya maeneo tuliyatemebelea na tukagundua kabisa kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo; ya kwanza, si kwamba hatuna minara, kuna maeneo ambayo tuna minara lakini nguvu yake haikuwa inatosha. Hivyo tulitoa maelekezo kwa watoa huduma kuhakikisha kwamba minara yao inakuwa na nguvu ili huu mwingiliano usitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna maeneo mengine ambayo hatukuwa na minara ndiyo maana mwaka jana sasa kupitia mradi wa *special zone* na *borders*, yaani mipakani na maeneo maalum, tulihakikisha kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo tunaenda kujenga minara yakiwemo maeneo ya Ngara ambapo kuna miradi tisa ambayo inaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Asante. Mheshimiwa Salome Makamba swalii la nyongeza.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya changamoto ya mawasiliano ambayo Mheshimiwa Waziri anakiri watu wamekuwa wakinunua bando, kwa sababu ya kuingia na kutoka kwa *internet* mtu anajikuta bando lake lina-expire kabla wakati hajalitumia. Sasa, kwa sababu hiyo, Je, Serikali haioni ipo haja ya kutengeneza utaratibu bando liwe linachajiwa kwa matumizi kwamba linaisha kwa sababu umetumia badala ya kuchajiwa kwa sababu muda wa lile bando umekwisha?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salome Makamba Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kulikuwa na changamoto hiyo lakini Serikali ikalitambua hilo na njia pekee ya kutatua changamoto hiyo ni Serikali tulitoa maelekezo ya kuhakikisha miradi yote inayojengwa nchini sasa inajengwa ikiwa na uwezo wa kutoa huduma ya *internet* hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tulibadilisha kanuni zetu pale ambapo unaona kabisa kwamba muda wako unaelekea kuisha lakini bando lako bado linatosha inawezekana ulikuwa umesafiri ukaenda sehemu ambayo haina *internet* basi utapata fursa ya kuhamisha au kuijunga na kifurushi kingine lakini na ile *balance* uliyokuwa nayo unai-*carry forward*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kupitia hizi njia ambazo Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba inaboresha huduma ya mawasiliano tunaamini kabisa kwamba kupitia njia hizi na mabadiliko ya kanuni zetu itawezesha wananchi kutumia bando lao na mpaka linaisha. Ahsante.

MWENYEKITI: Asante Mheshimiwa Jafari Chege swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kata ya Roche, Ikoma, Bukura pamoja na Goribe ni mionganoni mwa kata ambazo ziko mpakani kati ya Tanzania na Kenya. Mheshimiwa Waziri nafikiri ulipata ridhaa ya kuzitembelea kata hizi ukaona hazina mnara na hakuna mawasiliano yote katika kata hizi. Nilitaka njue katika zile minara ambayo umesema wanaitangaza mwezi Juni kama kata hizi nazo zinapata nafasi ya kutangaziwa ili waweze kupata mnara kuboresha na kuweka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mawasiliano kwenye maeneo haya ya mpakani na kimkakati?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chege Mbunge wa Rarya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Mheshimiwa Chege kwa sababu tumekuwa tukishirikiana vizuri sana; na maeneo na kata ambazo amezitaja Mheshimiwa chege tulishafika katika maeneo hayo. Vilevile katika mpango wa utekelezaji wa Tanzania Kidigitali tayari maeneo haya tumeyaingiza na Mheshimiwa Chege tayari anafahamu hilo. Kwa hiyo, kilichobaki sasa ni utekelezaji tu na tayari mkandarasi yuko tayari kwa ajili ya kuanza kazi mara moja kwa ajili ya maeneo hayo katika Jimbo la Rarya. Ahsante.

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa *Engineer Andrea Kundo Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari* kwa majibu mazuri. Sasa tunakwenda Wizara ya Maliasili na Utalii namwita Mheshimiwa Erick Shigongo Mbunge wa Buchosa aulize swali lake.

Na. 193

Tatizo la Mamba Jimboni Buchosa

MHE. ERIC J. SHIGONGO aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itazuia Mamba wanaoua watu na kujenga uzio wa nondo maeneo ambayo watu huchota maji Jimboni Buchosa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo Mbunge wa Jimbo la Buchosa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na matukio mbalimbali ya wanyama wakali kujeruhi au kusababisha vifo vyta watu pembezoni mwa maeneo yenye maziwa, mito na mabwawa hususani mamba. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Migongano baina ya Binadamu na Wanyama wakali na waharibifu. Aidha, kuanzia kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 jumla ya mamba wawili wamevunwa katika Kata ya Maisome Wilayani Buchosa. Vilevile, katika kipindi tajwa watu 992 wamepewa elimu kuhusu namna ya kuepuka madhara ya wanyama wakali na waharibifu. Hadi sasa kikosi cha Askari wa Uhifadhi watatu wapo uwandani wanaendelea na doria za kudhibiti mamba katika Wilaya ya Buchosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazishauri Mamlaka ya Serikali za Mtaa (Halmashauri) kuandaa mpango madhubuti wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vizimba na Wizara ya Maliasili na Utalii itatoa wataalam.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Erick James Shigongo swali la nyongeza.

MHE. ERICK J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni kweli Mamba wawili walikutwa wamekufa ziwani, si kwamba walivunwa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, na kwa kuwa akina mama wananchi wa Buchosa bado wanaendelea kuliwa na Mamba mpaka sasa; swali la kwanza;

Je, Waziri anaweza kuchukua hatua kwa watumishi wake ambao nina uhakika kwamba wamemdanganya ili jambo hili lisitokee siku nyngine?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wananchi wa Buchose wanahitaji *commitment* ya Serikali ya kwamba ni lini sasa vizimba hivi vitajengwa ili kuokoa maisha yao wakati wanateka maji? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eric James Shigongo Mbunge wa Jimbo la Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Erick Shigongo kwa kuendelea kufatilia eneo hili ambalo kumekuwa na changamoto ya wanyama wakali hususan mamba. Ni kweli alikuja na alimwona Mheshimiwa Waziri, lakini pia tulipeleka askari kule, wamekuwa wakifatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikidhibitika kweli kwamba hawa askari wamedanganya kwamba hawakwenda na wale mamba wamekutwa wako pembeni wamekufa, hatua za kinidhamu na za kiutumishi ninamwelekeza Katibu Mkuu azichukue haraka mara moja; kama itathibitika tu kwamba hawa askari wamedanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii tumekuwa tukijenga vizimba vya mfano kuonyesha namna ambavyo hawa wanyama wanaweza wakadhibitiwa na wananchi wakaendelea na shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi tu kwamba tutapeleka wataalamu wataenda kujenga kizimba cha mfano ambacho kanda ya ziwa pia wataenda kujifunza pale. Lakini kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba kwa kuwa haya maeneo kwa asilimia kubwa yanamilikiwa na Serikali za Mitaa zikiwemo Halmashauri. Tunazielekeza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Halmashauri ziweze kutenga fedha kwa ajili ya kujenga vizimba ili kusaidia hawa wananchi waendelee na shughuli za kibinadamu, ahsante.

MWENYEKITI: Asante Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mbunge wa Korogwe Vijijini swali la nyongeza.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tangu mwaka 2019 mpaka sasa watu watatu wamethibitika kufa kwa sababu ya tembo kwenye kata za Mkomazi na kata za Mkumbara kule Korogwe Vijijini na sasa hivi tunapozungumza hali ya uharibifu wa mazao ni kubwa sana. Ni upi mkakati madhubuti wa Serikali kuhakikisha kwamba tunawasaidia wananchi wetu kudhibiti tembo na wanyama wengine wasiendelee kuathiri mazao lakini na maisha ya wananchi wetu? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali la yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli wiki iliyopita tu tulikuwa tuna changamoto ya tembo ambao walivamia katika maeneo ya mashamba ya katani na mashamba ya mipunga, lakini tulipeleka askari.

Changamoto iliyopo ni kwamba wale askari walikuwa ni wachache. Lakini nimuahidi Mheshimiwa Mnzava wananchi wa Korogwe zoezi linalofuata sasa hivi ni kwamba tumeamua kutafuta askari wa ziada ambao tutakuwa tunawaajiri kwa muda ili kuongeza nguvu katika maeneo ambayo yana changamoto ya wanyama wakali ili hawa wananchi katika kipindi cha mwezi wa nne mpaka wa saba waweze kuvuna mazao yao bila tatizo. Hili naliweka ni *commitment* ya Serikali tunaenda kulitekeleza mara moja.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Asia Halamga Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuulizwa swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia simba na tembo wanaoharibu mazao pamoja na mifugo katika Kata ya Magugu pamoja na Vilima Vitatu Jimbo la Babati Vijijini pamoja na Jimbo la Kiteto? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika Kijiji cha Magugu tulikuwa na changamoto ya simba ambayo sisi tulionia ni changamoto ngeni sana kwa sababu tumezoea ni tembo, mamba na viboko; lakini tulipeleka askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tunayoipata ni kwamba hawa wenyeji baada ya kuonesha kwamba mipaka ya hifadhi inakuwa maeneo fulani wenyeji wanaseogea karibu sana wanaweka mazizi kando kando ya hifadhi. Sasa Simba anapotoka cha kwanza anaona kitoweo kiko karibu, kwa hiyo 'mimi niwaombe wananchi wanaoishi maeneo hayo kwamba tunapoweka kando kando ya hifadhi *beacon* hii unaweka zizi la ng'ombe hapa. Na hili limekuwa ni changamoto kubwa kwa sababu hao hao wanatega ikifika maeneo kadhaa basi anaingiza hata ng'ombe hifadhini anaweza wanapata chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe wafugaji, kwamba kuweka zizi kando kando ya hifadhi ni kuleta hatarishi ya wanyama wakali kusababisha kuliwa hii mifugo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na wanyama hatarishi kama simba. Lakini tumeendelea kutoa ushirikiano na askari wataendelea kuwepo katika maeneo hayo ili kudhibiti simba wanaotamani kula mifugo.

MWENYEKITI: Prof. Ndakidemi swali la nyongeza.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la kima, ngedere na nyani kwa vijiji vinavyopakana na Mlima Kilimanjaro na wanyama hawa wamekuwa wanasababisha uharibifu mkubwa sana wa mazao ikiwa ni pamoja na kula kuku na kusababisha umaskini.

Je, Serikali ina mpango gani kusaidia wananchi wetu kukabiliana na changamoto hii?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Moshi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyezekiti, ni kweli kuna changamoto ya ngedere, nyani na kadhalika katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro; lakini tumeanzisha utaratibu wa kugawa miti ambaao tunatarajia kuanza ili kuwepo na upandaji wa miti katika maeneo ambayo tunaamini haya tukiweza kuyazuia na kuyahifadhi vizuri basi wanyama hawa wataweza kuishi maeneo salama zaidi kuliko ilivyo sasa ni kweupe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, lakini kwa wakati huo huo tulishaahidi kwamba hawa ngedere tutatafuta namna ya kwenda kuwapunguza na kupeleka katika maeneo mengine ya hifadhi. Hilo nimuhahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalitekeleza. Ahsante.

MWENYEKITI: Kwenye Wizara hii swali la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Shangai Mbunge wa Ngorongoro.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swalii; kwamba kwenye kata za Swali Sambao, Lweipiri na Ololosopan, tembo wamekuwa wakiharibu mazao pamoja na kuumiza wananchi.

Je, Serikali ina mkakati upi wa kuhakikisha kwamba wananchi wale wanafidiwa?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Shangai Mbunge wa Ngorongoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu mwanzo, kwamba sasa tuna mpango wa kuangalia namna ya kuwa na askari wa kutosha ili kipindi kile ambacho ni cha migogoro kati ya binadamu ya wanyama wakali, basi hawa askari waweze kuelekea katika maeneo hayo na kudhibiti hawa wanyama wakali. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Maliasili ya Utalii sasa namuita Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge wa Viti Maalum aulize swalii lake.

Na. 194

Kukuza Utalii wa Fukwe za Bahari Nchini

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukuza utalii wa fukwe za bahari nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, aliijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kubuni mikakati mbalimbali ya kuendeleza Mazao mbalimbali ya Utalii, ikiwemo Utalii wa FUKWE. Katika kutekeleza mikakati hiyo, Idadi ya Watalii wanaotembelea fukwe zetu zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara imeendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na hilo, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

- i. Kwanza ni kubaini maeneo mapya ya fukwe za Bahari ya Hindi yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji wa shughuli za utalii katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara;
- ii. Lakini pia kuweka utaratibu wa kusajili maeneo ya fukwe yanayofaa kwa shughuli za Utalii kama Maeneo Maalum ya Uwekezaji wa Shughuli za Utalii (*Tourism Special Economic Zone*); na
- iii. Lakini la mwisho ni kuendelea kuwashamasisha wamiliki wa maeneo ya fukwe nchini ili kusajili maeneo ya fukwe wanayoyamiliki chini ya utaratibu wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji wa Shughuli za Utalii kwa lengo la kuiwezesha Serikali kushirikiana na wamiliki hao kuhimiza uwekezaji wa utalii wa fukwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tunza Issa Malapo swalii la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nataka tu kujua wanasema kubaini maeneo mapya ya uwekezaji kwani yale ya zamani Mheshimiwa Waziri mmeayaendeleza? Hilo swalii langu la kwanza?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule kwetu Mtwara hususan wilaya ya Mtwara ambayo inahusisha Jimbo la Mtwara mjini na Mtwara Vijiji kuna fukwe nzuri sana ambayo ikiendelezwa itavutia utalii na hivyo kusababisha shughuli za maendeleo pale Mtwara zipatikane sasa swali langu. Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wanatangaza fukwe zile zinaendelezwa ili watalii waje? nakushukuru.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Tunza kwa kuliona hili na mimi niseme tu kwamba haya maeneo ambayo ni maeneo ya fukwe kwa asilimia kubwa yanamiliikiwa na Serikali za Mitaa lakini pia na wananchi binafsi. Kwa hiyo sisi tumekuwa tukitafuta wawekezaji lakini baada ya kutafuta wawekezaji tunawapeleka katika wamiliki ambao wanamiliiki haya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo baada ya *Royal Tour* ambayo Mheshimiwa Rais, tunamshukuru sana, ameizindua na pia kutafuta wawekezaji tumetengeneza namna na mbinu bora ya kuwakanishwa sasa hawa wamiliki wa maeneo haya na kuyaweka wazi na kuyasajili ili sasa kuwepo na uwezekano ukipata mwekezaji basi unamuonyesha tu kwamba nenda hapa.

Kwa hiyo nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi Serikali inayashughulikia kwa ukaribu na hivi punde tutaanza kuwaona wawekezaji wengi wanaenda kwenye maeneo haya na tutahakikisha wanayapata kwa sababu tayari tumeshaanza kuyasajili na wamiliki wameshakuwa wazi na wameshaanza kuiona Serikali na tayari tuna mpango mzuri ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asya Mohammed swalii la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa nchini kuna maeneo ya fukwe ambayo yameendelezwa kiutalii, lakini maeneo haya yanakabiliwa na changamoto kubwa ya uchafuzi wa mazingira.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyahifadhi maeneo haya ili kuweza kuwavutia watalii nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asya Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo tunapeleka watalii lazima yawe ni masafi yenye kuvutia ili tuendelee kupata watalii. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye yale maeneo ambayo yanaonekana yana changamoto hizo Serikali itaendelea kuchukua hatua ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yanavutia na wawekezaji na watalii waendelee kuja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ni muda mrefu Nyanda za Juu Kusini tumekuwa tukiainisha vivutio vipyta mbalimbali vya utalii, lakini vile vile Nyanda za Juu Kusini tumebarikiwa kuwa na hifadhi ya kipekee ya Kituro ambayo hifadhi hii ulimwenguni ni aina ya kipekee, hakuna ambayo inafanana nayo.

Je, Serikali mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba mnakuza utalii wa nyanda za juu kusini?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja majibu kwa swali hili muhimu sana.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Neema kwa kuendelea kuhamasisha utalii na hili ninalisema kwa dhati kabisa kwa sababu sasa hivi *focus* yetu ni kuelekeza kwenye Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa *REGROW* ambaao ulishaanza tayari na tayari ni mradi ambaao una madhumuni ya kuboresha maeneo ya Nyanda za Juu Kusini hususan miundombinu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kuwa Kaskazini sasa hivi tunaelemewa watalii nikimaanisha kwamba ukipeleka watalii 1000 tayari kule kuna *jam*; *focus* ya Serikali ni kuelekeza hawa watalii sasa warudi nyanda za juu kusini na maeneo mengine na ndiyo mkakati wa Serikali. Nimhakikishie kwamba uhamasishaji unaoendelea sasa hivi ni kuwekeza lakini pia na kuhamasisha utalii katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini.

Kwa hiyo hili tumeliona na tunaendelea kulitengenezea mkakati madhubuti. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja sasa unaweza kwenda kuketi. Tunakwenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ninamuita Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali llake.

Na. 195

Ujenzi wa Barabara za Mkoa wa Manyara

MHE. YUSTINA A. RAHHI aliuliza: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara za Dareda – Dongobesh, Katesh – Haydom, Karatu – Mbulu – Haydom – Singida na Babati hadi Orkesumet kama ilivyoainishwa katika llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Eng/neer* Kasekenya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara za Dareda – Dongobesh (km 60), Katesh – Hydom (km 70), Karatu – Mbulu – Hydom – Singida (km 246) na Babati - Orkesumet (km 145). Kwa kipande cha Mbulu – Garbab chenye urefu wa kilometra 25, taratibu za zabuni ziko kwenye hatua za mwisho za kusaini mkataba. Kwa kipande cha kutoka Garbab – Muslur chenye urefu wa kilometra 25 maandalizi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi yako kwenye hatua za mwisho. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu zilizobaki. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi Mbunge wa Viti Maalum swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naishukuru pia Serikali kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, naipongeza Serikali kwa barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom, kipande kinachoanza Mbulu Garbab, kipande cha kilomita 25 taratibu za manunuzi zimeanza tangu Mei, 2021 na hadi sasa haujakamilika. Sasa wananchi wa Mbulu hamu yao ni kuona kwamba barabara hiyo inajengwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini taratibu hizo zitakamilika na ujenzi huo uanze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii langu la pili, barabara hizo nilizozitaja, Barabara ya Dareda, Dongobesh, Kartesh Hydom, Babati Orkesumet kuptitia Galapo ni ahadi ya Serikali kwa wananchi wa Manyara ya muda mrefu. Lakini vile vile ni ahadi ya viongozi wa Serikali wakati wa kampeni. Ni barabara ambazo ziko kwenye llani ya Chama.

Sasa, ni lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa barabara hizo? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi kwa jinsi anavyosaidiana na Wabunge mbalimbali wa Mkoa wa Manyara ambao barabara hizo zinapita kwenye Majimbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametaja karibu barabara za mkoa mzima wa Manyara. Mimi nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipande alichokitaja kwenye swalii lake la kwanza la Mbulu Garbab zabuni ilishatangazwa na sasa hivi tuko kwenye hatua ya kusaini mkataba; kwa hiyo siyo hadithi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipande cha pili cha Garbab Muslur tayari tumeshandaa zabuni na inatangazwa muda wowote. Kwa hiyo tutahakikisha kwamba kipande hiki cha kilomita 50 katii ya Mbulu na Hydom kitajengwa. Kwa barabara zingine alizozitaja ya Hydom - Katesh tayari tulishafanya usanifu wa awali na tunaendelea usanifu wa kina. Dongobesh – Dareda tayari tumeshakamilisha usanifu wa kina.

Vilevile Babati kwenda Galapo hadi Orkesmet barabara hii tunaendelea kuifanyia usanifu ili sasa tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa wa Mkoa wa Manyara kwamba Serikali iliahidi na hatua zinaendelea kufanyika kuhakikisha kwamba ahadi zinatekelezwa kama zilivyo kwenye llani, lakini pia tunajenga hizo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Agnes Marwa swali la nyongeza.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya ya Rorya ni kati ya wilaya ambazo ziko nyuma sana kimaendeleo kutokana na changamoto ya miundombinu. Sasa;

je Serikali haioni kuna ulazima wa kuanza ujenzi wa barabara inayopita Mika, Utigi, Shirati hadi Kirongo; ukizingatia ni muda mrefu sasa, tangu 2017, 2018 ikiwa inafanyiwa upembuzi yakinifu?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara aliyoitaja inayoanzia Utigi katika Jimbo la Rorya ipo kwenye mpango wa kufanyiwa usanifu ili ikishafanyiwa usanifu tujue gharama halafu Serikali kama ilivyo kwenye llani tuweze kupata gharama na tuanze kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Oral Njeza swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kuwa barabara ya Ishonje, Kikondo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuelekea Makete kwa muda mrefu sasa imekuweko kwenye bajeti ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini sasa hiyo barabara, hususan kipande cha Ishodye, Kikondo kuelekea Makete, itajengwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekitti, Barabara aliyoitaja ya Ishonje Kikonde Makete ilitangazwa kilomita kama 25 halkupata mkandarasi. Lakini imetangazwa tena ambapo sasa tumeongeza hata kilometra siyo tena 25 ni kilomita kama 50, na ni mwendelezo wa barabara ya kutoka Njombe, Makete kuja Ishondye ambayo inaunganisha mkoa wa Mbeya na mkoa wa Njombe. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari barabara hii imeshatangazwa na ni taratibu tu za manunuzi ambapo tutaanza kuanzia Makete kuendeleza kwenda kuunganisha na mkoa wa Mbeya. Ahsante.

MWENYEKITI: Dkt. Ishengoma, swali la nyongeza.

DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swali dogo. Barabara ya kuanzia Kilosa, Lumuma Mpwapwa Ulering'ombe mpaka Ruaha ni mbovu sana.

Je, ni lini angalau itafanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara zote za *TANROADS* zinatengenezwa kwa kiwango cha changarawe. Kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo katika mwaka huu wa fedha tutahakikisha kwamba tunaitengeneza kama kuna sehemu ina udongo tutahakikisha kwamba tunapeleka fedha ili tuweze kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupidika muda wowote ili kutoa huduma bora kwa wananchi wahusika, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya lleje hivi karibuni tumeona namna gani maafa yamekuwa yakinoteka kutokana na maporomoko yanayotokea katika barabara ya Ikuti, Sange, Katengele, Kafule mpaka Ikinga. Nilitamani kufahamu ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha barabara hizi zinajengwa kwa kiwango cha lamī? Ahsante

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara alizozitaja za kuanzia Isongole, Ibungu, Katengele hadi Kimo ambayo inaunganisha lleje na Wilaya ya Rungwe; lakini pia barabara za Isongole, Ibungu, Malangali, Ikinga hadi Kasumulu zinazouanganisha Wilaya ya lleje na Kyela ni barabara ambazo zinapita kwenye miinuko na ni kweli kulitokea maporomoko

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

makubwa sasa mimi mwenyewe nilienda kwasababu zilikuwa zimefunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachoendelea sasa hivi ni kwamba ni kuzifanya usanifu wa kina barabara ya Isongole, Ibungu, Malangali, Ikinga hadi Kasumulu ili kufanya maandalizi kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami. Lakini hatua ambazo zimechukuliwa kwa sasa ni kuondoa vile vifusi ili barabara ziweze kufunguka maana yake zilikuwa zimefungwa na nisema tu katika haya maporomoko tulipoteza watu watano baada ya kutokea *land slide* kwa hiyo unawenza ukaona lakini barabara ya kutoka Ibungu kwenda Tukuyu tutaainisha maeneo korofii ili yaweze kufanyiwa matengenezo maalum na barabara hiyo iweze kuitikia kwa kipindi chote cha mwaka, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Kasekenya Msongwe kwa majibu yako tunaendelea na Wizara ya Afya sasa namwita Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 196

Vifo vya Akina Mama – Mwanza

MHE. KABULA E. SHITOBELO aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza kabisa tatizo la vifo vya akinamama katika Mkoa wa Mwanza?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Dkt. Mollel.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali ya Mheshimiwa kabula Enock Shitobelo Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeimarisha huduma za akina mama kujifungulia katika vituo vya huduma katika Mkoa wa Mwanza kwa kujenga vituo vya afya 22 vinavyotoa huduma za upasuaji, na inaendelea na ujenzi wa vituo vya afya 15 vitakavyotoa huduma za upasuaji mara vitakapokamilika. Aidha, serikali imeimarisha utoaji wa elimu ya Afya ya uzazi kuhusu viashiria vya hatari kwa akina mama wajawazito na kupitia ajira mpya zilizotangazwa itapeleka wataalamu zaidi ili kuhakikisha akina mama wajawazito wanapata huduma sahihi kutoka kwa wataalamu, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabula Shitobelo, swalii la nyongeza.

MHE. KABULA E. SHITOBELO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, je, sasa Serikali imeshafanya utafiti kujua ni watumishi wangapi wataapeleka, na je, kwenye hizi ajira mpya watapeleka watumishi wangapi kwa ujumla? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake *specific* kwa Mkoa wa Mwanza kwamba tutapeleka watumishi wangapi, labda tu nimwambie kwamba inajulikana kwamba kwenye *level* ya zahanati wanahitajika watumishi wangapi, kwenye *level* ya kituo cha afya inahitajika watumishi wa wangapi kwenye *level* ya hospitali ya wilaya wanahitajika watumishi wangapi mpaka tunapofika Taifa. Lakini kama kawaida kutokana na bajeti na uwezo wa Serikali imekuwa si rahisi kuhakikisha tunawapata wote kwa wakati mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali ilitangaza juzi ajira 32,000 nimuombe Mheshimiwa Mbunge ili nisipe nikamwambia data ambazo si sahihi tuje tukae tuangalie specifically Mkoa wa Mwanza kwenye ajira hizi wanapata watumishi wangapi kwenye eneo hilo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mabula swalii la nyongeza.

STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kujua. Pamoja na maandalizi ya vifaa kwenye vituo vinavyojengwa, tunavyo takribani vituo vinne ambavyo vimeshakamilika; kule Igoma, Fumagila, Bulale pamoja na Nyengezi;

Ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kupeleka vifaa kwenye vitu hivi ambavyo viro tayari na kuanza kutoa huduma? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele sasa cha Wizara ya Afya na Waziri wa Afya ameshaelekeza wataalam wote, kwamba vituo vingi sasa vimeshakamilika na ujenzi wa kwa kiasi kikubwa sasa umeshafanyika.

Sasa kipaumbele cha kwanza ni kuhakikisha kuwa vituo ambavyo viro tayari vinaanza kazi na kuhakikisha vina vifaa na watumishi. Kwa hiyo ndani ya mwaka huu kabla ya mwezi wa 10 vituo vyote vitakuwa vimepata vifaa tiba na vitakuwa vimeanza na wataalam watakuwa *site*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnes Hokororo, swalii la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza kutupa mrejesho wa vifo vya uzazi vinavyotokana na uzembe ili tuweze kuwa na imani kwamba Serikali inafuatilia? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kila kifo kinachotokea cha mama anayejifungua huwa kinajadiliwa. Sasa, anasema kwamba ni lini wataanza kutupa mrejesho; kwakweli ni kazi yetu pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwetu Mheshimiwa Waziri wa Afya ameshaelekeza, na kwamba tumegundua watu kama *Red Cross* wana mtandao mkubwa sana kutoka taifa mpaka tunafika kwenye vitongoji vyetu na ni mtandao wa kijamii. Tunafikiri kwamba tukiwashirikisha hao, tunataka sasa, kama ilivyo elimu, kwenye vituo vyetu vya afya na zahanati zetu kuwepo na *ownership* wa kijamii, kwamba kila tatizo linapotokea liwepo wanajamii wanajadili inajulikana kwenye jamii na *information* zinaenda vizuri kwenye jamii. Kwa namna hiyo tutaweza kupunguza vifo vya akina mama

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile sisi wanaume tunahitaji kuwa na *ownership* ya ujauzito wa akina mama tangu mama anavyobeba mimba tuweze kushirikiana na mama mpaka siku anapojifungua. Tukifanya hivyo nayo itatusaidia vizuri sana kwasababu kila baba anapenda kujisifia mtoto wake ambaye anafaulu vizuri shuleni, lakini kufaulu kwa mtoto vizuri shuleni kunaendana vilevile na kuanza kutunza mimba toka siku mimba inavyobebwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo akinababa kama tunapenda watoto wafanya vizuri shuleni wawe *brilliant* kwenye maisha tuanze na mimba siku mama anapobebea ujauzito. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna hiyo suala la afya litakuwa sio suala la wataalam wa Afya peke yao, litakuwa suala la kijamii. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Takwimu zinaonesha Watanzania takribani milioni kumi na tano, sawasawa na asilimia 34.2 ni maskini kabisa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa kadri ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais ili akina mama wajawazito waweze kupata huduma ya afya na kupunguza vifo vyao?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jibu swali zuri la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kama mnavyojua Wabunge, tayari kwenye Kamati ya Bunge ya huduma na Maendeleo ya Jamii tumewaelezea na tumewafafanulia hatua tulizozifikia kwenye suala zima la bima ya afya. Na nafikiri Bunge zima limeshaelekeza sisi Wabunge tuna uchaguzi. Kwa sababu ukiangalia mtu anaweza akasubiri akaacha kuweka luku kwenye nyumba yake umeme usiwepo na akasubiri kesho lakini akiugua haiwezi kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaweza akaamka akiwa na afya yake kufuata maji mbali zaidi, lakini afya hawezi hata iliyopo ndani ya nyumba yake hawezi.

Kwa hiyo ni uchaguzi wetu, tutakapoleta Mswada tuamue tunapata vyanzo gani ambavyo vitatusaidia kuweza kuweka kwenye mfuko wa afya; tupate bilioni 149.77 ambazo zitatusaidia na kuwasaidia wale Watanzania wasiweza kujilipia mfuko wa mima ili sasa tufikie hatua ya sisi kuanzisha bima ya afya kwa wote. Ahsante sana Wabunge. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako, sasa unaweza kwenda kuketi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Maswali na majibu; hapa naomba kutambulisha wageni

Naomba nianze na wageni 10 wa Mheshimiwa David Kihenzile Mbunge ambao ni rafiki zake kutoka Dodoma na Dar es Salaam wakiongozwa na Bwana Raphael Banzi, mke wake pamoja na Mhandisi Tumaini Mbwambo, Raphael Riela na wengine wote, karibuni sana Bungeni. (*Makofii*)

Aidha, wageni 53 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula (Mb) ambaye ni Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni wanakwaya wa kwaya ya Mtakatifu Joseph kutoka Parokia ya Ilemela Mkoani Mwanza wakiongozwa na Ndugu Francis Mabula. Karibuni sana watumishi wa Mungu.

Wageni 11 wa Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mb) Waziri wa Maji ambao ni watumishi wa Wizara ya Maji, Makatibu wa Waziri, Makatibu Mhutasi wa Wizara ya Maji pamoja na Dereva wa Waziri kutoka jijini Dodoma. Karibuni sana mnaomsaidia Mheshimiwa Waziri kwenye kuchakata suala la maji kwenye nchi yetu. (*Makofii*)

Wageni wengine saba wa Mheshimiwa Waziri Aweso ambao ni ndugu zake kutoka Pangani Mkoani Tanga. Karibuni sana kwa kutuletea pia Mbunge ambaye ni Waziri anachapa kazi vizuri hapa.

Wageni 35 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini Mbunge, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni viongozi wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Neema Mkwachu. karibuni sana. Sijui kama naona vizuri naona kama kuna Mzee Mavunde au naona vibaya? Karibu sana mzee wetu, karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga (Mb) Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambaye ni Mhadhiri kutoka chuo kikuu cha Arusha Dkt. David Wanani.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi Mbunge ambao ni wapiga kura wake kutoka Lushoto Mkoani Tanga, ambao ni pamoja na ndugu Gasper Shekigenda pamoja na Sylvester Ngota. Karibuni sana, bila shaka nanyi mtakuwa mnahusika kwenye yale mambo yetu aliyokuwa anatutengenezea kipindi kile. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya (Mb) ambaye ni Mkurugenzi wa *Capacity and Institutional Strengthening (FHI 360)* Dkt. Beatus Leon. Yupo wapi, tumtambue huyu Dkt. Beatus Leon *okey*, wageni wengine wa Mheshimiwa Chaya, ni walimu kutoka Nkonko Sekondari ambayo iliongoza kiwilaya matokeo ya kidato cha nne. Hongereni sana. Pia wameambatana na viongozi wa Kata ya Nkonko kutoka Manyoni Mkoani Singida; Viongozi wa Kata, ahsanteni sana kwa kusimamia maendeleo ya kata yetu. (*Makofi*)

Wageni 31 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga (Mb) ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Vwawa Wilayani Mbozi Mkoa wa Songwe. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, na hongereni kwa kuendelea kufanya kazi ya kumsaidia Mheshimiwa na kumlindia Jimbo akiwa huku. Wanaongozwa na Ndugu George Msyani ambaye ni mwenyekiti wa Halmashauri. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka (Mb) ambao ni kaka zake kutoka Karagwe Mkoani Kagera. Karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa (Mb) ambaye ni ndugu Ishaq Mohamed Ame kutoka Zanzibar. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dennis Londo (Mb) ambao ni mdogo wake na rafiki zake kutoka Jijini Dodoma. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Daimu Mpakate (Mb) ambaao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam; Ndugu Silvanus Mumba pamoja na ndugu Isdory Kiteve. Karibuni sana.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Sylvia Sigula Mbunge ambaao ni viongozi wa Jukwaa la hedhi salama Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Katibu wa Jukwaa la hedhi salama Tanzania Ndugu Severine Allute. Karibuni sana sana sana. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke (Mb) ambaye ni mdogo wake kutoka Kasulu Mkoani Kigoma, Ndugu Oliver Gaston. Ahsante sana.

Wageni 10 wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava (Mb) ambaao ni viongozi wa vyama vya Ushirika wa Mkonge kutoka Jimbo la Korogwe Vijiji Mkoani Tanga, karibuni sana. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Geoffrey Mwambe (Mb) ambaye ni mdogo wake; Mheshimiwa Nestory Chilimba ambaye ni Diwani wa kata ya Mwena Wilaya ya Masasi; karibu sana bwana Chilimba; pamoja na wenyeviti nane wa vyama vya msingi (*AMCOS*) kutoka Masasi Mjini Mkoani Mtwara. Karibuni sana. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Mkundi (Mb) ambaye ni mwanasheria wa taasisi inayoambatana na mimba za utotonii, Ndugu Naima Said. Karibu sana. (*Makofii*)

Aidha wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na wanafunzi 25 na walimu sita kutoka shule ya msingi Autonia ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Antonia Donard. Karibuni sana wanafunzi pamoja na walezi ambaao ni walimu. (*Makofii*)

Wanafunzi 55 kutoka chuo kikuu cha Jordan cha Mkoani Morogoro karibuni sana wanafunzi kutoka Morogoro chuo kikuu cha Jordan. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wageni saba kutoka shirika la Ndege *Precision* kutoka jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo ndugu Patrick Mwanri. Karibuni sana sana sana.

Wageni wawili ambao ni watumishi wa Shirika la Bima la Taifa kutoka Makao Makuu ya Dar es Salaam, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge hapa kuna matangazo mengine mawili; tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Spika; anasema uwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Shirika la Bima la Taifa wameweka panda lao la Maonesho eneo la Bunge nyumba ya Ukumbi wa Msekwa na wanaendelea kuwepo hadi tarehe 18 Mei, 2022. Waheshimiwa Wabunge na watumishi mnaombwa kwenda kupata maelezo kuhusu masuala ya bima mbalimbali.

Vilevile watatoa mada kuhusiana na masuala ya Bima tarehe 18 Mei, 2022 saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Aidha, kuna tangazo hapa kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club*. *Bunge Sport Club* inawatangazia waheshimiwa Wabunge kuwa tarehe 14 Mei, 2022 kutakuwa na mechi za kirafiki za mpira wa miguu (*football*) na mpira wa pete (*netball*) kati ya *Bunge Sports Club* na Iringa *All Stars Veterans*. Mechi hizi zitachezwa katika viwanja vifuatavyo:-

i. Mpira wa Miguu utakuwa kiwacha cha *Fountain Gate Academy* kilichopo Mlimwa C.

ii. Mpira wa pete utakuwa kiwanja cha Jamhuri.

Michezo yote itachezwa saa 10 jioni hivyo, Waheshimwia Wabunge wote mnaombwa kujitokeza kwa wingi kushangalia timu zetu. (*Makofii*)

Katibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Tunaendelea na mjadala wa Wizara ya Maji na wachangiaji wetu watakuwa ni hawa wafuatao; wapo hapa, lakini tutaanza na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi akifuaatiwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembwenwe wakati huo Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sanakwa kunipa fursa hii, kwamba leo nimekuwa mchangiaji wa kwanza katika bajeti hii ya Wizara ya Maji, nakushukuru sana. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla yayote naomba kumpongeza Waziri wa Maji pamoja timu yake kwa kazi kubwa anayoifanya ya kujenga miradi mikubwa na kusimamia kwa weledi mkubwa, nampongeza sana Waziri kazi yake inaonekana na akijua wazi kabisa kwamba maji ni uhai na kwamba amekwishasema maji hayana mbadala na kwakweli anatendea haki, nampongeza sana. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba hilo niseme tu, tumshukuru Mungu kwa Tanzania bado tunarasilimali ya maji ya kutosha. Kwa mfano maji yanayoweza kupatikana kwa mwaka ni lita za ujazo bilioni 126, na kati ya hizo bilioni 105 zipo juu ya usawa wa ardhi na bilioni 26 zipo chini ya ardhi; ni maji ambayo yanaweza kupatikana kwa mwaka. Hii inafanya Mtanzania kuweza kutumia maji wastani wa lita 2,250 kwa mwaka, ambapo kiwango cha kimataifa ingekuwa ni lita 1700, na chini ya hapo tungeingia kwenye *water stress*. Kwa hiyo, tunaona kwamba tunabahati pengine kazi kubwa ni namna gani tunaweza kupata maji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo nitoe wito, nimuombe na Waziri kabisa kwamba tunapaswa kuhifadhi vyanzo vya maji ili kwamba kiwango hiki kiendelee kuwepo. Kwa sababu kwa kuharibu vyanzo vya maji pengine kiwango hiki kinachowenza kupatikana kikapungua. Kwa hiyo, akishirikiana na mabonde ya maji nitoe rai kabisa kwamba hifadhi ya vyanzo vya maji ifanyike ili maji yaweze kupatikana kwa watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo Mkoa wa Manyara una changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji. Wakati tukiongelea kwamba Taifa tunaenda kwenye asilimia 72 pengine na kuendelea, ya *coverage* ya upatikanaji wa maji lakini Mkoa wa Manyara bado tuna asilimia 58 pengine na chini. Hali hii ni mbaya zaidi kwa maeneo ya pembezoni, maeneo ya kanda za chini na maeneo ya wafugaji maji ni machache na ukizingatia vyanzo vya kudumu za maji tiririka hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba *tu-focus* sasa ya Waziri iende kwenye maeneo hayo kwa sababu kuna mama zangu kule bado wanatembea kilometra nyingi kutafuta maji. Kwa mfano tu kwenye Wilaya ya Mbulu, ukienda kwenye ukanda wa chini wa Yaeda Chini, Endamilay, Eshkeshi, Masieda hali ya maji kule ni mbaya. Nampongeza kwamba huko pia ameweeka bajeti ya kuchimba visima. Mimi nimuombe tu kabisa kwamba fedha hizi azitoe na visima hivi vichimbwe ili mama zangu waliopo kule waki-Wabarbeig, Wakiiraki wapunguze huu mwendo, kwa sababu kule bado kuna kuamshana wakati wa jogoo la kwanza ili kwenda kukinga maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nimpongeze tu kwa sababu hata Hanang' ana mpango wa kuchimba visima tisa kwenye maeneo magumu kama hayo. Maeneo ya Endagau, Wareta, Dumbeta pamoja na mengine. Maeneo haya ni korofi kwa upatikanaji wa maji na kwamba hakuna vyanzo vya maji tiririka. Vilevile anampango wa kuchimba visima 13 katika Wilaya ya Simanjiro pamoja na kufanya *extension* na mradi mkubwa kabisa ule wa Orkesument

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambao alizindua Makamu wa Rais kwamba sasa anapeleka maji Ruremo kutoka mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kabisa kwamba, katika Wilaya ya Kiteto kuna changamoto kubwa ya maji kwa binadamu hata kwa mifugo na ndiyo maana tunapata vifo vingi vya mifugo. Watu wa Kiteto wameomba kuchimbiwa Bwawa kubwa la Dongo. Bwawa hili lipo kwenye mpango wako na ninaona kwamba mionganini mwa mabwawa ambayo umeyatambua kwamba yanaweza yakachimbwa ni pamoja na Bwawa la Dongo. Mimi nikuombe sana, Bwawa hili la Dongo ni suluhisho kwa watu wa Kiteto wameomba zaidi ya miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bwawa hili faida yake kwanza ni kunusuru mafuriko yanayotokea kule Dumila. *Can you imagine* mvua inanyesha Manyara lakini mafuriko yanaenda mpaka Morogoro, ikiharibu mazao ya watu wa Dumila, miundombinu pamoja na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa hili litakapokamilika lina uwezo wa kusaidia maji katika Wilaya ya Kongwa pamoja na Wilaya ya Gairo; na inakuwa na kazi kubwa, tutapata maji ya binadamu na maji ya mifugo. Mimi unasikia kila siku nikilia na mifugo ya Kiteto inavyokufa wakati wa ukame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile itatumika katika kilimo cha umwagiliaji tukawa na uhakika wa chakula; na tukijua kwamba Kiteto ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula lakini ndiyo yenye idadi kubwa pia ya mifugo. Vilevile itasaidia katika ufugaji wa samani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba hili uliweke katika mpango mkakati kama unavyofanya mikakati ya Farkwa na Kidunda. Hili Bwawa la Dongo ninakuomba sana; litakuwa suluhisho kubwa kwa watu wa Kiteto wote changamoto ya maji itakuwa imeisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ninahamasisha uvunaji wa maji. Nimeona Wizara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wamejitahidi wametengeneza mwongozo wa uvunaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taasisi zetu maji ni ya shida, na lakini ukiona maji ya mvua ni rasilimali muhimu. Kama tungekuwa na tabia ya kuvuna maji ya mvua tungekuwa na uwezo wa kupata maji ya kutosha na kuongeza kiwango cha maji kinachopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule hizi tunakutana na wanafunzi, unaona wanavyobeba maji wakipeleka shulenii, hatujui wamepata wapi vyanzo hivyo vya maji. Lakini uvunaji wa maji ni *project* rahisi wana, miundombinu ya kutosha ya paa, kinachotakiwa pale pengine ni kuweka *matank* ya kuvuna maji na ikawasidia wanafunzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye taasisi za afya, ukienda katika zahanati zilizopo pembezoni bado changamoto ya maji ni kubwa na maji ni muhimu sana kwenye taasisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana, kwa mwongozo huo utaratibu wa uvunaji wa maji katika taasisi uwe kipaumbele na uendeleee; lakini utaratibu wa uvunaji wa maji pia kwa wananchi wa kawaida uendeleee kuhamashisha kuititia kwenye halmashauri zao. Maji ya mvua yakivunwa inaweza kuwa suluhisho kwa maji ya mifugo pamoja na matumizi ya binadamu. Sisi tunaona kabisa pengine miradi ya TARURA na TANROADSikipita wakichimba udongo wao wakaacha yale mashimo kipindi cha kiangazi kinasaidia mifugo, ndiyo maji ambayo yanapatikana.

Sasa kumbe na sisi ukihamasisha wafugaji hata na wakulima wanauwezo mkubwa kabisa wa kuchimba vilambo vidogo vidogo wakaweza kuifadhi maji na kwa hiyo, ikawasaidia kipindi cha kiangazi. Naomba sana, mwongozo huo ukipita kwenye taasisi, lakini vilevile mwongozo huo ufike halmashauri ili wananchi kwa pamoja waweze kuhamashisha kuvuna maji ya mvua yaweze kutumika kipindi cha kiangazi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga hoja mkono kwa mchango wangu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Twaha Ally Mpembewi.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuwa mchangiaji katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza kabisa nilikuwa naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya Tanzania hii katika sekta zote zile ikiwemo sekta hii ya maji vile vile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waislam tunaamini pale kwenye *Quran* kuna aya inasema kwamba *wallahu yarzuku myashau bighairi hisab*; kwamba Mwenyezi Mungu anamruzuku mwanadamu mambo bila hesabu ya aina yoyote ile. Sifa hizi zipo kwa mdogo wangu Aweso. Aweso ni mnyenyeketu, mtulivu, mwadilifu, mchapakazi, anaheshima, na mabega yake yapo chini kila siku. Ndugu yangu endelea kuwa hivyo hivyo chapa kazi na sisi kaka zako tuko nyuma yako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mheshimiwa Waziri anamsemo wake huwa anasema, kwamba ukiona Kobe kapanda katika mti basi kapandishwa huyo si bure. Mimi niseme tu Naibu Waziri anafanya kazi kweli kweli. Nikushukuru sana dada yangu kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuweza kumsaidia Mheshimiwa Waziri na kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa ujumla wake. (*Makof*)

Mhehimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila; katika Wizara hii ya Maji kuna Katibu Mkuu ndugu yangu Sanga. Huyu bwana ni muadilifu kweli kweli huyu bwana ni muungwana kweli anatoa ushirikiano kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wabunge ukimpigia simu anapokea pale ambapo akishindwa kupata simu yako anakutumia *message* na atakwambia samahani kiongozi nilikuwa kwenye mukutano. Katibu wetu Mkuu fanyakazi na mimi niseme tu katika kipindi hiki cha sasa hivi katika Awamu ya Sita Mheshimiwa Rais Wizara ya Maji inakwenda kufanya mabadiliko makubwa sana kwa kuwa na Katibu Mkuu kama ndugu yangu Sanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee mbele. Mkurugenzi wetu wa *RUWASA* anafanya kazi nzuri kwelikweli, Mheshimiwa Rais akufanya kosa kuliona jicho lake pale lakini pale kwangu tuna meneja wa *RUWASA*, kijana yule anafanya kazi safi sana shida yake ni moja tu yule kijana ni Samaki Nchungu anatokea kule Mtwara na wale ni watoto wetu sasa tunashindwa kumpa zawadi pale Kibiti ya kuweza kumpa mke lakini anachapa kazi vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisimama hapa, wakati nimesimama nilikuwa nimeomba fedha katika miradi mbalimbali ambayo iliyokuwa imesimama katika Jimbo la Kibiti. Mheshimiwa Waziri aliniambia kwamba kaka yangu usiwe na wasiwasi tutajitahidi kadri ya uwezo wetu tutapeleka maendeleo kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Mimi ninafaraja kusema tumepeleka fedha katika Mradi wa Mtunda Shilingi milioni 790 mkandarasi yupo *site* nani kama Mama Samia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hivyo haitoshi tumeweza vile vile kupewa fedha pale katika Kata ya Mjawa Shilingi milioni 502 mkandarasi yuko *site*, mabomba yametambazwa katika Kata ya Mjawa utafikiri vile uyoga nani kama Mama Samia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niendelee mbele pale Kilula Tambwe kuna mradi mzuri sana wa maji umepelekwa pale shilingi milioni 452 mkandarasi yupo *site* kazi zinaendelea na Diwani wa Kata ile ndugu yangu Tabwe anaendelea kusimamia mradi ule safi sana Mheshimiwa Rais tunamshukuru. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo kuna mradi wa Shilingi bilioni 1.3 mradi wa pale Nyanjati kwenda kule Kivinja A. Mradi ule kila kitu kimeshakamilika tunasubiri tu kusaini makaratasi yale ya mkandarasi. Mimi nikuombe chondechonde Mheshimiwa Waziri hakikisha kwamba hili linaenda kufanikiwa na mwaka jana nilisema hapa mambo yakiwa mazuri tutakupa zawadi na kwa uadilifu uliokuwa nao jana niliwaona shemeji zangu sijui kama ile ruhusa umepata mke wa tatu yupo pale anakusubiri. Tunaomba sana tuhakikishe kwamba ule mradi unakwenda kusainiwa na unakwenda kufanya kazi moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa kuliko yote namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Nilimwambia kwamba katika Jimbo letu la Kibiti kuna maeneo ya *Delta* kule pamoja na kata za Kihongoloni, Maparoni, Mbuchi, na Msala. Tangu jimbo lile liliiyokuwa limeanzishwa hawajawahi kuona bomba, Mheshimiwa Waziri akaniambia kwamba bwana sikiliza tunakwenda kufanya mpango kutafuta fedha na tunaenda kufanya upembuzi yakinifu katika Bonde la Mto Rufiji. Nataka niseme tu, Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana mzigo umetoka shughuli zinaendelea piga kazi nani kama Mama Samia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa haya yanayotokea mimi niseme tu sisi watu wa Wilaya ya Kibiti tukiwa tunapigaga kura zile za kuchagua Rais ndiyo huwa tunaongoza Mkoa wa Pwani 2025 panapo uhai sijui Mama huyu atazibeba beba viyi zile kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba niendelee mbele. Pamoja na kuyasema yote haya mazuri mimi nilikuwa naomba niishauri Serikali katika mambo mawili tu; jambo la kwanza nilikuwa naomba nishauri Serikali; jana nimewasikia Wabunge wenzangu na sisi ni wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sizungumzii tu Kibiti peke yake tumesikia malalamiko ya watu kutoka Mtwara na watu kutoka Lindi, bajeti tunajua kwamba haitoshi, Mheshimiwa Waziri angalieni huko Serikalini kama itapendeza twende tukawatafute wadau ambao wanaweza waka-*finance* hii

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

miradi na kujengwa vile vile wadau wapo mnaweza mkayatoa maji katika mradi ule wa Mtwara Ruvuma *Walter Project* wapo wadau wanaweza wakaifanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama vile haitoshi, kwa ndugu yangu Mabula jana aliongea kwa ukubwa sana vile vile wadau wapo, tuwatafute ambao wanaweza wakaifanya miradi hii mikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi naomba niungane na Mheshimiwa Ngasa; jana alishauri jambo moja la msingi kwelikweli. Alisema kuwa kwenye hii miradi wakati tunatoa hizi *tender* tuangalie ukubwa wa zile *tender*. Najua kuna sheria zetu za manunuzi zinatubana, lakini tuwe *flexible*. Kama inapendeza kuna vimiradimiradi hivi milioni 500, milioni 700 labda mpaka bilioni moja itolewe katika ngazi ya wilaya kule tunaisimamia karibu sisi na madiwani na. Ile miradi mingine mikubwa mikubwa inaweza kwenda katika ngazi ya mkoa ili mambo mengine yakawa yanakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na yote haya, naomba tu niseme, Mkao wetu wa Pwani mmetufanyia mambo makubwa sana ukizingatia kwamba pale sisi tumefungiwa mradi mzuri sana pale Chalinze kwa ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwani. Sisi Mkao wa Pwani ni Mkao wa Viwanda, maji ni uti wa uhai, lakini kama hivyo haitoshi katika shughuli zetu za mambo ya viwanda maji ni kitu cha msingi. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais, tunakushukuru sana Mheshimiwa Aweso piga kazi na sisi tupo atakayekuzingua na mimi nakwambia tu kaka zako tupo, tutakusimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la mwisho naomba nizungumze tena ni lamsingi kwelikweli. Mheshimiwa Waziri huyu ana mambo mengi. Sasa, ikikupendeza, tutakapopitisha hii bajeti mimi nilikuwa naomba tu unipe Mheshimiwa Naibu Waziri niende naye Kibiti, twende kule twende tukakague miradi ile, tukazungumze na wananchi kule. Nataka nimuhakikishie tu Mheshimiwa Naibu Waziri akifika kule pweza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wataliwa kambare watapatikana changu wapo na mambo mengine yataendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninasema kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, nilimuita Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu. Sasa naomba wafuatao wajiandae, Mheshimiwa Justine Nyamoga, Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Venant Daut Protas.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie kwenye wizara hii. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu Jumaa Aweso Mbunge na Naibu Waziri dada yangu Mahundi na watendaji wao wote wa wizara hii ya Maji, Fungu 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukweli kazi wanayoifanya ni kazi kubwa ni kazi ya kizalendo nchi yetu ni kubwa. Miradi inayohitajika ni mingi na maji hayana Subira. Mwananchi uweze kumwambia usubiri maji kesho au kesho kutwa hali ya maji ni muhimu kupatikana kwa wananchi wetu kwa haraka na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Nampongeza kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Mwaka 2021/2022 nilizungumza hapa, nikalia kwa muda sana na nikasema kwenye maswali yangu ya msingi naya nyongeza mliyonipa nafasi ya kuuliza, juu ya tanki ya mradi mkubwa pale mshikamano ambao utakuja kuwa majibu ya sehemu kubwa ya Jimbo la Kibamba. Mheshimiwa Rais alisikia kupitia mwamvuli wake Mheshimiwa Waziri, alifika jimboni mwezi wa nane mwishoni mwaka jana na kusaini mkataba ule hadharani mbele ya wananchi wa Jimbo la Kibamba na tayari kazi ile kubwa inafanyika,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimshukuru sana, kwamba fedha zilizokopwa za tirioni 1.3 za UVIKO zilipelekwa zaidi ya bilioni 139 za maendeleo katika Wizara ya Maji fungu 49, na bilioni 2.5 zilitolewa kwenda Kibamba kwa ajili ya mradi huu wa mshikamano. Nikushukuru sana Mheshimiwa Rais na kwa usikivu wa waziri wako kwenye eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli, panakuwepo na mazuri mengi lakini vile vile na changamoto huwa zipo. Nifurahi tu, nifurahi kwa maana kimbilio la ukosefu wa fedha linaweza likatamkwa katika njia nyingine kama UVIKO ilienda kuongezea 139, lakini kila mwaka tunawapangia au tunawapitishia *almost* bilioni 680 katika Wizara hii. Lakini za maendeleo ni takribani bilioni 646 lakini walivyoongezewa na hizo 139 zikafika takriban bilioni 785, bajeti ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupanga na kupata ni vitu viwili tofauti hawa wanabahati sana wamepanga wamewekewa hizo lakini wamepokea takribani bilioni 743 ambapo taarifa ya Waziri inasema ni asilimia 95. Hii ni pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais pia sana, sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama tunapata kile tulichokipanga kwa nini sasa miradi haitekelezeki kwa wakati? Kwanini miradi haitekelezeki kwa wakati? Wananchi wa Jimbo la Kibamba wanaendelea kulia na mimi huwa nalia hapa mwakilishiwao. Kibamba ndiyo imelisha Ubungo yote Jimbo la Ubungo kaka yangu Profesa Kitila Alexander Mkumbo yupo hapa. Lakini Kibamba ndiyo inalisha Pugu, kila siku nasema, *I mean* Kisarawe hadi na huko Pugu; mradi mkubwa umeenda Kibamba – Kirasawe, asilimia 95 wananchi wa kule kwa kaka yangu Jafo wanakunywa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawana maji Jimbo la Kibamba. Tunaambiwa hapa asilimia 86 katika miji, nafurahi hiyo ni takwimu ya jumla na uwiano au *average*. Lakini ukienda *specific* Kibamba natamka tu maeneo machache na Mijini, na Waheshimiwa Wabunge hapa zaidi ya 50 wanaishi kwenye Jimbo la Kibamba na Mawaziri zaidi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya 15 wako. Ipo siku nitawataja kwa majina ili muweze kuona umuhimu wa Jimbo lile. Mimi nasema ni Dar es Salaam Vijijini, mkubali ni Dar es Salaam Vijijini kwa sababu wanahitaji *attention* kubwa ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, maeneo ambayo ni maarufu na wananchi wanayajua na humu wote wanajua. Nasema Mpiji Magohe, Msumi, Msakuzi yote Kaskazini na Kusini hakuna maji kabisa. Vilevile, maeneo machache ya Kwembe, King'azi A nimezungumza watu wanakunywa maji machafu ya visima, machafu ya rangi na Mheshimiwa Waziri anajua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme, leo nilisema sitosema sana. Kazi mpaka sasa inafanyika. Sisemi kwamba hafanyi. Ipo miradi mitatu nimesema ukiondoa Mshikamano wa Mheshimiwa Rais, mradi wa Kitaifa. Nimesema mradi wa Kitopeni upo kwenye taarifa zao. Tuliahidiwa na Mheshimiwa Waziri tangu mwezi wa nane kwamba mwezi wa 12 tungepata hii miradi mitatu, ambayo ni Kitopeni, Mradi wa Mabwepande kule kwa Askofu Gwajima namuibia maji kwenye Tanki la Malolo kuja kilometra 8.2 hadi *Mpiji Center* kujazia pale Kidesa mpaka leo miezi sita imeongezeka. *Christmastutaenda* na Waziri kunywa pale maji, hakuna miezi sita imeongezeka. Tenki pale kutokea Kwembe Katiluelekeea King'azi AB na Kilimahewa tumewaambiya wananchi pale, tumeenda na Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mbunge. Leo hawa viongozi ninaowataja hawawezi kwenda watapigwa mawe. Hawawezi kwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tumeahidiwa mimi na wewe, kwa nini tunadanganywa? Mpango mzuri ulionao ni kuongeza uwezo na kutoa mafunzo mazuri kwa Watendaji wako wa ndani kwa ajili ya kazi za *extension* na *distribution* zifanyike kwa wakati. Kama bado uwezo mdogo, muone jinsi na mikakati ya dharula kuiokoa Dar es Salaam maeneo ya pembezoni. Mimi nimekusifia kazi unaifanya vizuri kama kijana mwenzangu lakini kama unaangushwa, sisemi unaangushwa na Ruemeja; anafanya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kazi mpaka mnamuongezea na Tanga, Korogwe, Same na maeneo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimi niaombe sana, leo siwezi kumaliza kusema, jicho la Serikali lijielekeze Kibamba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante...

MHE. ISSA J. MTEMVU: ...vinginevyo mtamuondoa Mheshimiwa Mtemvu Kibamba na siasa itaendelea kuwa ngumu sana katika maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu kwa mchango wako wa Dar es Salaam Vijijiini. Nilimwita Mheshimiwa Justin Nyamoga. Wakati huo Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Venant Daud Protas wanajiandaa.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nishukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wa Mkoa. Vilevile Injinia Joyce Bahati wa RUWASA lakini pia ndugu yangu Palanjo wa IRUWASA kwa kazi kubwa inayofanyika katika Jimbo la Kilolo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposimama hapa mara ya kwanza kuchangia Wizara hii kuna mambo kadhaa niliomba mwaka jana, na niishukuru sana Wizara hii kwa usikivu. Niliomba usambazaji wa maji katika Mji wa Ilula. Ninashukuru sana Wizara hii imechukua hatua, milioni 500 zilizotolewa kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ajili ya miradi ya UVIKO zilipelekwa pale na usambazaji umefanyika. Ninawaomba wale wanahabari waliokuwa wanataja Vitongoji vya kuzunguka llula havina maji waende sasa wakapige picha kwa sababu maji yanatoka ili tuje walikuwa na nia njema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu, wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri kwa usikivu wako umeongeza shilingi milioni 500 kwa ajili ya Mji wa Ilula. Ninakushukuru sana, tenda ile itangazwe mapema ili ule usambazaji uendelee katika vitongoji vyote vya Kata ya Ilula na Nyarumbu ili wananchi wale waendelee kunufaika na maji. Haikutosha kupitia *IRUWASA* shilingi milioni 350 kwa ajili ya Mji Mdogo wa Kilolo ambazo pia juzi kwenye mazungumzo umepitisha. Kwa maana hiyo ndani ya bajeti ya mwaka huu tayari tuna shilingi milioni 850 zinaenda ambazo zimeongezeka katika Bajeti iliyopita. Ninakushukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikakushukuru kwa ajili ya miradi mingine niliyoomba mwaka jana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri mmeifanyia kazi. Mradi wa Uhambingeto ambao umekuwa ni chechefu kwa muda mrefu. Mradi huu tayari umeshatafutiwa mkandarasi na amepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba kuweka *sign* ile mikataba mapema ili mradi ule wa Kata ya Uhambingeto uweze kufanyika mapema. Ninashukuru pia kwamba kuna miradi mingine miwili ambayo imechukua muda kidogo kupata wakandarasi lakini tayari imepatiwa fedha. Mradi wa Masege Masalali, Kihesa Mgagao na Mradi wa Ifua – Lisoli ambayo pia tuliiomba mwaka jana na imepata fedha. Mimi ninashukuru sana kwa sababu mmefanya kazi mapema na ninaona kwamba kuna dalili njema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri huwa anasema wali wa kushiba huonekana kwenye sahani na mimi nakubaliana naye. Lakini kuna vijiji na kata ambazo huo wali wa kushiba zinauona ila kama tunavyoenda kwenye hoteli

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

umefunikwa na ile karatasi ya nailoni bado haujafunuliwa.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kata ambazo bado hazijapata maji. Naomba nitaje baadhi ya maeneo. Kata nzima ya Ng'ang'ange haijapata maji tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Lakini pamoja na hayo, tunavyo vijiji baadhi ambavyo kuna mradi wa Mto Mtitu ambao ni Mradi wa Mto Mtitu ni mradi wa mkoa siyo mradi wa wilaya. Mradi wa Mto Mtitu maji yake yanapita katika Majimbo ya Kilolo Kalenga, Iringa Mjini pamoja na Jimbo la Isimani. Na huu mradi tayari pendekezo limeshaletwa liko mezani kwako kwa ajili ya kuomba mkopo kwa Serikari ya Korea. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mradi huu ufanyiwe kazi kwa sababu una vijiji vingi sana katika Jimbo la Kilolo pia kikiwepo Kijiji cha Kitoo. Kijiji cha Mtitu chenyewe ambao ndio Mto Mtitu unaitwa nacho bado hakijapata maji na ninaomba mradi huu ufanyiwe *design* nzuri ili uweze kukidhi pia baadhi ya maeneo ya Kilolo; kwa sababu chanzo ni Kilolo lakini ukiangalia Vijiji vya Kilolo ni vichache vitakavyopata. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa Kilolo – Isimani ambao Mheshimiwa Waziri unaufahamu, ulishautembelea. Mimi pamoja na Mheshimiwa Lukuvi wa Isimani tunakuomba mradi ule ukamilike. Umefika asilimia 64 na imebaki kidogo, na una-*covervijiji* vingi sana vya Kilolo pamoja na vya Isimani. Ninakusih i sana katika bajeti ya mwaka ujao ukamilishe mradi ule ili wananchi wa Kilolo na wananchi wa Isimani waweze kunufaika na mradi ule kwa sababu ni mradi mkubwa ambao una maslahi. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitoe ushauri mdogo kuhusu miradi iliyopo katika Jimbo la Kilolo. Jimbo la Kilolo lina vyanzo vingi vya maji kwa hiyo, miradi mingi ni miradi midogomidogo kwa sababu tukitengeneza miradi mikubwa itakuwa gharama kubwa isiyokuwa na umuhimu. Nimeona kuna *tendency* ya kuiangalia kwa ukubwa miradi mikubwa lakini hii miradi ya Shilingi Milioni 500 tayari umeshasambaza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maji vijiji vitatu, Shilingi milioni 600 umeshasambaza maji kata tatu, kidogo inapewa umuhimu mdogo kutokana na udogo wake kwa sababu ni ya gharama ndogo. Mimi napenda hii miradi ipate kipaumbele imalizwe mapema kwa sababu miradi mikubwa inachukua muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili unahusu suala la mita za maji. Mheshimiwa Waziri unafahamu kwamba kwenye umeme tumeshatoka kabisa kwenye *post paid* watu kuzungukazunguka kwenye nyumba kusoma mita ni *unnecessary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani pale Mkoa wa Iringa mmeshajaribu *prepaid* na inafanya kazi vizuri. Mimi ninaomba twende kwenye *prepaid* tuachane na watu kuzunguka, mwisho watu watapigwa mawe waambiwe ni panya *road* kumbe ni wasoma mita. Kwa hiyo, mimi ninaomba sana kwamba twende kwenye *prepaid* tuachane na haya mambo ya *postpaid*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kushauri ni Jumuiya hizi za Usimamizi wa Maji. Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba miradi hii imekuwa mingi na inakamilishwa kwa haraka, lakini ni kweli kwamba hakuna mfumo bora wa usimamizi wa hii miradi kwenye vijiji na hizi Jumuiya za Usimamizi wa watumiaji maji bado hazijawa imara vyaa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kuwe na utaratibu mzuri ili miradi hii iweze kuwa bora na endelevu. Na tukumbuke kwamba kwenye vijiji vyetu si kwamba sasa hivi watu wanataka kuchota maji kwenye vituo tuu. Kama sisi tulivyo mijini na wao pia wanataka maji yafike kwenye nyumba zao. Kwa hiyo, hizi Jumuiya zikiimarishwa zitasaidia kuweka taratibu nzuri za kuingiza maji kwenye nyumba zao. Mimi naomba sana hizi Jumuiya ziangaliwe ili tuweze kuboresha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa mchango wako.

Sasa ninamuita Mheshimiwa Sebastian Kapufi aweze kuchangia. (*Makofii*)

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi pia, kama ilivyo ada, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wengineo. Kwa ujumla wake Mheshimiwa Waziri wewe ni mtu rahimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo mimi nitajielekeza zaidi katika suala la uendelezaji wa rasilimali za maji na utafutaji wa vyanzo vipyta. Eneo kubwa nita-*concentrate* hapo lakini niishukuru Wizara kwa ujumla wake. Najua sisii kwa maana ya Mpanda mahitaji ni lita 11,370,000 lakini tunapata lita 6,050,000. Tuna upungufu wa lita 5,320,000. Hiyo ndiyo sura ya suala la maji pale kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nitakuwa si muungwana nisiposhukuru. Nafahamu kwamba kwa muda wote huu tuna Miradi ya Ikorongo Namba Moja na Ikorongo Namba Mbili. Vilevile kuna Mradi wa Manga ambao takribani shilingi bilioni 7.5 tumeletewa kutoka Serikalini. Lakini pia niishukuru kwa maana ya miradi mitatu. Tuna Mradi mmoja wa Mwamkulu ambayo hiyo Mwamkulu inakwenda Mkwajuni, Mlima Kipara na St. Maria. Tulipata fedha za UVIKO ambayo ilikuwa ni takribani shilingi milioni 476. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tuna mradi wa Kakese ambao ni Mfuko wa Maji wa Taifa, tulibahatika kupata shilingi milioni 951. Tunao mradi wa Milala kwenda Kampuni, tulibahatika kupata shilingi milioni 458. Hizo zote kwa ujumla wake nimshukuru Mheshimiwa Waziri. Isipokuwa, maombi yetu mapya kwako Mheshimiwa Waziri, tunaomba shilingi milioni 572 ili kuweza kumalizia mradi wa Kakese wenye thamani ya shilingi milioni 412 na Shilingi milioni 160 Mradi wa Milala kwenda Kampuni. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo natamani nilete picha kwa hili jambo ambalo nilisema, ramani ya mtandao wa maji na masuala ya vyanzo vipyta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuzungumza hapa. Bahati nzuri Waziri wa Fedha aliwahi kuleta taarifa akielezea wenzetu wa China. Ukiiangalia China pamoja na ukubwa wake lakini wametengeneza mtandao wa maji. Mtu wa Kaskazini ana uwezo wa ku-*supply* maji mpaka Kusini, mtu wa Kusini ana uwezo ku-*supply* maji mpaka Kaskazini, *likewise* Magharibi, Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini; nchi hii kwa ujumla wake ikiwa kuna miradi mikubwa; leo tunatoa bomba la mafuta kutoka Uganda linakwenda mpaka Tanga. Tuna bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam linakwenda mpaka Zambia. Ipaté picha hiyo Mheshimiwa Waziri, na nikuombe, unayo nafasi ya kuacha kumbukumbu. Mzee wa Toronto pale Dodoma ameacha kumbukumbu ya miti. Unaouwezo wa kuacha kumbukumbu Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii visima sikatai, mabwawa sikatai. Lakini uwezekano wa kuiunganisha nchi kwa mtandao wa maji upo, tunachotakiwa ni kuthubutu. Bomba linaweza likatoka Dar es Salaam likafika Katavi. Bomba linaweza likatoka Bukoba likafika Mtwara. Inawezekana ni kuthubutu tu; na kupanga ni kuchagua. Lakini unaweza ukapanga kufeli, ukishindwa kupanga umepanga kufeli. Kwa hiyo, mimi niombe sana, na katika hili kuna nchi nyingine hatujafika huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa ukienda kwa nchi za wenzetu wana-*treat* maji ya bahari, hatujafika huko, kwamba nchi hii tufike sehemu labda kama ni Bahari ya Hindi, tuyatoe maji ya Bahari ya Hindi kuyaleta huko, hatujafika hapo, vyanzo vinatosha. Chukua Ziwa Nyasa, chukua Ziwa Tanganyika, chukua Ziwa Rukwa inatosha. Habari ya visima sijataja *Victoria* na mimi kwa ajili ya uzalendo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sioni tabu hata kama maji ya Ziwa *Victoria* yamatfikia mtu wa Dodoma sawa ni mipango ya ki-nchi. (*Makofi*)

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Taarifa. Taarifa. Mimi hapa Kingu.

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Kingu Elibariki.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa mchangiaji taarifa ya kwamba mambo mazito na ya muhimu anayoyazungumza ambayo kimsingi mimi naya-reflect kwamba ni *long term plan* ambazo Wizara yetu inaweza ikasaidia katika kuleta maendeleo makubwa katika sekta ya maji lakini bahati mbaya sana Wizara ya Fedha nimejaribu kuangalia hapa simuoni Waziri, simuoni Naibu vitu kama hivi vingeweza kusaidia sana angalau kama mmoja anakuwa hayupo basi mmoja awepo kwa ajili ya kuchukua kumbukumbu ya kutengeneza mipango ya muda mrefu ya nchi. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kapufi unapokea taarifa?

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme pamoja na kuongelea mipango ya muda mrefu lakini watu waliofanikiwa duniani ni wenyewe jeuri ya kuthubutu. Mimi pale kwangu Mpanda tunalo Bwawa la Milala. Bwawa lile limechimbwa miaka ya 1950. Tuna chanzo cha Mto Ugala, Mkoloni kwa ajili ya kuyapeleka maji kwenye uchimbaji wa madini ameyatoa maji Ugala kuyaleta Mpanda Mjini, amechimba Bwawa la Milala uko miaka ya 1950. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watu wa miaka ya 1950 walikuwa na mitazamo hiyo mipana, vipi kizazi cha sasa hivi? Kwa hiyo, naendelea kuomba hilo. Nishukuru kwa maana na miji 28 na Waziri mimi Mpanda pale najua kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maana miji 28, mji wangu umeguswa. Nikikataa hicho kidogo nitakuwa mtu wa ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia habari ya kuendeleza Bwala la Milala, lakini chanzo cha uhakika ni Ziwa Tanganyika. Niombe sana; na nikilisema hilo liende sambamba kwa Mji wa Mpanda. Ukitumia maji safi inakwenda bila kujuliza, utazalisha maji taka. Hatuna mfumo wa maji taka. Niombe sana wenzetu wa mipango miji; jamani maji taka bado ni bidhaa muhimu.

Leo mahali kama Dodoma kwa kupitia maji taka, ukizalisha maji masafi mfumo wa maji taka ndio unapendezesha miji. Ukienda miji ya watu wengine hawaangaiki kumwagilia maua na vitu vingine ni kutokana na maji taka. Uki-treat maji taka unapata uwezekano kwanza hamtobanana kwenye kutumia maji safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuendelee kujipanga huko Mheshimiwa Waziri ili kuhakikisha habari ya maji taka isiwe ni tatizo iwe ni jambo la kuwekwa kwenye mipango yako pia. Miji inakua, Mji wangu wa Mpanda kasi yake ya kukua, na wewe Mheshimiwa Waziri umeshafika pale...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: ... Kasi ya kukua ni kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi. Nilimwita Mheshimiwa Venant Daud Protas, lakini wakati wafuatao wanajandaa, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii ya kuwa mmoja wa mchangiaji katika wizara hii muhimu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za makusudi za kwenda kutatua changamoto za maji katika nchi yetu ya Tanzania na majimbo yote ya Tanzania likiwemo Jimbo langu la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jitihada na kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Shukrani hizi zienda kwenye Wizara nzima ya Maji, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu; kiukweli mimi wamekuwa wakinipa ushirikiano mkubwa pindi ninapopata changamoto kwenye miradi yangu ambayo nitaitaja hapo baadaye. Nikiwa nawakimbilia basi wao wanani pa ushirikiano na changamoto hizo kuzitatua. Mimi niwashukuru sana, endeleeni kutulea na endeleeni kutusikiliza kwa sababu sisi tumeletwa hapa kwa nia ya kuwatetea wananchi na wananchi tukileta shida zao kwenu na nyie mnazitatua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo ngazi ya Wizara pia niwashukuru viongozi ambao wao wanawasaidia kutatua changamoto katika mikoa yetu na wilaya. Nimshukuru Meneja wa *RUWASA* mkoa wetu wa Tabora Ndugu Kapufi, anafanya kazi nzuri sana na ndio maana mkoa wetu umeheshimika kwa kuwa wa kwanza kitaifa kwa kutoa huduma bora ya maji.

Nimshukuru Meneja wetu wa Wilaya *Mr. Shibiki*, kiukweli anafanya kazi kubwa sana. Kuna kipindi Mheshimiwa Waziri nilikuwa meneja huyu amekosa usafiri lakini kwake usafiri haukuwa kigezo kutokufika *site*, alikuwa anatuma mpaka bodaboda ili aweze kwenda kutatua na kusikiliza kero ambazo zilikuwa zinawakabili wananchi. Nilikuja kwako na umeshanipa ahadi yakunilettea gari basi ninaami akipata gari changamoto zote za maji katika jimbo langu litakuwa limetatalika kwa asilimia kubwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo mambo machache sana nimempongeza Mheshimiwa Waziri na niendelee kukuomba tena. Tarehe 29 mwaka 2021 niliuliza hapa swali la msingi kuhusu Wizara ya Maji, niliuliza kuhusu Mradi wa Ziwa Victoria ambao unaendelea katika Jimbo la Igalula ambapo utatatua changamoto katika kata nne za Goweko, Igalula, Kigwa na Nsololo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuitia majibu yako, na siku hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri hakuwepo, ulijibu wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Maji; uliniambia mradi huu utakwenda kukamilika kabla ya mwaka wa fedha 2022 kuisha. Leo tumbakiza siku kama arobaini na tano mwaka wa fedha uishe lakini mradi ule huko katika asilimia thelathini kwenda arobaini, na haujafika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri; lengo la huduma na limeshaonyesha dhamira kwa sababu mradi huu umeanza; na juzi hapa Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa alikuja na viongozi wa chama tukaja ofisini kwako tukafanya kikao na wataalam. Kulikuwa changamoto ya ulipaji baadhi ya *certificate*. Siku ileile ulitoa maelekezo na *certificate* zililipwa na yule mkandarasi aliletu mabomba yako *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palikuwa na changamoto ya mkandarasi wa kuchimba msingi kwa sababu ya masika. Sasa, masika imekwisha na sasa mmuagize arudi *site* aendelee na kazi ili kuwafikishia maji wananchi wa Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe jambo lingine Mheshimiwa Waziri. Hii mikataba ambayo wanatuletea kule inakuwa na mkanganyiko mkubwa sana. Unakuta mtekelezaji ni *RUWASA* kule ngazi ya wilaya lakini anayetumika kununua mabomba ni anatoka Makao Makuu yani Wizarani sasa mnakuwa mtu wa wizara atambui umuhimu wa adha anayoipata kule Meneja wa *RUWASA* wa wilaya na wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mikoa. Sasa ninyi mna-*relax* kwa sababu ya ucheleweshaji wa kulipa *certificate* hasa ususani wa *supply* ya vifaa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri, kwenye mradi wangu aliniahidi ataenda kuongea na *supplier* alete mabomba yote lakini jambo lile bado halijafanyika. Nimbuombe atakapopata muda amuite *supplier* huyo alete, na asianze kutupa vigezo, kwamba akifikisha kilometra haleti vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, Mheshimiwa Waziri tuna mradi ambao wewe ulikuwaga Naibu Waziri wakati huo waziri *Professor Mbalawa* mliuja katika Kata ya Tura pale mwaka 2019 mkaahidi kwamba ku-*supply* katika Mji wa Tura utakamilika baada ya miezi mitatu. Tangu mwaka 2019 mpaka leo ule mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto si mameneja wangu wa Wilaya na Mkoa, changamoto iko katika hatua ya manunuzi ngazi ya Taifa. Niombe Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri waendeni wakatatue changamoto hii. Wananchi kila siku nikienda kule wananiuliza ni lini sasa kitendawili naomba ukakitatue ili waweze kupata maji katika maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la tatu ambalo nilitaka nishauri, na niombe Mheshimiwa Waziri mwaka jana aliniahidi kuwa usanifu wa bwawa la Kizengi umekamilika, lakini kwenye bajeti hii nimefungua vifungu vyote na majedwali yote sijaona amelipangia fedha. Ni muombe Mheshimiwa Waziri, Jimbo la Igalula lina changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji. Nishukuru kwenye fedha za UVIKO nilipata milioni 505 ambazo zitawezesha kuchimbwa visima 15; lakini kwa takwimu mpaka sasa hivi vimechimbwa visima sita ambapo katika Vijiji vya Kalangatu, Mwisolo pamoja na Isaga wamechimba wamekosa. Ni vijiji vitatu tu ambako wamechimba maji wamepata ambavyo ni Vijiji vya Kalangale, Mwamabondo na Mwamdalaligo, wamechimba maji wamepata lakini si mengi sana. Kwa hiyo ukiangalia jiografia ya Jimbo la Igalula maji ya visima si muhimu sana. Ili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutatua changamoto hizo ni kuwepo kwa upatikanaji wa maji ya mabwawa. Nimuombe; kwenye Bwawa la Kizenji usanifu umekamilika; sasa anipelekee fedha ili zikatatue asilimia zaidi ya 80 ya upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru juzi ameniletea wasanifu wengine waliokwenda kufanya usanifu kwa ajili ya kujenga Bwawa katika Kata ya Miswaki. Hata hivyo *solution* ya Jimbo la Igalula ni kuniletea mabwawa na si visima. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri pamoja na jitihada kubwa unazozifanya za kumsaidia Mheshimiwa Rais za kuweza kwenda kutatua changamoto ya maji miradi ilioanzishwa awali naomba iende ikakamilike kwenye mwaka huu wa fedha ili, wananchi wetu waone yale maneno wanayosema Mheshimiwa Rais akiwa kwenye majukwaa na mikoa mbalimbali basi yawafikie wananchi wetu wa Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja na niwapongeze wizara iendelee kufanya kazi nzuri. Ahsanteni sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Venant sasa namwita Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo aweze kuchangia.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kauli mbiu yake ya kumtua mama ndoo. Wote tunatambua imeitikiwa sana na inafanya vizuri. Lengo la mama lilikuwa ni kuhakikisha kwamba kila mama anayetafuta maji ayapate ndani ya mita 200 na ndio maana umeona wabunge wengi hapa wanasmama kupongeza. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Iakini pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na timu yake yote bila kumsahau Mheshimiwa *Engineer Naibu* Waziri pamoja na timu yote kama ambavyo wanafanya kazi. Kimsingi wameonyesha nia thabiti ya kupata majibu ya changamoto ya uhaba na upungufu wa maji safi na salama; kama sehemu yao ya kazi ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri. Kuna wakati kule Mtwara uwa hakukaliki kabisa na sauti zilipaswa kwa kiasi kikubwa. Mheshimiwa Katani jana alisema, Mheshimiwa Waziri alikuja na alijionea hali halisi mimi hapa ndani kila ninaposimama ninakuwa nikiuliza maswali ya maji ya kuokota; na nilitamani sana Mheshimiwa Wiziri ama waziri mdogo Naibu Waziri wangkuja kujiona hayo maji ya kuokota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara bado changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie leo, kuna kipindi wakati wa kiangazi sisi wananchi wa Mtwara tunakosa maji hata ya kupikia chakula; na hiyo ilishuhudiwa na viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi Kitaifa, Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu, wali ulipikwa kwa maji ya tikiti sijui kama ninaeleweka vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunavyozungumzia suala la upungufu ama uhaba ama hii changamoto ya maji safi na salama nadhani kwa Mkoa wa Mtwara ndio inaongoza, namba moja. Hata takwimu za upatikanaji wa maji, zile ambazo zimekuwa zikiandaliwa na watalam kwenye mkutano wa *RCC* zilikataliwa, na hapo ilikuwa inaonyesha ni asilimia 61. Lakini kiuhalisia, kule vijijini maji hakuna kabisa ndiyo maana tunapopata mvua zinaponyesha yale maji yanayotiririka juu kabisa tunayakusanya tukichota kwenye ndoo tunayaweka ili lile tope likae chini halafu ndipo tunakunywa hayo maji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, kwenye hilo eneo tu, hivi Serikali ilishawahi kufanya *coordination* kati ya Wizara ya Maji na Wizara ya Afya ikajua kwamba ikitatua hii changamoto ya maji kwa kiasi kikubwa tutapunguza gharama za matibabu kule kwenye Wizara ya Afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara wamesema; mimi sisemi kwamba Serikali haijafanya kazi, imefanya, na Mheshimiwa Waziri alikuja na tumeona alikwamua miradi chechefu lakini pia yapo maeneo pia kwama vimeshimbwa lakini bado changamoto yetu ni kubwa sana hali ya upatikanaji wa huduma za maji vijiji tunavijiji 800 kati ya hiyo vijiji 800 vijiji visivyo na maji ni 324 unaweza ukajiona hali ilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suluhisho la kwetu sisi ni maeneo mawili tu kwanza ni chanzo cha Mto Ruvuma ambapo kwenye kitabu cha waziri inasema hiyo ndio maeneo ya miradi ya kimkakati lakini pili ni chanzo chetu cha Makonde ambayo inajazwa kwa chanzo cha Mahuta Mkunya pamoja na Mitema.

Mheshimiwa Mqwenyekiti, sasa, ukienda kwenye chanzo cha Mitema *reserve* yake kwa mwaka ni mita za ujazo milioni 65 lakini kwa mahitaji ya watu wa Newala Tandahimba na Nanyamba kwa siku ni mita za ujazo elfu 27; ukifanya kwa mwaka ni mita za ujazo milioni 9.9. Ukienda Mtwara peke yake mahitaji ni mita za ujazo 21, na ukifanya kwa mwaka ni milioni 7.7. *Total*/ya mahitaji yetu sisi kwa Nanyamba Mtwara Newala na Tandahimba ni mita za ujazo elfu 17 wakati chanzo cha Mitema uwezo wake kwa mwaka ni mita za ujazo milioni 65; maana yake ni kwamba inatumika kwa asilimia 27 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri watu huku wamepongeza, na wewe umekuwa ukisema ndio mheo wa mgonjwa ndio utaweza kutoa dawa. Nikuombe sana kaka yangu Aweso, hiki chanzo cha Mitema kitumike chote kiweze kutatua tatizo la maji kwenye hizi wilaya nne.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mradi hapa tumeona imeandikwa Makonde, lakini Mheshimiwa Waziri hatujui, hivyo *scope* ya mradi huu wa Makonde ni ipi? inaanzia wapi? Mawanda yake yanaanza wapi na yanaishia wapi? Fedha zake pia hazionekani, ndio tunasubiri fedha za ndani, ni Shilingi ngapi, zitafanya nini, zitawanufaisha wananchi wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, mimi bado naona kama hali ni tete na haitabiliiki. Ukienda kwenye Mradi wa Kuboresha Miji 28 imetajwa pale Makonde. Sasa mimi nikawa najiuliza, hivyo *beneficially*wa Makonde ni akina nani? Haitaji kwenye kitabu. Je ni Newala, Tandahimba, Nanyamba, Mtwara? Sasa hapo ndipo ambapo panaleta kizungumkuti. Ni vema Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie, nani maana Makonde ni chanzo....

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti ninaomba sana; pamoja na hilo ukarabati wa mabomba ya Mtwara ukafanyiwe kazi kwa sababu yale mabomba bado yana miaka 40 na pengine tutakapokuja mwakani na sisi hatutaspera kwa sauti hizi kwa sababu tutakuwa tumenufaika...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Agnes kwa mchango wako.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana nilimuita Mheshimiwa Esther Lukago Midimu wakati huo wafuatao wanajijandaa Mheshimiwa Aida Khenani Mheshimiwa Ramadhani Ighondo Abeid na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais wangu mpendwa Mama Samia Suluhu kwa kazi nzuri alizozifanya, Mwenyezi Mungu ambariki sana.

Pili nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya Mwenyezi Mungu ambariki sana. Tatu nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu Waziri na *cabinet* yake, wanafanya kazi nzuri. Mheshimiwa Aweso unafanya kazi nzuri mwanangu, Mungu akubariki.

Mheshimiwa mwenyekiti, tunamuona Mheshimiwa Waziri anazunguka nchi nzima kukagua miradi ya maendeleo; Mungu ambariki sana pamoja na Naibu Waziri. Nawapongeza Mawaziri wa Wizara pamoja na Naibu Mawaziri, wanafanya kazi nzuri, wanazunguka nchi nzima kukagua miradi ya maendeleo, Mungu awabariki sana. Nampongeza sana Meneja wetu wa Maji wa Mkoa, Mariam, kwa kazi nzuri anazozifanya, Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia milioni 400 kwa ajili ya Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Mkoa wa Simiyu katika Wilaya za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa pamoja na Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waziri tayari ameshasema, bilioni 400 zimeshapatikana. Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati ya kumtua mama ndoo kichwani. Na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba pesa, hizo bilioni 400 zimepatikana 400, ila bado wanatafuta mkandarasi. Niombé Serikali yangu sikuvi ya Chama Cha Mapinduzi mkandarasi apatikane haraka ili wananchi wa Mkoa wa Simiyu tuweze kupata maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachi wa Mkoa wa Simiyu ni wakulima wazuri, maji yale yakifika tutalima kilimo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

cha umwagiliaji kwa mazao ya mbogamboga, mazao ya biashara na mazao ya chakula. Sasa, tukipata mazao ya chakula tuta-supply hata mikoa ya Jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sera ya Serikali ni kuwa na uwanja wa ndege kila mkoa kwa maana hiyo na Mkoa wa Simiyu tutapata uwanja wa ndege na eneo tumeshatenga. Kwa hiyo tutalima mbogomboga, cabage biringanya pilipili hoho nyanya tutasafirisha na kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa tisa ilio harini kukumbwa na janga. Kama tutapata Maji ya Ziwa Victoria yatatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Simiyu ni mkoa wa wafugaji, tuna ng'ombe millioni mbili tuna mbuzi zaldi ya milioni nne tuna Kondoo zaidi ya milioni tatu, tuna bata na kuku pia. Wanyama wote hao wanahitaji maji; na maji ni uhai. Wanyama hawa wakipata maji watazaliana lakini vilevile na wafugaji watapata utajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeza Serikali kwa Wilaya ya Meatu Kata ya Mwanuzi ambayo ilikuwa na shida sana ya maji, ilikuwa inakunywa maji ya tope, maji meusi ambayo yalikuwa yamechanganyika na tope lakini. Sasa hivi Serikali imejitahidi toka mradi ule ukamilike sasa hivi maji ya Meatu ni mazuri na ni meupe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji Meatu kukatikatika linasababishwa na kukatikatika kwa umeme. Ombi kubwa kwa Mkoa wa Simiyu kitu tunachokilomba Serikali itusaidie ni kutujengea kituo kile cha kupoza umeme ambacho kitasaidia sana. Vilevile miradi yote iliyoko sasa hivi Wilaya ya Meatu inayoendelea ikikamiliika Wilaya ya Meatu itapunguza shida za maji kwa sababu itafikia asilimia 84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeza Serikali kwa mradi wa maji unaotoka Lamadi kwenda Mkula mradi huu umesaidia sana umegharibu bilioni mbili. Niombe Serikali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yangu sikivu, kuna vijiji viwili vimebakı kupitiwa na huo mradi ambavyo ni; Kijiji cha Chabutwa na Kijiji cha Mwanale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kuna Kata ya Nyaluande vijiji vyote vitatu havijapata maji. Vijiji hivyo ni Nyaluande yenewe Mwagindi na Mwamkale. Pia Kata ya Igalukiro ina changamoto kubwa ya maji Kijiji cha Runala na Mwamagigisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuiomba Serikali yangu Sikivu, Wilaya ya Bariadi Kata za Sima, Gudui na Isanga kuna shida sana ya maji. Naomba Serikali ibaini mitaa yenye shida sana ya maji ili iweze kutupatia maji. Lakini vilevile naendelea kuipongeza Serikali kwa ajili ya Wilaya ya Itilima ambako tuna miradi mingi inayoendelea iliyokamilika. Hata hivyo, kuna Kata ya Kinamweri ina tatizo sana la maji. Naiomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie hapa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Aida Khenani

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima. Niwashukuru sana pia wananchi wangu wa Jimbo la Nkasi Kaskazini kwa mapito magumu ambayo kaka yangu Aweso

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

anayajua vizuri. Pamoja na changamoto hizo ambazo zinaendelea nikupongeze pia waziri kwa jitihada zako binafsi, lakini pamoja na timu yako, namna ambavyo mnakuwa watu wa kusiliza Wabunge wenzeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana viongozi wangu wa maji kuanzia mkoa mpaka wilaya namna ambavyo wanajitahidi kwa namna ambavyo wanaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza namna ambavyo fedha inapotea zaidi kwenye kutafuta vyanzo nya maji. Wilaya ya Nkasi ni mionganoni mwa wilaya ambazo kuanzia mbunge wa kwanza nchi ilipopata uhuru jambo la kuzungumza mara nyingi ndani ya Bunge ni maji mpaka mimi nazungumza leo maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mchache nitakwenda kwenye mapendekezo. Pamoja na kwamba kuna miradi ambayo inaendelea kwenye Wilaya ya Nkasi. Tuna mradi wa Kabwe ambaao umeshakamilika wa bilioni 1.7, tuna mradi wa Isale ambaao ni kichefuchefu mpaka leo, leo ni mara ya tano nazungumza kwa bilioni 5.5, tuna mradi wa Katongolo wa milioni 349, tuna mradi wa Namanyere wa bilioni 1.9 ambaao na wewe umekuja kulipa hiyo fedha mwezi Disemba mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nasema fedha nyingi zinapotea pamoja nahii Miradi ninayoizungumza bado haiwezi kumaliza changamoto ya maji hata robo kwa changamoto iliyopo kwa Wilaya ya Nkasi. Kwanini fedha nyingi inatumikaa kwenda kutafuta vyanzo wakati chanzo kipo? Hili ni tatizo kubwa kwenye Wizara hii ya maji fedha inayotengwa ni jambo moja, fedha inayokwenda ni jambo jingine lakini miradi ambayo inakwenda kuanzishwa na kukamilika ni jambo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushauri Mheshimiwa Waziri; pamoja na wataalamu waku walioenda darasani ni vizuri wanapokwenda kutafuta vyanzo jambo hili likawa ni shirikishi kwa watu wa eneo husika. Nimezungumza mara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kadhaa hapa kwamba Mkao wa Rukwa sisi kipaumbele chetu hatuitaji maneno mengine tunahitaji maji kutoka Ziwa Tanganyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linahitaji miujiza gani? Linahitaji uthubutu wa viongozi mlioko madarakani. Kama kutoka Kilando kuja na manyele ambapo kuna Kata tano ni kilomita 64, hesabu walizopiga kugawanya tu maji kuyatoa pale ni kama bilioni 70 mpaka 100. Hizi fedha zote ambazo mmekuwa mnatenga kama kweli jambo ni kuthubutu tu kwanini mmeshindwa kutoa maji ziwa Tanganyika mnazidi kupoteza fedha kutafuta vyanzo ilhali chanzo kipo? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hiki ulichokiandika hapa, kwamba mnakwenda kutumia maziwa makuu lakini nikiona bajeti yako uliyopewa napata changamoto na utekelezaji wa hiki unachokizungumza. Bajeti ni ndogo sana na hamuwezi kutumia maziwa makuu kwa hii bajeti iliyopo. Niombe Serikali kama kauli mbiu ya Rais wetu akiwa Makamu wa Rais ni kumtua mama ndoo kichani twende nayo kwa vitendo kwa kuipa Wizara ya Maji kipaumbele kwa kwenda kutatua changamoto za maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana Nkasi wameniagiza, kama unafikiri ni gharama kubwa kwenda kuchukua yale maji ,kwa kuwa chanzo kipo, ina maana tumeshaepusha tayari fedha ya kutafuta chanzo, tunazungumzi habari ya ku-*treat* maji na kuyapeleka kwa wananchi. Wananchi wanasema wa Nkasi wako tayari kuanza leo kuchimba mtaro wenyewe kwa mikono mpaka Kilami. Naomba na wewe kama mtoto ambaye unajua maumivu anayopitia mwanamke hii lugha ni ngumu sana nimeona na mimi nikufikishie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najiuliza, mbona kuna maeneo yana miradi ambayo ni ya milioni 600, bilioni 500, Rukwa tuna bahati mbaya gani? Hiyo bilioni 100 au 70 leo tunazungumza Habari ya maji? Wananchi wa Kata ya Kipundu walikusimamisha pale ulivyokuja. vilevile wananchi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Kata za Namanyere, Isumta, Mkomolo pamoja na Mtenga! Yaani unashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niseme kati ya maajabu ya dunia ya Tanzania kuna maajabu mengine. Yaani Kata ya Kipili ninapofanya mkuutano mimi ukigeuka likipiga wimbi kubwa maji yanakuja kunigusa mpaka mimi lakini wananchi hawana maji ya kutumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji nini? Mungu ametupa maji kilichokosekana ni uthubutu wa viongozi mliopo kama maji yapo yanaonekana kuyapandisha kufikisha kwa wananchi kuna shida gani? Na hili jambo, kwa sababu ya muda unavyokwenda haraka zaidi, naomba nizungumze fedha ambazo zinatumika kwenye upotevu wa maji. Tunapima maji ambayo yanazalishwa na maji ambayo yanawafikia wananchi, maji kwa utaratibu wa kawaida yakipotea asilimia 20 tunajua yanapotea kwenye vyonzo mbalimbali aidha miundombinu na vitu vingine lakini kwa Tanzania ni asilimia 35 ya upotevu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya *EWURA* ya Machi, 2022, walizalisha maji millioni 322, lakini maji yaliyopotea ni mita za ujazo milioni 113.5 sawa na asilimia 36.8. Ukipeleka kwenye fedha inamaana fedha ambazo walikusanya ni bilioni 484.2 zilizopotea ni bilioni 178.9. Kwa hiyo kama ni mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika na kuzambaza Mkoa wa Rukwa mngesambaza na fedha ikabaki, lakini inapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri nilazima fedha itengwe kwa ajili ya kuboresha miundombinu yam aji kuepusha upotevu wa maji ili fedha hiyo ambayo inapotea iende kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tujue vigezo vinavyotumika kupeleka miradi ya kimkakati kwenye haya maeneo. Mkao wa Rukwa tuko kwenye miji 28, lakini Ziwa Tanganyika tunalo na nyie mnasema gharama ni kubwa, bilioni 70 mnasema gharama ni kubwa, lakini kuna maeneo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yanapata zaidi ya hiyo fedha, lakini maji yanapotea kwa gharama nyangi zaidi ya fedha. Tunaomba kwa kuwa ulifika na ukaona na unasema mara nyangi hatuitaji kauli tunahitaji maji. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Aida Khenani, nilimuita Mheshimiwa Ramadhani Ughondo, wakati huo Mheshimiwa Mzava nimeona atachangia badaye kidogo. Mheshimiwa Ramadhani Abeid, Mheshimiwa Michael Mwakamo na Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa angalau na mimi kuwasemea wananchi wenzangu wa Jimbo la Singida kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya. Pia nitangulize shukrani zangu nyangi sana kwa Waziri wetu Pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifana kuhakikisha nchi yetu inapata maji. Na hapa lazima tutambue juhudhi kubwa zinazofanywa na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kusema kweli hata ukifuatilia hotuba yangu yam waka jana kwenye wizara nilikuwa mkali sana na nilisikitika kwa ile hali ya wananchi wetu kunywa maji pamoja na Wanyama. Lakini mwaka huu nitakwenda kuzungumza kwa kutoa shukrani na pongezi kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwa kipindi hiki kifupi cha miaka hii miwili au huu mwaka mmoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Singida Kaskazini tumepeata miradi mipya yam aji 15 ambayo inatafikisha asilimia 67 ya upatikanaji wa maji endapo miradi itakamilika ipasavyo, ambapo tumepeata visima 15 vyenye thamani ya shilingi milioni 420 kila kimoja katika Kijiji cha Ntondo, Kwae, Sekotoure, Kinyamwenda, Msikii, Mwalala, Poku, Igauri, Mwakiti, Itamka, Mkenge, Makuro, Misinko, Msimihi na Maghandi. Maeneo haya sasa yanaenda ya kupata uponyaji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nichukue fursa hii pia kuwapongeza watendaji wa Wizara ya Maji, kwa maana ya RUWASA pale Mkoani. Meneja wa Mkoa pamoja na Meneja wa Wilaya pamoja na staff *wao* kwakweli wanatupa ushirikiano sana katika kuhakikisha jamii yaw ana Singida inapata maji safi na salama wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia wadau wa Sekta Binafsi wanaoshirikiana na Serikali kuhakikisha wananchi wetu wanapata maji, wakiwemo *World Save International, World Division* pamoja *Silver Crescense* ya kutoka Uturuki ambao wametusaidia kukarabati na kuchimba visima vipyta vipatavyo 44 katika vijiji mbalimbali vya Jimbo letu la Singida Kaskazini. Kwa hiyo, ninaendelea kuwashukuru na kuwaomba waendelee kutupa ushirikiano kuhakikisha kila mtu katika Jimbo letu la Singida Kaskazini anapata maji safi na salama wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye kuwasilisha changamoto chache ambazo ninaomba sana Mheshimiwa Waziri azingatie na kuhakikisha tunazipatia ufumbuzi ili tuendane na hii kasi ambayo nimeizungumza hapa tunayoitarajia, ya kupata maji safi. Moja ya changamoto kuna vijiji ambavyo tuliwahi kuchimba maji lakini kwakweli maji haya yanapatikana ya chumvi na si salama kwa binadamu. Kwa hiyo, maeneo yale yanahitaji tupeleke bomba. Mojawapo ni kijiji cha Gaiye kitongoji cha Gairu katika kijiji cha Sagara pamoja na kijiji cha Mangida tumechimba visima kadhaa lakini maji hayakupatikana. Kwa hiyo maeneo haya nimuombe sana Mheshimiwa Waziri tuende tukafanye usambazi kutoka kwenye kile chanzo cha Sagara ambacho kina maji ya kutosha; lakini tu hatujatandika mabomba niombe sana tufanye usambazaji tuwapelekee hawa wananchi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siku nilienda kuomba kura pale walinipa maji ya chumvi. Tafsiri yake ni kwamba yale maji kama yanafaa nami niyanywe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikukaribishe siku moja na wewe uje haya maji uone kwamba kuna shida. Kwa hiyo, nikuombe

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ushirikiano tuwasambazie maji na wala si umbali mrefu ni kama kilometa moja tu ambayo wala si gharama kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nimeitaja miradi mikubwa sana ya maji hapa, nikiacha ile minne ambayo tayari imeshakamilika. Ule mradi wa Wamitura ambao una thamani wa Shilingi milioni 565 kuna ule mradi wa Mweganji shilingi milioni 565, ule mradi wa Ndibeshi Shilingi 565. Miradi hii ina gharama kubwa lakini changamoto kubwa ipo kwenye usimamizi. Idara yetu ya RUWASA hawana vitendea kazi hata gari hawana. Unampa mtu mradi wa shilingi *billions of money* lakini namna ya kuusimamia kufika pale kwenye *field* hawana uwezo huo kwasababu ya vitendea kazi.

Niombe sana tuwasaidie hawa watu wapate magari, wapate vitendea kazi ili waweze kufika kwenye maeneo ya kazi kwa wakati na kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na eneo la jumuiya za watumia maji amezungumza Mbunge dakika mbili tatu zilizopita kuhusu uwezo mdogo alionao wakifedha hata kitaalamu. Tunategeneza miradi ya kutosha ya fedha nydingi lakini kwenye eneo la uendeshaji tunakwama. Niombe wale watalamu wawili mhasibu pamoja na fundi hawa wawe ni waajiriwa wa Serikali pamoja na fundi hawa wawe ni waajiriwa wa Serikali na walipwe na Serikali ili tuweze kuwamanage, na tuweze kuwafuatilia na kuwasimamia ipasavyo. Hii itasaidia kwenye ufanisi kwa maana ya *efficiency* ya hii miradi pamoja na kudumu iweze kudumu ili kuendelea kuwashudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeomba pia Wizara wanisaidie, hasa Mheshimiwa Waziri ni kwenye kuongeza upanuzi wa miradi. Hii miradi ambayo nimeitaja hapa kumi na tano ni miradi minne tu ambayo itafanyiwa usambazaji. Niombe sana hii miradi iongezewe fedha ili tuweze kufanya upanuzi hata yale maeneo mengine

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambayo hayajafikiwa tunaweza tukayafikia kwa kufanya upanuzi, kwa maana ya kuweka mtandao wa bomba kwenye maeneo ambayo hayana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuna vijiji ambavyo tumeomba kwa *Next budget* vijiji ambavyo vinashinda kubwa sana ya maji na havina mradi wowote kijiji cha Semfur, Ndugwira, Ikiu, Kibaoni na kule Mukulu Mheshimiwa Waziri ulifika siku ile ulivyokuja tuliwaahidi wananchi na walifurahi sana. Kwanza ujio wako pale ulipokuja walifurahi na ulivyowaahidi maji kwakweli walifurahi zaidi. Sasa wameendelea kunikumbusha Bwana Mheshimiwa Waziri alituahidi kisima hapa vipi? Kwa hiyo, sasa niwasilishe tena ombi hili kwako Mheshimiwa Waziri angalau basi nawao wapate maji yale siku ukienda sasa tuyanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuwasilisha hili lakini pia kwenye maeneo kuna miradi ambayo tayari inafanya kazi mathalani mradi wa maji pale mji mdogo wa Iliongero ambao ndiyo makao makuu ya halmashauri. Ule mradi ni wa muda mrefu unachanzo cha uhakika cha maji, lakini shida ni maji yale yapo maeneo machache hata maeneo ya karibu tu hayapati maji. Kwa hiyo, niombe tufanye upanuzi kwa kuongeza miundo mbinu kama vile kujenga matanki pamoja na mabomba ili wananchi wapate maji ipasavyo. Pale vilevile kuna watumishi wa Serikali wanakwenda makazini asubuhi wanarudi wamechoka wanahitaji wapate maji salama na yakutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana mradi huu wa Iliongero pamoja na ule wa Mji mdogo wa Ngamu ifanyiwe upanuzi wa kutosha ili wananchi wengi wapate maji; kwa sababu pengine inaweza ikatupunguzia hata adha ya kuhangaika kuchimba visima vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niombe pia, kwenye hizi jumuiya za watumia maji kuna shida moja ambayo naiona, kwamba hawa wananchi wale wakata risiti wale wanatumia zile risiti za mkono stakabadhi ni vyema wangkuwa na zile *EFD Machines* ambazo kwanza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zitaepusha upotevu wa fedha lakini pia zitasaidia hata kufuatilia mapato yanayopatikana ambapo wakati mwingine miradi hii inaharibika tunashindwa kuikarabati. Kwa hiyo, niombe sasa ni vyema watu hawa wapatiwe *EFD machine* kwaajili ya kuhakikisha tunadhibiti mapato yanayopatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya mimi niwasilishe sana taarifa yangu hii lakini niendelee kuiomba Wizara kuhakikisha kwamba hii miradi ambayo wameahidi kututekelezea mwaka huu ichimbwe kwa wakati na fedha zije kwa wakati ili *next time* nikija hapa Mheshimiwa Waziri tuwe tunapongezana tu si kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nishukuru sana, niwasilishe hotuba yangu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani Ighondo Abeid namuita...

MHE. ABEID R. IGHONDO: Naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nilimuita Mheshimiwa Michael Mwakamo wakati huo Mheshimiwa Nashon Bidyanguze anajiadaa.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia. Kwakweli leo kama kanuni zingekuwa zinaruhusu ningekuomba tungeimba nyimbo moja ya msemaji mkubwa sana wa timu kubwa nchini; kwamba hawaamini macho yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi watu wengi walikuwa wanafikiri utekelezwaji wa Bajeti ya Serikali hasa kwenye hii Wizara ya Maji ulikuwa ni mdogo sana. Lakini kwa namna ya pekee kupitia hotuba ya Waziri mwenye dhamana ametuthibitishia Watanzania, kwamba Mama, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka huu ametoa asilimia 95 mpaka sasa ya bajeti ambayo iliombwa na Wizara.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa namna ya pekee kwa niaba ya Watanzania na hususani wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijiji ni nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kuwekeza nguvu kwenye miradi hii ya maji ambayo ni changamoto kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili nipongeze watendaji wa ngazi za chini. Pale Mkao wa Pwani na Wilaya ya Kibaha tunao akina mama wawili *Engineer Beatrice* na *Engineer Debora kwakweli* ni akina mama wa mfano kwasababu wanashughulika sana na matatizo ya maji kwenye maeneo mbalimbali vijiji. Niwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 14 ameonesha miradi inayotekelwa kwa ajili ya utunzaji wa vyanzo vya maji. Nimeamua nianzie hapa nami kumuonesha sehemu ya chanzo cha maji ambacho kinaharibika kwa kiwango kikubwa lakini hakijatengenezewa mradi wa kuweza kudhibiti uharibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakumbuka jiji la Dar es Salaam na Mkao wa Pwani unapata maji ya kunywa na matumizi mengine kutoka kwenye chanzo cha Mto Ruvu. Chanzo hiki cha Mto Ruvu kinaathirika na mambo mbalimbali ikiwemo kule juu ambapo kunakwenda kuchimbwa bwawa kubwa kwaajili ya kuhifadhi. Lakini pale jimboni Kibaha Vijiji kwenye eneo la Kitomondo Mto Ruvu umehama, umeondoka kwenye njia yake ya asili unakwenda kwenye maeneo mengine unapeleka maji kwenye mabwawa ambayo si chanzo cha mabomba yanayopelekea Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri Wizara na hasa watendaji walio karibu na chanzo hicho wangekwenda pale Kitomondo wakaone, wakazibe ule mto uliohama ambao umepoteza muelekeo wake. Badala ya kuelekea kwenye vyanzo mashine ya maji pale Ruvu chini na Ruvu juu umechepuka umeenda sehemu nyingine. Kwa hiyo maji mengi sana yanapotea yanaingiwa kwenye Bwawa linaitwa Bwawa la Mongomole, yanasaababisha yasipite kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

chanzo cha Mtambo wa maji hivyo kupelekea kwenye mitambo ile kuwa na maji machache na yanayopelekea Dar es Salaam kukosa maji kwa kipindi kikubwa. Kwa hiyo ningewashauri sana Serikali wangekwenda pale wakaone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa ingekuwa busara sana nikaomba, kaka yangu wa Kibiti alimuomba Waziri ikiwezekana Naibu Waziri aende kule Kibiti. Na mimi nitumie nafasi hiihii kabla hujafika Kibiti ungeruhusiwa usimame pale Kibaha twende ukaone ile hali ya Kitomondo halafu uweze kuitolea maelekezo ya kuokoa maji kwenda Jiji la Dar es Salaam. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya maneno haya, lakini vilevile kwenye Hotuba ya Bajeti Mheshimiwa Waziri amezungumza suala la Mradi wa Maji ya kutoka Mlandizi kwenda Chalinze mpaka kule Mboga. Mradi huu umekamilika na ni mzuri niwapongeze sana Serikali, lakini tarehe 22 mwezi wa tatu tulipokuwa tunafanya uzinduzi wa Mradi huu pale Chalinze na Mheshimiwa Rais, Rais alitoa tamko la kuongeza fedha la takriban milioni 500 kwa ajili ya kuongeza vitolea maji kwenye maeneo kadhaa.

Nikuombe Mheshimiwa Waziri, Mradi ule hauelekei tu upande huo, Mradi ule pia unahudumia kipande cha kutoka Kata ya Gwata na Maghimbi ambavyo viro ndani ya Jimbo la Wilaya ya Kibaha Vijijini. Lakini upande ule wa Jimbo la Kibaha Vijijini upatikanaji wa maji ni wa shida sana, kwa sababu inaonekana wale watumishi hawafungui pale kwenye maunganisho yanayopeleka maji kule. Kwa hiyo Chalinze maji yanatoka lakini Gwata maji hayapatikani, Magindu maji hayapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kitendo hiki kunapelekea wananchi wa Kata hizo wawe na maswali ya sintofahamu. Na wanatafakari maswali ambayo kwa kweli mimi kama Mbunge siwezi kuyauliza na kuyazungumza hapa. Sasa, niwaombe watumishi waweze kuzingatia utoaji wa maji kwenye mradi ule kwa maeneo yote ambayo bomba hilo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

limepita kwa sababu linahitaji kuwahudumia watanzania wote kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye maeneo hayo ambayo ninasema kutokana na zile fedha ambazo Mheshimiwa Rais amezitamka siku ile ya tarehe 22 ni vyema tukafikiria kupeleka maji kutoka kwenye bomba kubwa kutoka pale linapotoka Gumba kwenda Ndwtati, Kigoda na Ngware, ambako hawana kabisa maji na bomba limepita karibu na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo upo Mji wa Mlandizi, Mji wa Mlandizi ndiko kwenye mtambo mkubwa sana wa maji unaozalishwa kupeleka Dar es Salaam. Wabunge wote wanaozungumza wa Mkoa wa Dar es Salaam wanazungumzia mtambo ambao uko pale Mlandizi. Cha kusikitisha ni kwamba Mlandizi palepale vipo vitongoji ambavyo havina maji, wanatumia maji ya kisima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba tunafahamu kwamba mtambo ule ni kwa watu wote, lakini ni vizuri basi watu wa Vitongoji vya Msongora, Kidai, Kisadi, Madimla, Mwanabwito, Kikongo, Mkino na Lupunga wangeweza kupatiwa maji kwa sababu mtambo uko karibu na wao na bomba kubwa haliko mbali kutoka kwenye maeneo ambao wao wapo. Lakini cha kusikitisha maeneo hayo niliyoyataja wanatumia maji ya kisima, jambo ambalo kwa kweli siyo zuri. Tunatakiwa tuwapatie maji safi na salama na ufumbuzi wake ni kuwaunganisha kwenye bomba la maji ambalo linatoka pale katika Mradi wa DAWASA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na haya nimalizie kwa kuishukuru Serikali. Nimeona kwenye Kitabu cha Bajeti na kwenye Hotuba ya Waziri, katika miradi mipyä inayokwenda kutekelezwa kuna Miradi ya Kwala, Kimara Misale, Ruvu station na Mradi wa Vinyenze, Uyombo na Masaki. Kwa kweli niishukuru Serikali kwa kupanga miradi hii ambayo itatekelezwa kwenye Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa nataka nitoe angalizo kidogo kwenye eneo lile la Kwala. Kwala ni eneo kubwa la kimkakati na sote tunafahamu kwamba eneo lile tumeliandaa kwa ajili uwekezaji wa viwanda na bahati nzuri wameshapatikana wawekezaji wa kuweza kujenga viwanda kwenye eneo lile. Huu Mradi kwa kadri ambavyo uliandaliwa, kwa sababu unasimamiwa na *RUWASA*, na mimi ninaufahamu Mradi huu kwa jinsi ulivyodizainiwa ulikuwa unaishia pale kwenye eneo la katikati katika maeneo ya Kwala. Lile eneo la viwanda haukuwa na mpango wa kupelekwa maji kwa sababu kulikuwa ni eneo kubwa la wazi.

Sasa kwa sababu tumeshapata wawekezaji na tayari wana nguvu ya kutaka kwenda kuwekeza pale; ningewashauri na ningomba sana Serikali tufanye utaratibu wa kuutanua huu Mradi Kwala ufile kule kwenye maeneo ya Kwala ili wakati wanaana ujenzi watu hawa wasiwe wanapata tabu ya tatizo la maji. Waweze kuhakikisha kwamba ujenzi unaendelea na maendeleo ya hilo eneo uwe unatekelezwa kwa kadri ambavyo mradi umekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuna Mradi wa Mpiji ambapo amesema ulikuwa umekamilika kwa utekelezaji. Mheshimiwa Waziri naomba nikujulishe kwamba mradi huu kweli umekamilika lakini kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa majie. Hii ni kwa sababu chanzo ambacho wanakitumia katika huu mradi nikuunganisha kwenye bomba kubwa la *DAWASA* ambalo linaunganishiwa pale Tumbi. Lakini kutokana na mazingira yaliyopo na bomba lilouanganishiwa Tumbi kuwa dogo maeneo haya Mpiji pamoja na Boko Mnemela hayapati maji kabisa. Hayapati maji kwa sababu inaonekana sehemu ambayo wameunganisha haina nguvu ya kutosha kupeleka maji kwenye maeneo haya. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utoe maelekezo yako kwa watendaji wa *DAWASA* ikiwezekana walibadilishe lile bomba dogo ambalo wanasema linaanzia pale kwenye kile chanzo ili waweke bomba linalofanana na kupeleka maji kwenye maeneo haya ili tuweze kuondoa adha hiyo ya watanzania kwenye maeneo haya.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwakamo kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze wakati huo Profesa Shukrani Elisha Manya, Dkt. John Danielson Pallangyo na Mheshimiwa Kanyasu unajiandaa.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameweza kutupa afya kuweza kuingia hapa Bungeni tuweze kujadili mambo ya Kitaifa, mambo ya maendeleo ya wananchi wa nchi yetu ya Tanzania na kwenye Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi kwanza ni sema kwamba naunga mkono hoja Wizara hii. Vilevile nimpongeze Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya katika nchi yetu na katika majimbo yetu. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wote wanaoendelea kumsaidia kwenye Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nijikite katika maeneo ambayo fedha zimekuja na zimeweza kutatua matatizo katika Jimbo langu. Zimekuja milioni 645 katika Vijiji vya Mwakizega na Kabeba; huu Mradi ulikuwa umekwama kwa muda mrefu. Imekuja milioni 43 kwa Kijiji cha Sunuka kwa ajili ya ujenzi wa tenki la maji lita 150,000. Pia imekuja milioni 992 kwa ajili ya Vijiji vya Sigunga na Kangwena Mkandarasi amepelekwa pale tarehe 07 mwezi huu wa Tano. Lakini pia 1,600,000,000.00 kwa ajili ya Vijiji vya Herembe pamja na Kaparamsenga. Mradi huu bado unafanyiwa *vetting*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia milioni 281 kwenda Kijiji cha Mdabazi kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati huu Mradi ni wa muda mrefu lakini ulikuwa kidogo hautoi maji lakini mpaka leo nilikuwa naongea na Diwani bado kuna shida kidogo. Lakini kuna milioni 281 ambayo imetengwa kwa ajili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya kufanya ukarabari. Milioni 450 ni kwa ajili ya Kijiji cha Kashaguru. Pia milioni 495 Vijiji vya Mlela na Kandaga. Mkandarasi yupo *site*; ingawa fedha ilichelewa kufika lakini juzi niliambiwa wamelipwa na wanaendelea na Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, milioni 650 kwa ajili ya Kijiji cha Malagarasi Mkandarasi yupo anaendelea. Milioni 87 kwa ajili Vijiji vya Basanza na Msebeyi hivi sasa gari za kuchimba visima viwili ziko pale kwa ajili ya Basanza na Msebeyi. Milioni 132 Kijiji cha Rukoma ukarabati, huu Mradi ni wa mwaka 2012, ni mradi wa muda mrefu sana. Ulikwama kwa sababu ya ubadhirifu wa wale wanaopewa kazi ya kutengeneza mradi huu, lakini nashukuru kwamba hii milioni 132 tayari hata nilikuwa naongea na Mwenyekiti leo wa Kijiji kuna baadhi ya sehemu maji yameanza kutoka. Hata hivyo kwenye tenki lenyewe yalikuwa hata hayafiki lakini Mwenyekiti amethibitishia Kijiji kwamba maji yanaingia kwenye tenki na limejaa; kwa bado sasa namna ya kuepeleka maji kwenye magati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili kwa kweli inasikitisha sana kwa sababu tangu mwaka 2012 ni muda mrefu sana ni miaka 10 wananchi wanasubiri maji na fedha imepelekwa pale. Yaani unaweza kuona jinsi ambavyo watendaji wanavyoichonganisha Serikali na wananchi, kabisa, haipendezi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tukimaliza Bunge hili twenda ukaone kabisa wananchi watafurahi sana na mimi nitafurahi sana, mimi naomba niende na wewe mwenyewe Waziri kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia 2,400,000,000.00 Kijiji cha Kaziromimba Mradi uko pale lakini bahati mbaya sana Kijiji kile, Mheshimiwa Waziri jambo la kusikitisha sana, naomba unisikilize. Kuna tenki ambalo liliagizwa kwa ajili ya Mradi ule liko Bandarini sasa hivi ni mwezi wa tatu. Wananchi wanajiuliza hivi lile tenki ambalo tulahidiwa kwamba linakuja, limetoka nje ya nchi limekuja mpaka Bandarini mbona bado liko pale Bandarini? Na mimi Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie

kabisa pamoja na kwamba nimekushukuru na kukupongeza lakini kwenye eneo hili nakusudia kushika shilingi yako kama hukutoa maelezo mazuri ni lini tenki hili litatoka Dar es Salaam Bandarini kwenda pale Kazuramimba ili wananchi wakazi wanaokaribia kufika 48,000 waweze kufaidi maji. Lakini pia katika eneo la Kijiji cha Uvinza ambacho ndiyo chenye jina ambalo kimebeba Makao Makuu ya Wilaya. Kijiji kile Mheshimiwa Makamu wa Rais juzi juzi alisimamishwa pale wakalalamika kwamba Kijiji kile hakina maji, lakini mimi nilivyofuatilia ni kweli kijiji kina maji, lakini Vitongoji vyake ndiyo bado havijapelekewa maji. Na hili Mheshimiwa Makamu wa Rais alinipigia simu kunipa taarifa kwamba Mbunge angalia kwa nini wananchi wa Uvinza wanalamika maji. Maji yapo lakini kwenye maeneo ya Vitongoji ndiyo maji hayajafika. Lakini pia pale Makao Makuu ya Halmashauri bado kuna shida ya mtandao wa maji mradi wa maji pale bado kuna shida, ni kizungurumkuti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Nguruka, Mradi ule ulikamilika vizuri lakini bahati mbaya sana haufanyi kazi vizuri na wananchi wameshindwa kuupokea kwa maana ya matumizi kwa sababu ule mradi chanzo chake kwa maana ya *pump* inatumia mafuta ya *petrol*.

Kwa hiyo sasa unaweza ukaona kwamba gherama ni kubwa mimi nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri kwenye chanzo kile cha maji basi kwa kuwa umeme haujafika basi tuweke miundombinu ya *solar* ili wananchi waweze kufaidi maji ambayo kidogo yatakuwa na nafuu pale Nguruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nguruka imebeba Kata mbili, kwa maana ya Kata ya Nguruka yenye na Kata ya Itebula, kwa hiyo unaweza ukaona kwamba Mradi huu ni mradi mzuri sana na umeshakamilika lakini wananchi wameshindwa ku-*afford* bei kwa sababu ya mafuta ile *pump* inayosukuma yale mafuta. Lakini pia ninajua utatuletea fedha mwaka huu wa fedha lakini bado kuna Vijiji vingi sana havijapata maji kwa mfano Vijiji vya Kata ya Mgabo vyote vitano havijapata maji, Kata ya Mtego wa Noti vyote havijapata maji Nachakulu haijapata maji ni Vijiji vingi sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nilikuwa nadhani katika eneo hili wengi wamesema na mimi naomba niseme lakini nashukuru kwamba kwenye Hotuba yako umeongea vizuri kwamba unakusudia kutumia vyanzo vyaa maji yanayotokana na Ziwa ili yaweze kusaidia kwenye maeneo hayo. Kwa mfano Ziwa Tanganyika ni chanzo kizuri cha maji kwa nini kisitumike hiki? Wabunge wengi wamelalamika ametoka kuzungumza Mbunge mwenzangu wa Sumbawanga kule, lakini Wabunge....

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bidyanguze, muda wako umekwisha.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: ... kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri katika eneo hili chanzo cha Ziwa Tanganyika kiweze kutumika. Ahsante sana, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya.

MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika Hotuba ya Bateji ya Wizara ya Maji ambayo kwa Mwaka huu wa Fedha inakwenda kutumia bilioni 709.36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipende kupongeza na kutambua jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Maji, na hasa dhamira njema na utashi kwa Mheshimiwa Rais wa kuwapatia wananchi wake maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani pamoja na matumizi mengineyo. Ni jitihada hizi za Serikali ambazo sasa tunaona dhamira njema ya Mheshimiwa Rais. Tunaongelea Mradi Mkubwa unaotoa maji kutoka Ziwa Victoria kuleta katika Makao Makuu ya nchi hapa Dodoma. Hili linatambua neema ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia, ukiiangalia Jiografia ya Afrika utagundua

kwamba sisi ni moja ya nchi ambayo tumebarikiwa sana kuzungukwa na Maziwa Makuu matatu tena mojawapo ni Ziwa Tanganyika likiwa ni moja ya Ziwa lenye kina kirefu katika Maziwa ya hapa Duniani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na kwamba hesabu si nyepesi kihivyo lakini kutoka Ziwa Victoria kuja Dodoma ni kilomita 700. Ukichukua umbali huo huo kutoka Ziwa Tanganyika au kutoka Ziwa Nyasa utagundua kwamba kama tukivitumia vyanzo vikuu hivi vitatu nusu ya nchi ya Tanzania inapaswa kuwa *supplied* na maji bila kutafuta vyanzo vidogo vidogo vinavyokauka. Kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza sana kwamba kwa dhamira njema ya Mheshimiwa Rais na utashi wa Serikali kama tumethubutu kubuni Mradi unaotoka Ziwa Victoria hadi Dodoma, utashi huo huo uelekezwe katika vyanzo vikuu vingine vya Ziwa Tanganyika ambalo ni Ziwa lenye kina kirefu, maji ambayo hayatakauka na Ziwa Nyasa na tuone kwamba vyanzo hivi vingine vidogo vidogo ndivyo vihudumie sehemu nyingine ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo matatu. Jambo la kwanza ni mfumo wa uondoaji maji taka pamoja na usafi wa mijji. Hadi sasa kwa kadri ya ripoti ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba tumefanikiwa kuwa na mifumo hiyo kwa asilimia 15 na kwamba lengo letu ni kwenda asilimia 30 ifikapo mwaka 2025. Na utangundua kwamba tuna miaka mitatu ambayo imebaki na sisi ndiyo tuko nusu ya mwendo. Sasa nipende pia kutambua kwamba kama hatuwezi kuwa na uondoshaji na mifumo mizuri ya kuondoa maji taka katika mijji yetu, mijji yetu inakuwa siyo misafi na ndiyo maana utakuta mito inayotiririka katika mijji yetu siyo misafi. Lakini katika nchi za wenzetu maeneo ambapo unakuwa na baraka ya mto kupita katikati ya Mji ndiyo maeneo ambayo yamefanywa kuwa ya vivutio, sehemu za utalii na mito inajengwa kiasi kwamba hata boti zinapita, watu wanafanya sherehe mle. Lakini sisi kwa sababu ya kutokuwa na mifumo mizuri mito yetu inakuwa inatiririsha maji taka. Na hilo Mheshimiwa Waziri nilizani kwamba Serikali iweze kutoa msukumo mkubwa ili kwamba Miji yetu iweze

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuwa misafi. Kwa hiyo, Wizara ya Ardhi hapa pamoja Mipango Miji watusaidie, wananchi wasitutangulie ili kwamba tunapopanga makazi basi na mifumo ile ya kuondoa maji taka iweze kupangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu mabwawa ya Kimkakati ya Farkwa pamoja na Kidunda; yameongelewa na Wabunge wenhgi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati miradi hii inaibuliwa ni kweli kwamba idadi ya watu katika miji husika ilikuwa ni ndogo. Sasa kama tunaiita kwamba ni miradi ya kimkakati maana yake ni kwamba hata tengeo lake la fedha linapaswa kuwa la kimkakati. Haliwezi kusubiri bajeti ya kila mwaka kwa sababu la sivyo idadi ya watu itazidi kuongezeka katika miji, watu watakosa maji na tutajikuta kwamba tunashindwa kuwa na miji ambayo ni salama ni misafi na pla miji inakuwa hailingani na maendeleo tunayoyataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri nilidhani kwamba hebu tuendelee kulipanga kimkakati, na hasa haya mawili; kwa sababu Farkwa inapaswa ihudumie hapa Makao Makuu ya Nchi, lakini pia Dar es Salaam tunaona kwamba idadi ya watu inazidi kuongezeka. Kama wewe mwenyewe ulivyosema chanzo cha Ruvu kilionesha kukauka mwaka uliopita. Kwa hiyo, hili lazima lipangwe kimkakati ili tuweze kuwasaidia wananchi wa maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kuongelea ni ujenzi wa mabwawa wa ukubwa na malambo madogo. Tumeendelea kushuhudia kwamba utekelezaji wa miradi hii mingine inafanikiwa lakini mingine haifanikiwi; na ni kwa sababu miradi inakamilika halafu kiongozi wa kitaifa anakwenda kukagua anakuja kupewa taarifa ya kwamba mradi huu siyo thamani ya fedha. Sasa hapa nadhani tunapaswa Serikali ifanye mkakati kwamba tunapeleka fedha nyangi sana katika kujenga haya malambo. Sasa mimi pendekezo langu, ili isitokee Kiongozi wa Kitaifa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

anakwenda kwenye mradi halafu anakuta mradi umetengenezwa vibaya tuwe na kamati za *continues monitoring and evaluation* zinazohusisha viongozo wa Tamisemi; ili Waziri wa Maji anapokwenda au Waziri Mkuu anapokwenda kukagua mwisho wa wakati basi hata Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya pamoja na timu yote ya Tamisemi wanaweza kuwajibika kwamba tuliukagua kila wakati na hivyo tutaondokana na dhana ya fedha kutolewa lakini mradi unakuja kukataliwa kwa sababu fedha zimetumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama, Kamati hizi za *Continues Monitoring and Evaluation* zitakuwa zinagharimu fedha kidogo; tuzitumie ili kuepuka miradi kuja kukataliwa kwa sababu imekuwa inatumika vibaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja na ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa Shukrani Elisha Manya kwa mchango wako na kwa kuzingatia muda pia. Nilimuita Mheshimiwa John Danielson Pallangyo wakati huo Mheshimiwa Constatine Kanyasu anajiaandaa.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye hoja hii ambayo ipo mezani; na nijielekeze moja kwa katika pongezi. Nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso na Naibu wake pamoja na watendaji wote pale Wizarani, nikianza na Katibu Mkuu, Wakurugenzi lakini pia Mtendaji Mkuu wa RUWASA, Injinia Clement kwa kweli wameonesha wanatekeleza shughuli zao vizuri sana na wanastahili pongezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia taarifa ya utekelezaji kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hali ya upatikanaji wa maji lengo mpaka 2025 kwa upande wa vijini ni asilimia 85 lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza Wizara imeshafanikiwa kwa kiwango cha Asilimia 74.5 upatikanaji wa maji safi na salama vijijini; lakini pia asilimia 86.5 kwa upatikanaji wa maji salama mijini. Haya ni mafanikio

makubwa sana, tunaendelea kuwapongeza Waziri na timu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio katika utekelezaji wa miradi mpaka tunavyozungumza sasa hivi kwa mwaka wa fedha tunaoumalizia, Wizara imekwishatekeleza miradi kwa kiwango cha *percent* 95. Hayo ni mafanikio makubwa sana, na tunapongeza wizara kwa kazi nzuri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma Pugu miaka ya nyuma hiyo, wakati nasoma pale *A level/tatizo la maji liliwu* *nightmare*. Lakini mwezi Machi nilikwenda kule nikiwa kwenye ziara ya Kamati yetu nikakuta Wizara imetekeleza mradi, pale Kisarawe kuna tanki la lita milioni 10 na kuelekea upande wa Pugu kuna tanki la lita milioni mbili maana yake ni kwamba lile tatizo la maji Pugu limemalizika. Nilifurahi mno, nilibubujika furaha; nichukue nafasi hii kwa kweli kipekee kabisa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wizarani kwa kazi nzuri ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mafanikio ya wizara hayakuishia Pugu hata kule jimboni kwangu mambo ni mazuri. Kuna mradi ambao unaendelea sasa hivi katika Kata ya Keri na kwa Lusambu mradi wa maji Kijiji cha Patandi wenyewe thamani ya shilingi bilioni 2.7, Mkandarasi yupo kazini. Tunashukuru sana na tunapongeza Serikali kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, kuna mradi wa milioni 379 Kijiji cha Nshupu wa uboreshaji, kazi inaendelea tunaishukuru sana Serikali na kumpongeza Waziri. Pia kuna Mradi wa Kijiji cha Nkure milioni 502 wa fedha za UVIKO utekelezaji unaendelea, tunaishukuru na kuipongeza Serikali. Aidha, wakati Waziri walivyokuja kwenye ziara jimboni kwangu kukabidhi Kituo cha Utafiti wa Kuondoa Madini ya Fluoride kwenye Maji ambapo ilikuwa kinakabidhiwa Chuo cha Maji, Mheshimiwa Waziri ali-*initiate* mradi wa kuboresha upatikanaji wa maji Kijiji cha Kiwawa na Ngongongare na akatoa Shilingi milioni 100 kama fedha za awali. Mradi ule ni Shilingi bilioni, 1.6. Kazi inaendelea na *RUWASA* na *AUSA*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanashughulikia hiyo kazi. Tunashukuru na kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa Imbasen, Kikatiti na Maji ya chai wa gharama ya Shilingi billioni nne. Nasikia sasa hivi utekelezaji bado upo kwenye *stage* ya manunuzi. Tunashindwa kuelewa ni kwanini huo mradi umechelewa sana kwa sababu ulikuwa unapaswa uanze wakati mmoja na mradi wa Patandi. Niweke angalizo kwamba inaelekea *RUWASA* wanakumbatia sana sana taratibu za manunuzi, hawajaweza kuzi-*delegate* chini kwa Mamlaka za Mkoa na Wilaya. Ni vizuri wakafanya *delegation* ili hizi kazi zikafanyika haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mafanikio ya wizara si bure, ni *reflection* ya kazi nzuri ambayo inafanywa na Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. Nichukue nafasi hii kipekee kabisa na kwa dhati ya moyo wangu kumpongeza kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, anatubeba Watanzania kama watoto wake. Hata ukiangalia anavyohangaika; juzi tulizindua Filamu ya *Royal Tour* ambayo kimsingi imekuja kuitangaza nchi yetu hasa kwenye utalii. Yote kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watanzania tunatoka hapa tulipo tunakuza utalii kwa maendeleo ya nchi hii. Lakini pia mwaka jana alituletea fedha za maendeleo nje ya bajeti ambapo hivi fedha milioni 502 ambazo na sisi tumepata Kijiji cha Nkure zilielekezwa kutoka kwenye lile fungu Shilingi trillioni 1.3.; tunamshukuru na tunampongeza tunamuombea maisha marefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi ya kuzungumza lakini nasiki kengele imeshalia, basi nichukue nafasi hii kukushukuru sana naunga mkono hoja, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana, sasa namuita Mheshimiwa Constatine Kanyasu aweze kuchangia.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba pia nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Lakini kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya, nawapongeza sana; sisi ambaao tumekuwa tukiomba maji kwa miaka mingi tangu Bunge lililokwisha mpaka sasa tunaona kazi kubwa ambayo Serikali inafanya kwa sababu kuna sehemu maji yamefika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Geita Mjini inaaminika kwamba ni miongoni mwa miji inayokua kwa kasi zaidi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Sababu za kukua kwa Mji wa Geita ni uwepo wa shughuli nyingi zinazohamasisha watu kuja, za kiuchumi, ikiwemo madini. Ongezeko la watu linaongeza sana uwekezaji; na kwa bahati nzuri sana ni kwamba Mji wa Geita Mjini maji yako km 8 kutoka katikati ya mji kwenda Ziwani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nianze kuishukuru sana Serikali. Kwanza katika ukurasa wa 53 Serikali inasema mchakato mzima wa miji 24 umekamilika na kwamba sasa utekelezaji utaanza tunakushukuru sana. tunamshukuru Mheshimiwa Rais tulimsikia siku ya wiki ya maji; na tunaamini kwamba kabla Bunge hili halijaisha Mheshimiwa Waziri tunaamini Mheshimiwa Rais atatuzindulia mradi huo uweze kuanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali pia tumepata fedha kwa ajili ya kupanua chanzo cha maji; na naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza sana *GEUWASA* wanafanya kazi yao vizuri, wanafanya kazi yao vizuri katika Mji wa Geita na kwa kweli wanastahili pongezi.

Sasa tunapanua chanzo cha maji umetupa bilioni moja, tunashukuru sana. Lakini yale maji yanatoka Nungwe; yakinika Nungwe yanapita Manga, Nyakabale na kwenye Kata ya Mgusu. Kule yanapotoka maji, maji wanayopata ni yale ambayo hayajasafishwa; yanayouja kwenye bomba ambalo linatoa maji ziwani; kwa hiyo, ili wapate maji safi inabidi maji yafike Geita Mjini halifu yarudi km 8 kule yanakosafishwa, kule hakuna usambazaji wa maji. kwa hiyo Mheshimiwa Waziri pamoja na sifa hizi za *GEUWASA* nadhani

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

GEUWASA wanastahili kuongezewa fedha ili wapeleke mtandao wa maji na salama kule yanapotoka maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya Mji wa Geita ni takribani lita milioni 18 mpaka milioni 20. Sasa hivi tunapata lita milioni tano. Kitakapotanuliwa hiki chanzo cha maji tunaamini kitatusogeza karibu lita milioni 8, bado tutakuwa na *gape* ya takriban lita milioni 12. Jambo pekee ambalo linanipa faraja ni kwamba utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji unaanza. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri naomba kuishukuru Serikali, mwaka huu wa fedha unaokwisha tulipata fedha na tumepeleka maji katika mitaa takriban 12; na tumejenga matenki mapya takriban matatu. Sasa nimeona kwenye bajeti yako ya sasa unatupatia fedha kwa ajili ya kuongeza usambazaji wa maji kwenye Kata za Shiloleli na Bulela.

Mheshimiwa Waziri zipo kata zingine ambazo tumetafiti maji ya visima yamekosekana; pamoja na kusubiri maji ya bomba Kata za Nyanguku na za Ihanamilo kila walipochimba visima *RUWASA* walikosa maji. Sasa niombe, wakati tunasubiri mradi huo ambao utachukua takriban miaka mitatu, wananchi hawa, kama unavyosema mwenyewe Kwamba hakuna mbadala wa maji, waweze kutafutiwa njia nyingine ya kupata maji salama na safi kwa ajili ya maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo, ni kwa sababu kila inapofika kiangazi, wananchi wa Kata za Nyanguku na Ihanamilo wanaanza kusafiri kutafuta maji kama vile wanavyosafiri watu wa Mikoa ya nchi kavu kama Shinyanga na wapi huko na matela ya ng'ombe kwenda kutafuta maji kwenye mabwawa; lakini sisi tupo kilomita nane kutoka ziwani. Kwa hiyo naamini kwamba, jambo hili linaweza kutafutiwa ufumbuzi katika kipindi hiki ambacho Serikali bado hajasaini na hatujaanza mkataba huo mkubwa wa kupeleka maji. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri juzi niliuliza swali hapa na ulisema kwamba Serikali itaanza mchakato kwa ajili ya ukarabati wa bwawa la Kasamwa, nashukuru sana nimeona kwamba mchakato huo utaanza. Mji wa Kasamwa ni Mji wa pili kwa ukubwa katika Jimbo la Geita Mjini; tuna watu takribani 25,000 mpaka 30,000. Vilevile ni mji ambao unashughuli nydingi za kiuchumi. Tuna maji ya visima, maji ya bomba ya kutoka Ziwa Victoria hayajafika. Tunashukuru kwenye mpango maji yatafika kwenye Mji wa Kasamwa. Kwa hiyo, ombi langu hapa ni kwamba katika fedha hizi chache ambazo tutapata mtuongezee fedha ili huu Mji wa Kaswamwa mtandao wa maji haya ya visima pamoja na kwamba kuna kisima Kanyala na kuna tenki limejengwa pale maji yawafikie wananchi takriban 30,000 ya huu Mji Mdogo wa Kaswamwa. Kwa sababu huu mji ni mkubwa na kama visima hivi viwili vilivyopo vitaendelea kuwepo, uwezekano wa kiangazi maji yanapopungua kupata shida ya maji ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, naamni kwamba kama ambavyo watu wote wamekupongeza; wananchi wa Geita Mjini wana matumaini makubwa na wizara yako na kazi nzuri unayoifanya wewe na Naibu wako. Tunaomba tu Mheshimiwa Rais aturahishie mradi wa Miji 24 ili tuweze kupata maji safi na salama. Nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu, namuita Mheshimiwa Timoth Mnzava aweze kuchangia. Wakati huo naomba niwataje watakaofuatia, Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutujaalia uzima na kutuwezesha kuifanya kazi hii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mimi kwa kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Timu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yenu yote mnafanyakazi nzuri sana na kazi yenu inatubariki sana; tunawapongeza tunawatia moyo muendelee na kazi hiyo. Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara yako siyo ninyi tu Wizarani hata ukienda kwenye taasisi zenu sisi wa vijijini tunabarikiwa na kazi nzuri sana inayofanywa na wenzetu wa RUWASA. Mkurugenzi Mkuu anajitahidi anafanyakazi vizuri. Kule Tanga sisi Injinia wetu wa Mkoa anafanyakazi nzuri na kipekee sana Meneja wetu wa RUWASA wa wilaya na timu yake nzima. Kwenye kazi huweza kuwa kuna changamaoto lakini kijana yule anajitahidi anafanyakazi nzuri muendelee kumtia moyo sisi tunamtegemea na anaifanyakazi vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Waziri na timu yake, napenda nitumie nafasi hii katika kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maji, kumpongeza sana sasa sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa mawili; jambo la kwanza kwa kujiongeza na kutafuta fedha nje ya utaratibu wetu; fedha kwa ajili ya UVIKO, zimetusaidia sana kwenye upande pia wa sekta ya maji. Jambo la pili, kipekee ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake; kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye ule ukurasa wa 10 mpaka Mwezi Aprili, wizara imepokea fedha kwa asilimia 95 ya matarajio tuliyoyaweka kwenye bajeti. Tunavyosema mama anaupiga mwangi wako watu wengine wanakuwa na mashaka mashaka na wengine wanakuwa na maswali. Kunawezi kuwa na changamoto za ndani, za kitaifa lakini haiondoi ukweli kwamba mama anaupiga mwangi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwenye hili nitafanya tu rejea ya maeneo machache. Tumepokea fedha kwa asilimia 95 mpaka Mwezi Aprili, 2022. Nimekwenda kutafuta hotuba za bajeti za Wizara ya Maji, nikachukua na maandiko mengine, mwaka 2017/2018 mpaka mwezi Machi, 2018 fedha za maendeleo zilitoka kwa asilimia 12.3, matumizi ya kawaida ilitoka asilimia 73. Mwaka 2018/2019 mpaka mwezi Machi, 2019 fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa asilimia 68, fedha za maendeleo zilitoka kwa asilimia 51; nimekwenda Mwaka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2019/2020 matumizi ya kawaida tulipewa kwa asilimia 70 mpaka mwezi Machi, matumizi ya maendeleo kwa asilimia 74. Lakini mwaka uliopita 2021 Mpaka mwezi Aprili, 2020 zillizotoka kwenye bajeti zilitoka kwa asilimia 72 kwa matumizi ya kawaida na asilimia 53.4 kwa matumizi ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza kwenye bajeti hii Wizara imepokea fedha kwa asilimia 95. Huu ndio ushahidi kwamba mama anaupiga mwingi sana. Kizuri zaidi sio tu kwenye kutoa fedha; sisi wote ni mashahidi, fedha zinatolewa kazi inafanyika na kazi inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukua mfano wa Jimbo la Korogwe Vijijini tuna miradi zaidi ya mitano ambayo imekamilika; na miradi sita ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali inaendelea sasa hivni na miradi milne tunatarajla kusaini mikataba wiki inayokuja na nina miradi mitano iko kwenye hatua mbalimbali za manunuzi hakika mama anaupiga mwingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kwa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais lakini na Serikali yake, na kwa hiyo kwa pongezi hizi mimi sina mambo mengi; nina maombi tu machache nikukumbushe wewe na wenzako wa Wizarani ili kazi iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi ule wa maji wa Vuga – Mlembule pale Mombo ni wa muda mrefu umeshatoa fedha. Kuna uzito kidogo kwa upande wa ule mradi wa kule Lushoto, ambako ndiko kwenye chanzo cha maji. Tusaidie kuongeza nguvu mradi huo ukamilike tuwape huduma ya maji watu wa Mombo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la pili, nimeona kwenye ukurasa wa 56, umesema vizuri sana kuhusu Mradi wa Maji wa Miji 28, na umesema tayari kila kitu kimekamilika tunasubiri kusaini utekelezaji wa miradi hii ukaanzu. Naendelea kukumbusha Wizara yako, katika ile miradi ya miji 28 ambayo inaanza sasa kwa fedha kutoka India; kuna miji

ya Muheza kwa akina Hamis, Handeni na Korogwe Mjini chanzo chao maji kiko pale Jimbo la Korogwe Vijiji Kata ya Mswaha. Ninakuomba sana kama tulivyokuwa tumeomba tangu mwanzoni tutakwenda kwenye utekelezaji, vile vijiji vilivyojirani na kile chanzo msikisahau vijiji vya hii Kata ya Mswaha viweze kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni mradi wa maji wa Mwanga – Same – Korogwe. Umeusema vizuri sana kwenye ukurasa wa 55 wa hotuba yako, na umeeleza changamoto ulizokutana nazo na hatua tulizochukua. Mimi nikuombe, baada ya kuitisha bajeti hapa hebu kaongeze nguvu jambo hili likamilike ili mradi huu ukamilike watu waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maombi hayo matatu ombi la nne, tulzungumza na Mheshimiwa Waziri kuhusu Bwawa la Mayuyu, na ulikuwa umeniahidi kwamba kesho ungekwenda kufanya ziara, na watu wa Korogwe wanakusubiri. Ninakuomba sana tuliangalie tuwajali wale watu bwawa lile ni bwawa muhimu ndilo wanadolitegemea kwa ajili ya kupata huduma za maji na huduma nyingine kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Mkoa wa Tanga ni mionganoni mwa mikoa nane ambayo haimo kwenye ule mradi wenu wa *EP4R*; na huko nyuma tumekuwa tukihudumiwa sana kwenye miradi yetu midogo midogo ilio mingi kuititia mradi wa *PbR*. Tunajua *program* ya *PbR* ndiyo inakwenda mwishoni *PbR5* ndiyo ya mwisho mradi *una-Phase Out*. Tunawaomba sana Wizarani mtusaidie kupata mradi mwingine wa aina hii au mtuunganishe na wenzetu wale wengine ambaao wako kwenye *EP4R* na sisi tuweze kupata huduma za miradi hii midogo midogo ili wananchi wetu waweze kupata huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Mheshimiwa Waziri unatambua changamoto niliyonayo kwenye Kata za Mkomaizi, Mkalamo, Magambo Kwalukonge na Mpale. Kata hizi zinachangamoto kubwa ya vyanzo vya maji. Tumeamua

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na ninyi Wizarani mliamua kutusaidia mradi mkubwa kutoka kwenye maji ya Mto Ruvu. Mkatuhidi kututafutia mshauri kwaajili ya kuja kufanya kazi ya usanifu na upembuzi yakinifu. Tunaomba mchakato huu uharakishwe kidogo, tumeusubiri kwa muda mrefu ili mambo yaende vizuri ili tumalize maeneo haya machache, tuunganishe na yale maeneo mengine makubwa ambayo watu wa Korogwe wanapatia huduma ya maji ili mambo yao yaweze kwenda kuwa vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja ninawatachia kila la kheri katika kutekeleza bajeti mtakayopitisha. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mbunge wa Korogwe Vijiji. Nilimuita Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Waziri wetu wa maji ndugu yetu Jumaa Aweso na *Engineer Maryprisca Mahundi*, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, viongozi wa mamlaka za maji, *RUWASA* na wale wa mabonde kusema ukweli hawa watu wanafanyakazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi inavyoiangalia kwa jicho la huruma hii Wizara yetu ya Maji. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba vijiji wanapata maji kwa asilimia 85 na mijini asilimia 95. Mpaka sasa hivi vijiji tumeshafikisha asilimia 74.5 na mijini tumeshafikisha asilimia 86.5. Kwa hiyo naipongeza Serikali kwa jinsi inavyopeleka fedha za kutosha katika Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ilikuwa imetenga Shilingi Bilioni 785.9, na hadi kufikia mwezi Machi tulishapeleka asilimia takriban 77, bado asilimia 23 tu. Kwa hiyo, najua Serikali ikimalizia hii asilimia 23 iliyobakia Wizara itaendelea kufanyakazi nzuri; na kutohana na upatikanaji huu wa fedha, Jumaa Aweso na wenzake wanafanyakazi nzuri wanang'ara

vizuri kabisa. Wamejitatihidi kuhakikisha kwamba ile kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani wanaitekeleza kwa vitendo kwa sababu kuna fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane kwamba takriban kila Mbunge hapa ana mradi mmoja au miwili ya maji. Kwa hiyo nitashangaa tunapopitisha bajeti ya Wizara hii; mimi ninawaomba kwa sababu mimi ni Mbunge wa Kamati inayoisimamia hii Wizara tupitishe ili Jumaa na wenzake wakafanye kazi vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia Wizara hii tulitembelea miradi ya maji kukagua kama wanafanyakazi vizuri. Tukaenda katika mradi wa Kimbiji – Mpera huko Dar es Salaam tukatembelea mradi wa Mlandizi – Chalinze, tumeona maajabu, *DAWASA* wanafanyakazi nzuri; na tulipendekeza, Mameneja wengine waende kwenye maeneo hayo wakajifunze jinsi ya kufanyakazi kama yule wa *DAWASA*, nampongezo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutembelea hii miradi lakini pia, katika hotuba ya Waziri ameonesha miradi ambayo imekamilika. Kwa mfano, kufikia mwezi wa Aprili miradi 303 ya vijijini ilikamilika, kuna miradi 127 iliyokuwa chechefu ameshakamilisha. Kuna miradi ya mijini 40 ambayo pia imeshakamilika. Yote hii ni kazi nzuri anayofanya Waziri pamoja na wenzake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu ameomba kupatiwa kiasi cha Shilingi Bilioni 657.9, na anategemea kukamilisha miradi na kutekeleza miradi mingi mipya ambayo kwa ujumla wake vijijini kuna miradi kama 1,029 yenye fedha nyingi ambazo ameonesha; mabwawa 15 na miradi ya mijini 175. Hii yote ni kazi nzuri ambayo Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inataka ifanyike ili akina mama wasipate shida ya maji. Kwa hiyo, nirudie tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tupitishe bajeti ili Jumaa aendelee akafanye kazi pamoja na wenzake. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudi kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijini kwa sababu kuna changamoto kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kata ambayo ninatoka ya Kibosho Kirima nikiri hapa kwamba Mbunge wenu huwa ninakwenda Jimboni kila nikitoka hapa, lakini mwaka mzima uliopita mwaka wote kwenye bomba langu pale nyumbani hakuna maji. Kwa hiyo najua una mipango mizuri naomba mtusaidie, ili mimi Mbunge wenu na wale wananchi wangu wapate maji ya kunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kibosho Kat i ambaayo ina vijiji 14 kati ya Kibosho kati na Kibosho Okaoni watu wameongezeka sana na mradi wa zamani hautoshelezi mahitaji ya watu pale. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri uangalie hizi Kata mbili vijiji 14 ni watu wengi, ili tuboreshe ile miundombinu wapate maji ya kunywa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kibosho Magharibi hapa kuna vijiji nane ambavyo havijapata maji. Kata hii kwa sasa hivi ilikuwa inapata maji kutoka eneo la Mheshimiwa Saashisha. Tunaiomba Wizara kwa jicho la huruma tutafute chanzo kwenye DC yetu, ili tuwaletee hawa watu maji ya kunywa nao wanufaik kama watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Mabogini kuna vijiji ambavyo tangu tupate uhuru vilikuwa havina hata maji ya mfereji kwa mfano, kule Umasaini. Niliuliza swali la nyongeza hapa bado narudia kukuomba Mheshimiwa Waziri kule Umasaini kule Remiti tuhakikishe tumepeleka maji ili wale wafugaji na wananchi wengine wapate maji ya kunywa.

Katika Kata ya *Old Moshi Mashariki* nakushukuru sana umenipa Shilingi milioni 400, *Engineer Kija Limbe* anajitahidi, lakini ninaomba, ikiwa ni pamoja na pale Kata ya Mbokomu, manunuzi myaboreshe ili hawa watu wapate maji ya kunywa na tuendelee kuisifia Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Katika Kata ya Kimochi pia nashukuru tulipata Shilingi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

500,000,000 kazi imeshaanza naomba tuchakarike ili hii miradi ionekane na watu wanufaik. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Uru Kusini katika ripoti ya *CAG* alisema kwamba yale maji ni machafu na hayafai kwa matumizi ya binadamu. Mheshimiwa Waziri watu wameshaogopa kwa sababu *CAG* ameshaandika kwamba yale maji yana matatizo. Naomba mje muangalie ili tuangalie tutakavyowasaidia hawa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaushauri kidogo; mambo ni mengi nitapeleka kwa maandishi. Kwa kuwa changamoto kubwa kule Kilimanjaro imekuwa ni upatikanaji wa vifaa ninashauri muwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba, *procurement* inafanyika mapema miradi inasainiwa mapema ile ambayo haihitaji *Force Account*. Kwa hiyo, manunuzi yafanyike ili hao Mameneja wetu wa *RUWASA* na yule Mkurugenzi wa *MUWASA* apate vifaa kwa wakati kwa sababu shida kubwa tumeona ni kwenye ununuzi wa vifaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa Ndakidemi kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Athuman Almas Maige aweze kuchangia.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana mimi kuniruhusu nichangie hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi naunga mkono pongezi zinazotolewa na Wabunge wenzangu kwa Wizara hii kwa ndugu yangu/mdogo wangu, Jumaa Aweso na Naibu Waziri Maryprisca Mahundi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii kwa kushirikiana na wenzao Mheshimiwa Katibu Mkuu *Engineer Sanga* na watumishi wengine wenye nidhamu nzuri sana katika Wizara hii hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha muda mfupi sana Wizara hii, Waziri huyu na wenzie wameokoa mamilioni ya fedha kutoka kwenye miradi iliyokuwa chechefu na hii haijapata kutokea kwa sababu miradi hii mingine imekaa miaka nenda rudi. Lakini pia nimehudhuria uzinduzi na Mheshimiwa Rais wa miradi mbalimbali kule Simanjiro Mugango, Kiabakari, Butiama na Misungwi. Miradi hii ilikuwa mikubwa sana na imepewa fedha na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na umeisimamia vizuri sana. Wizara hii haiwezi kupita bila hongera kubwa kutoka kwa Wabunge wote kwa sababu kila mahali Wizara hii imegusa tuwapongeze na hongera sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia kwa kazi nzuri ya kuyavuta maji kutoka Ziwa Victoria na kuyapeleka kwa babu zao Wanyamwezi Tabora, Igunga, Nzega na Uyui; maji yenye thamani ya Shilingi Billioni 615 na mradi ule umesimamiwa na unafanyakazi vizuri hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini pia sisi Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji tulitembelea miradi ya Kimbiji pamoja na Kisarawe II, ambayo ni miradi mikubwa imekaa muda mrefu sasa wameikwamua na inaendelea vizuri hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la upatikanaji wa fedha, ni lazima tuipongeze Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwapa fedha Wizara hii kwa kiwango cha asilimia 95 cha mahitaji yao ya fedha zilizokuwa zimepangwa. Hongera sana mama Samia Suluhu Hassan. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto katika Wizara hii ambazo hatuwezi kukaa kimya kwa sababu tunataka tuwasaidie na wao waweze kutusaidia. Kwanza, ukosefu wa mafundi, fundi mchundo na fundi sanifu. Miradi hii mikubwa ya maji ambayo tumeongelea hapa imefanikiwa kujengwa vizuri itahitaji matengenezo. Mimi ninashauri Wizara hii ifanyekazi karibu sana na Chuo chao cha Maji na wakiweshe, ili hatimaye wapate mafundi wa kutengeneza miradi hii itakapoharibika. Pia liko suala la kupungua kwa maji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wizara na Mamlaka zake zote za maji na *RUWASA* waanze sasa kufikiria jinsi ya kuhifadhi na kulinda vyanzo veya maji hasa Mito na ardhii oevu, kuvuna maji ya mvua, na ikiwezekana kuhifadhi maji hayo katika mabwawa makubwa badala ya kuacha yakapotea. Maji haya yanaweza kutokana na madaraja ya kwenye reli lakini pia na madaraja ya barabarani badala ya kuachwa yakafanye mafuriko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, suala la kumalizia miradi ambayo imeanzishwa mikubwa lakini bahati mbaya sana haikamiliki. Mfano mzuri, tulikuwa na mradi wa Ziwa Victoria kuleta maji Uyui, Tabora, Nzega na Igunga. Katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini kulikuwa na vijiji kadhaa ambavyo vimeorodheshwa; na Wizara hii ilibakisha fedha (bakaa) Shilingi Bilioni 25 na miradi hii kwenye vijiji hivyo ninavyovitaja vijiji vya Ikongoro, Kanyenye, Kiwembe, Mbiti na Mogwe gharama ya miradi ile yote kwenye vijiji hivyo ni kama Shilingi Bilioni 5 hivi. Walikuwa na Shilingi Bilioni 25 lakini vijiji vile mpaka leo havijapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina hakika hii hali ya kuacha miradi na fedha zipo inatuletea kasoro katika Wizara hii na mimi ninafikiri, Mheshimiwa Aweso na wenzake watarekebisha mara moja ili miradi itakayoanza na ambayo ina fedha ikamiliike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pia suala la makusanyo ya masurufu au fedha kwa ajili ya mamlaka zao za maji na *RUWASA*. Sasa hivi tunakusanya fedha hizi kwa kutumia dira au mita za maji, na kuna wasomaji. Sio vibaya ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Aweso, Naibu Waziri na Katibu Mkuu mkaiga wenzenu wa *TANESCO* ambaao waliiga mita za LUKU kutoka Afrika Kusini. Si vibaya na ninyi mkaiga hizi mita za LUKU; na tena niwapeni njia rahisi, mkaziita Lipia Maji Kadri unavyotumia (*LUMAKU*) na watu watakuwa tayari kulipia hayo maji kabla ya kuyatumia. Hii itaingiza mapato ya kutosha kwenye mamlaka za maji lakini pia *RUWASA*. Pia itaondoa gharama za udanganyifu wa watu wanaokwenda kusoma mita ambaao ni chechefu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Miji 28, tumeusikia; mimi naunga mkono, kwamba Waziri amesema kabla ya bajeti hii kabla ya mwezi Juni, mradi huu utaanza na kwamba Mheshimiwa Rais ameunga mkono na ameridhia mradi huu uanze. Hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nautaja mradi huu kwa sababu nami utanipitia utakapopita kwenda Sikonge. Utakapokwenda Urambo vijiji vyangu kadhaa vitapata maji na kutimiza jumla ya vijiji 58 katika Jimbo langu. Ukipita kwenda Urambo Vijiji vya Kata za Ndono, Ufuluma, Makazi, Mabama, Lakasisi A, Kalola na Isila vitapata maji kwa sababu viko ndani ya ile *kilometer* 12 za bomba la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mungu awatangulie na awape afya njema Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Jumaa Aweso, ndugu yangu Maryprisca Mahundi, *Engineer Sanga* na watumishi wote wa Wizara hii ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Athuman Almas Maige. Nilimuita Dkt. Florence George Samizi wakati huo Mheshimiwa Asenga Abubakari na Mheshimiwa Deus Clement Sangu wanajandaa.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza Rais wetu mama yetu mpenzi, kwa jinsi ambavyo anatekeleza ahadi yake ya kumtua mama ndoo kichwani kwa vitendo. Tumeshuhudia jinsi ambavyo ametoa fedha kwa asilimia 95 kwa Wizara hii. Ni pongezi kubwa sana tunamshukuru mama Mwenyezi Mungu aendeleee kumbariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kuwapongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waziri lakini na Katibu Mkuu *Engineer*Sanga. Kwa kweli Wizara hii imekuwa faraja kwetu. Tunapokwenda pale hata kama hujapewa fedha lakini unaondoka umecheka ni wakarimu ni Rahim wanatujibu vizuri wanatusikiliza; kwa kweli endeleeni kupiga kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana *Engineer* Mwenda wa Mkoa wa Kigoma kwa ushirikiano anaotupa pamoja na watendaji wake wote; *Engineer* Aida, *Engineer* Almasi wanafanya vizuri sana pale katika Jimbo la Muhamwe kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuishukuru Serikali kwa miradi ya maji vijiji ambayo imetekelawa katika Jimbo la Muhamwe. Tumeupokea mradi wa maji katika Kijiji cha Mkarazi wenyewe thamani ya bilioni 1.2. Tumeupokea mradi wa maji katika Kijiji cha Mkabuye wenyewe thamani ya bilioni 1.4. Tumepata maji katika Kijiji cha Buyezi wenyewe thamani ya milioni 230. Isitoshe tumepata pesa kutokana na pesa za UVIKO, milioni 500 ambazo zimekwenda kutekeleza maji katika Kijiji cha Mshwagule. Tumepata pia milioni 500 ambazo zimetekelawa mradi wa maji katika Kijiji cha Samvura, Kata ya Mnyambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo bado nina vijiji 11 mbavyo havina maji. Hivi ni vijiji vya Kumkuyu, Rubunga, Kukinama, Magarama, Kigina, Nyaruranga pamoja na Kasana. Nimepitia bajeti hii tunayokwenda kuipitisha sasa na mimi nitakwenda kuipitisha kwa kiwango cha hali ya juu, nitaiunga mkono kwa sababu, nimeona nimetengewa maji katika vijiji vitatu, Mikonko, Magarama na Lukaya ambayo itagharimu takribani bilioni 1.7. Naishukuru sana Serikali kwa kuendelea kulijali Jimbo la Muhamwe. Naishukuru sana Serikali kwa kuendelea kumtua mama ndoo kichwani kwa vitendo katika Jimbo hili la Muhamwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niishauri Serikali. Miradi hii ya vijiji scope yake imekuwa ndogo; kwa maana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwamba tunapata yale maji na tunapata yale magati, lakini watumiaji wale wa magati wanakuwa wengi na bado hatujawa na mtandao katika vijiji vyote. Hii inasababisha miradi hii kuharibika kwa haraka hasa uchakavu wa mabomba. Sasa, niiombe Serikali katika miradi hii ya vijijini tujitahidi kusambaza maji vijijini ili tufikie lengo la mwanamke asitembee zaidi ya mita 200 kufuata maji, ili kupunguza uharibifu wa haya mabomba, lakini pia kupunguza mwendo mrefu wa mama kwenda kwenye kituo cha kuchotea maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kutuletea wataalam katika hivi vituo. Wote ni mashahidi, changamoto ya maji vijijini ni kuwa na jumuiya za watumia maji hazina wataalam. Kwa hiyo, kwa kitendo hiki cha kutuletea wataalam kwenye jumuiya za watumia maji inatupa uhakika kwamba maji yapatikana. Kwa mfano kule kwangu Kumuhasha tunakaribu miezi sita hatupati maji kwa sababu tu hatuna mtaalamu mahali pale. Kule Malolegwaa hatupati maji kwa sababu hatuna mtaalamu. Kwa hiyo, kwa kuja na suluhisho la kuwa na wataalamu kwa jumuiya za watumia maji tutakuwa na uhakika wa kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunayo Mamlaka ya Maji Mjini; niendelee kuishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imetusaidia. Ni mwaka mmoja sasa tulikuwa na asilimia 27 ya huduma za maji. Unaweza ukaona jinsi gani ilikuwa ni changamoto maji Kibondo Mjini nahii ilikuwa ndio fimbo ya kumchapia Mbunge, hatuna maji. Nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imetusaidia, imetupatia milioni 595 tumejenga chujio pale mto wa Mgoboka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, imetupatia tena milioni 590 ambazo tumekwenda kununua *pump* na mabomba kwa ajili ya kuongeza mtandao wa maji Kibondo Mjini. Tunakwenda kuongeza mtandao wa maji kwa kilometra 11.9 ambazo zitatupa faida kwa watumiaji 550. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu, tulukuwa na deni kubwa sana la umeme kwenye vyanzo vya maji, milioni 283. Serikali imetusaidia imetulipia deni na sasa tumbaki na milioni 104 ambazo tunaamini Serikali hii ni sikivu, Serikali yetu ya mama yetu Samia Suluhu Hassan, itakwenda kutusaidia kumalizia hizo milioni 104. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeshapata yote. Tumepata chujio, tumepata mabomba, tumepata na *pump* za ku-*pump*, maji haya tutayapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali itusaidie. Ombi letu tunaomba tupate *tank* la kuhifadhiaya maji ili tuweze kuyasambaza. Tumeshaleta maombi, tunaomba *tank* la lita milioni 100.5 ambalo litagharimu bilioni 1.1. Ombi langu, naomba mtusaidie ili tuweze kutoka kwenye asilimia hizo tulizokuanzano, maana baada ya kutusaidia tumetoka 27 tuko 56 na tunalenga na sisi tufike huko 74 ambazo sinasemwa kwamba, ni za kitaifa. Sasa ili na sisi tufike kule tunaomba na sisi tupate *tank* la maji la thamani hiyo ya bilioni 1.1 ili tuweze kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waswahili wanasesma kushukuru sana ni kuomba tena. Niendelee kuiomba Serikali itusaidie wataalamu; mamlaka zetu hazina wataalam, hatuna *technical staff* pamoja na wahasibu. Ma-*engineer* hawa, *Engineer* Aidan na Almas wanakimbia sana. Mkiwaongezea hawa wataalamu basi kazi itafanyika vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe Serikali itusaidie miradi hii imetekelezwa kwenye maeneo ya watu ambao wanahitaji fidia. Katika Kituo kile cha Kumwai mradi huu umetekelezwa kwenye eneo la watu ambao wanadai fidia, milioni nane. Serikali haishindwi naomba mtusaidie. Familia hizi za akina Hamisi Omari na wenzake kila nikifika jimboni, mama tusaidie; na mimi nakuja leo kuiomba Serikali, naomba tuwalipe fidia wananchi hawa wa Kumwai ambao miradi hii ilitekelezwa kwenye maeneo yao. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe vitendeakazi. Jamani Jimbo la Muhamwe ni jimbo lilitoko pembeni, tunaomba magari tupate japo gari moja liweze kutusaidia tuweze kutembelea hivi vijiji ili utendaji kazi wa ma-engineer hawa uweze kuboreka zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelea bajeti kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa. Na mimi nichukue nafasi hii kuiomba, tuna ahadi ya Mheshimiwa Rais, hayati Magufuli, ya kujengewa bwawa katika Kata ya Busunzu. Naona sasa ni muda muafaka madam tumetenga bajeti basi na mimi naomba...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi kwa mchango wako.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Abubakari Asenga.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda na mimi kuchangia; na ninaanza kwa kuunga mkono hoja kwa sababu mimi nimesimama hapa sina nongwa kubwa na Waziri wetu wa Maji, Naibu wake na Katibu Mkuu. Naibu Waziri alikuja jimboni kwangu akapanda kwenye milima juu kabisa kwenye vyanzo vya maji, ametusaidia sana, Mungu awabariki sana mnafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa mara ya kwanza tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa kutusaidia Mradi wa Miji 28, mradi wa Kiburubutu ambao tangu Mbunge akiwa marehemu Abbas Gulamali ulikuwa haujafanyiwa kazi na haujapatiwa pesa, safari hii umepatiwa pesa kwa hiyo,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunawashukuru sana na tunawapongeza. Naomba tu mtusaidie katika vile visima ambavyo tumechimba sasahivi mpango wa pili ni ma-*tank* tupate fedha kwa ajili ya ma-*tank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muda wangu huu ambao nimepewa wa kuchangia sauti yangu inaongea kwa unyonge sana kutokana na masikitiko ya wananchi wangu ambao tunabioreshea maji; wengi ni wakulima wa mpunga na miwa.

Juzi tarehe 5 mwezi wa tano walikaa katika vyama vyao wakaamua kuhusu maslahi yao ya miwa katika mikutano yao mikuu, lakini jana nimepokea simu zaidi ya hamsini wakiwa wanasiitika kuhusu maamuzi yaliyofanywa na Serikali kuingilia maamuzi yao; kwa kweli imenisikitisha sana. Natumia nafasi hii kusema ili Serikali iliyopo hapa isikie isaidie kufuatilia. Kama tunaboresha maji huku tunaendelea kuharibu na kuingilia shughuli za wananchi za uzalishaji itakuwa hatufanyi kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia muda wangu huu ili Mawaziri na viongozi waliokuwepo hapa wasikie. Kwenye biashara, kwenye kilimo cha muwa kuna shida kubwa sana. Naligusia hapa kwa sababu hakuna maana nydingine yoyote kama tunaboresha mambo ya maji kwa wananchi halafu wakulima kule wananyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna kiongozi wa Serikali ameenda kuzungumza na wananchi, hawajafurahia maamuzi yao Kata ya Sanji. Na kwa bahati nzuri nimeongea na Mheshimiwa RC, Mkuu wa Mkoa Shigela, analifanya kazi hili. Nimeongea na Waziri Bashe analifuatilia. Jambo hili halijakaa vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa naomba kutumia nafasi hii wananchi wangu wasikie kwamba, nimelisema hapa na tunalifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume zimeshaundwa kufuatilia jambo hili, lakini halfanyiwi kazi na tume zinachifwa taarifa, yanazushwa maneno ya uwongo kujenga faida ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watu kunufaika na kilimo cha muwa na sukari. Mambo haya ni kama yale yaliyotokea Kasalali, mambo haya ni kama yanayotokea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimetumia muda huu wa kuchangia Wizara ya Maji kushukuru kwa miradi waliyotuletea, lakini kwa kweli ni masikitiko makubwa sana na kilichotokea jana; kwa mara ya kwanza kupokea mimi simu karibu hamsini za wananchi wakilalamika wanataka kupanda mabasi kuja Dodoma kwa sababu maamuzi yao yamekiukwa. Ni imani yangu ni kwamba, kuwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa watachukua hatua madhubuti za kuwasikiliza wananchi wale upya; kwa sababu Sheria za Ushirika wamefuata na taratibu wamefuata, lakini zemeenda zimetenguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishia hapa. Nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Ni Taarifa au ni nini?

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kumpa Taarifa, naona ameshakaa.

MWENYEKITI: Alishamaliza kuzungumza Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana.

Nilikuita Mheshimiwa Deus Sangu.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu na mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu sana, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini *culture* waliyonayo, kwa maana *hierarchy* Wizara yao yote ni wasikivu, Katibu Mkuu, Meneja wangu wa Mkoa ndugu yangu Boaz, unafanya kazi nzuri na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Meneja wa *SUWASA* ndugu yangu Nzoa na Meneja wangu wa Wilaya, Maganga. Kwa kweli kazi yao ni nzuri, wanatupa ushirikiano mzuri kiasi kwamba, tunafurahia sana huduma katika Wizara yako hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanza kwa shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza kwa *mile stone* tuliyopiga kwenye miradi ya maji. Kwa muda mfupi nimeingia kama Mbunge nimeweza kushuhudia maajabu. Ajabu ya kwanza ambalo nitalisema kwako na kwa moyo mkunjufu ni mradi ule wa Ziwa Dogo la Kwela ambako sasahivi mko kwenye *final stage* ya kusaini mkataba wa bilioni tano. Utahudumia Kata za Kalambanzite, Lusaka, Laela, Nyangalua na Mnokola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tumepata fedha hizi billioni tano ni za mwanzo tu, lakini umuhimu wa mradi huu *uta-justify* na *investment* hii kwa sababu *return* ya hii *investment* ni pale tutakopofikisha maji haya katika Mji Mdogo wa Laela, Mnokola na Miandalua. Sasabu hii ya kusema ni nini, tuna chanzo kile kimeishiwa nguvu, ambacho Serikali iliwekeza bilioni 2.6 pale kwenye Mji Mdogo wa Laela umefika mara nyingi na badaye kukatokea mgogoro mkubwa umechukua miaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale kuna shida nyingine. Ule mradi mwanzo ulikuwa unatumia *system* ya *solar*: mliwekeza kama shilingi milioni mia moja na kidogo kwa ajili ya kununua *solar*. *Solar* ziko pale ziko *redundant* na mara nyingine sisi tunapata shida kupata maji kwenye Mji Mdogo wa Laela kwa sababu moja tu kwamba, umeme tunaotegemea ni wa Zambia. Wakati mwengine inapita hadi wiki mbili hatujapata umeme kwa hiyo, tunakuwa hatuwezi kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikuombe kwa kauli yao Mheshimiwa Waziri turudi, zile *solarzinakaa* pale zitakuwa *obsolete*. Tuzitumie ili zitusaidie ili zitusaidie pale tunapopata shida ya umeme zisaidie ku-*pump* maji ili wananchi wa Mji Mdogo wa Laela waweze kupata maji. Lakini chanzo cha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwela ndio kitaenda kumaliza matatizo ya kudumu kabisa kwa sababu ukifika mwezi wa saba na wa nane maji yanakuwa ndoo moja shingi elfu moja mpaka elfu mbili katika Mji Mdogo wa Laela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili nishukuru sana Serikali kwa mradi mkubwa wa kihistoria utakaoteklezwa ambao unaitwa *Kaoze Group* kule Bonde la Ziwa Rukwa. Mradi ule utaleta manufaa makubwa. Nashukuru mmetangaza kuanza na Kata ya Kaoze kwa bilioni moja na milioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimuombe Waziri, kwa mradi ule wa mamu, ule wa Marekani, ambao umekuja, muweze kupeleka mpaka vijiji vingine 13, kwa maana ya Kata za Kipeta na Kilangawani, ili wananchi wale ambao tangu ulimwengu huu kuumbwa hawajawahi kupata maji safi na salama na hawajawahi kuona maji kutoka kwenye bomba. Nikuombe ndugu yangu Waziri umekuwa ukini pa ushirikiano mzuri na Naibu wako, twendeni tukafanye jambo kubwa kwenye mradi huu wa *Kaoze Group* ili wale wananchi waweze kuandika historia kwamba, alipita Mheshimiwa Aweso, kama Waziri, alitufanya miujiza mikubwa ambayo hawajawahi huona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kuna ule mradi wa Bwawa la Ikozi, unalifahamu sana una miana zaidi ya minne bilioni 1.5 tumewekeza pale. Shida iliyopo pale kuna mambo mawili; kwanza kuna mgogoro ule na wale wananchi waliotoa yale mashamba. Nikuombe Waziri kuna mambo waeleweshwe tu wale wananchi, miaka minne hawajaeleweshwa kama kuna fidia au hakuna. Ni kuwaweka tu wapate *clarity* ya mradi ule utakavyokuwa, wakashajua hawana shida, maana wameshindwa kupata jibu kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twendeni tukawaambie ili pesa ulizoleta hizi karibuni tumesaini mkataba wa bilioni mbili wakaone faida ya hela ya mama bilioni mbili, sio ikatokea bilioni mbili imewekezwa pale muda mfupi tuanze kupata *sabotage* ya wananchi kwa sababu wana *complain*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwamba kuna mgogoro kwenye eneo lile la Ikoze. Najua ni jambo dogo kwako utaenda kuli-*address* ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nishukuru pia kwa mradi mkubwa sana ambao unaenda kuhudumia *Mkunda Group*, Kijiji cha Kaengesa, Kianda pamoja na Kijiji cha Itela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe jambo moja. Kuna vijiji viwili katika mradi huu vimesahaulika na viko njiani; Kijiji cha Katonto na Kijiji cha Kazi. Naomba tunapofanya huu mradi ambao tayari nao umesaini mkataba viwe *included* ili waweze kao kunufaika nah ii pesa bilioni moja na milioni 700 ambayo mama amewaleta wananchi wa Kata ya Lyangalile na wa Kata ya Kaengesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa namna kubwa kabisa na Wabunge wenzangu wa Kigoma, Katavi, Rukwa na Songwe wameongea. Mradi ambao utakuwa tiba ya kudumu ya tatizo la maji katika mikoa hii minne ni mradi kutoka Ziwa Tanganyika. Tuombe sana; *investment* ni kubwa tunakubali, lakini *return* ya *investment* hiyo na *economies* ya *scale* ambayo itapatikana kulingana na huu mradi itaenda kumaliza tatizo hili na hii miradi midogo ambayo *life span* yake ni miaka 20 tutaachananayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana pia kwa *CSR* uliyotoa pale kizungu ndani ya Kata yangu Muze, nakushukuru. Umekuwa kati ya Mawaziri waaminifu; ukipita ukaahidi jambo unatenda, maana kuna jamaa zangu walipita jimboni kwangu wakaahidi *CSR* miaka mitano, wengine mpaka wameondoka kwenye uwaziri nimesahau kabisa, ila wewe uliahidi ndani ya mwezi mmoja na muda mfupi ukaleta ile *CSR*. Nikupongeze ndugu yangu Mheshimiwa Aweso kazi yako imetukuka hakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho nishukuru pia kwa mradi ule unaoendelea wa Uviko pale Mwadui, Kata ya Mwadui, lakini pesa tuliyotenga kwa ajili ya Kata ya Kasekela. Halikadhalika llemba pale kwa mara ya kwanza nao

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watapata maji ya kutosheleza. Nikupongeze sana Waziri, kwa kweli mimi hayo niliyoyasema ndio nakuomba sana, *Lake Tanganyika* ndicho kilio chetu, ndio suluhu ya matatizo katika mikoa yetu hiyo minne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshasimama, Mwongozo gani tena?

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha saa 03:00 asubuhi mpaka saa 07:00 mchana tunawashukuru sana wachangiaji kwa hoja mbalimbali. Mambo mbalimbali yamezungumzwa, mojawapo likiwa ni kutazama namna gani mlundikano wa kazi zinavyokuwa makao makuu zinavyokwamisha shughuli kule kwenye *level* za mikoa na wilaya.

Hapa nina matangazo machache kutoka kwa Katibu wa Bunge; tangazo la kwanza anasema, Tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge, mnajulishwa kwamba, Mheshimiwa Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, anawakaribisha kushiriki katika ghafla ya Usiku wa *Royal Tour* takayofanyika tarehe 15 Mei, 2022 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete kuanzia Saa 12:00 jioni. Mgeni rasmi katika ghafla hiyo atakuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge mnasisitizwa kuhudhuria ghafla hiyo muhimu sana. Tarehe 15 Mei, kuanzia saa 12:00 jioni, usiku wa *Royal Tour* hapa Dodoma. (*Makofi*)

Aidha kuna wageni walioko hapa Bungeni mchana huu; wageni watatu wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi (Mb) na Naibu Waziri wa Maji kutoka Mkoani Mbeya ambao ni mtoto wake Morin Sala, mdogo wake Luhama Hezekiah

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Katibu wake Ndugu Beatrice Chisuba, Katibu wa Mheshimiwa Mbunge. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 93 wa Mheshimiwa Pauline Gekul (Mb), ambaye ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambao ni Jumuiya ya Shule ya Sekondari Nakwa kutoka Babati, Mkoani Manyara, wakiongozwa na Mkuu wa Shule ndugu Elias Iyo, ahsanteni sana, karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Wageni 114 wa Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea (Mb), ambao ni wanafunzi wa Chuo Cha Mipango, wakiongozwa na ndugu Denis Buchadi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wachangiaji, mjadala utaendelea mchana na watakaoanza kuchangia atakuwa ni Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Emmanuel Shangai na Mheshimiwa Edward Ole-Keita Kisau.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana, Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tukae, Katibu.

NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa
Mwaka wa Fedha 2022/2023**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Kuna Wabunge hapa ambao walikuwa wamesalia kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Amsabi

atafatiwa na Mheshimiwa Salma Kikwete, Mheshimiwa Stella Simon Fyao ajiandae. Mheshimiwa Amsabi Mrimi.

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii nzuri ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. Awali ya yote nimshukuru sana Rais kwa namna ya pekee kabisa kwa jinsi ambavyo anapambana kuhakikisha Watanzania wanapata maji. Hii inatokana na *a very strong political/will* aliyonayo pamoja na ubunifu mkubwa alionao katika kutafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, pia pale Serengeti tuna watu wa *RUWASA* wanafanya kazi nzuri sana wakiongozwa na Eng. Mchele. Wameendelea kupambana kila wakati kuhakikisha mambo yanaenda vizuri. Tunao watu wa *MUGUWASA*, taasisi inayosimamia utoaji wa maji katika mji wa Mugumu, pia wanafanya vizuri sana, na hivi karibuni kulikuwa na shida kubwa ya maji kuchafuka kutohana na tope la mvua nyngi kunyesha bado walifanya vizuri wakasafisha matenki, kwa hiyo wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kubwa kwa taasisi hizi mbili ni kwamba taasisi hizi ziongezewe vifaa vyta kutendea kazi. Watu wa *RUWASA* hawana gari za kutosha, wanayo gari moja na imechoka ilhalii wana miradi mingi ya kuisimamia. Kwa hiyo niombe sana Wizara, nimeona kwenye bajeti hamjawawekea fedha kwa ajili ya gari, niombe muwafikirie kuwaongezea gari. Lakini pia wanao watumishi wachache. Kwa mfano *RUWASA* wanaye engineer mmoja tu, *engineer* Mchele ambaye yeche huyo huyo ndiye Mkuu wa *RUWASA* katika wilaya nzima. Kwa hiyo *mostly* anafanya kazi za *administration*. Kwa hiyo tuongezee watumishi ili wawzeze kusimamia miradi hii vizuri kwa sababu *component* ya usimamizi ni ya muhimu sana ili tuweze kuwa na miradi mizuri na inayokamilika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakin pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wizara hii ya Maji. Wizara hii mnafanya vizuri sana, tumeona mkisimamia na kutekeleza majukumu yenu kwa umahiri mkubwa. Hii imechangia Wizara hii kuwa

na mafanikio makubwa sana. Kipekee sana nimshukuru Rais wetu kwa kutupatia kijana makini mahiri kabisa, rafiki yetu Aweso, anafanyakazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Baraza kuwa limetangazwa Waziri wa kwanza kukutana naye nilikutana na Aweso. Aweso ni mtu mahiri, ni msomi mzuri lakini ni mtu yuko tayari wakati wowote kupokea mawazo ya na maoni ya watu. Ni mtu unayeweza pia ukamkosoa, hana tatizo anasikiliza na anapokea mambo. Kwa hiyo nilizungumza naye na kukosoa jinsi utekelezaji wa mradi wa chujio pale Mugumu ulivyokuwa ukiendelea; na Awezo aliniambia hebu usiwe na wasiwasi hii umetoboa. Kweli baada ya muda mfupi miliona utekelezaji mkubwa fedha imepatikana na mradi ule ukakamilika; kwa hiyo tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo moja ambalo katika bajeti iliyopita, hii tunayoenda kukamilisha, ya mwaka 2021/2022; niombe sana Wizara, tuliomba kiasi cha milioni 800 hii ilikuwa kwa ajili ya kuhakikisha mradi huu sasa unapanuka kiasi cha kutosha. Kwa kufanya hivi ingetuwezesha kuondoa utegemezi ambao upo. Kumekuwa na utegemezi sana katika kuendesha ule mradi na kila mara tunawapigia simu umeme unakatwa kwa sababu mradi ule hauwezi kulipa gharama za umeme na zingine na zingine, sasa imekuwa ni shida. Pamoja na kazi hii nzuri ambayo Serikali imefanya ya kutupatia fedha na mradi ule wa chujio kukamilika na *expansion* ile ambayo Mheshimiwa Aweso ulipokuja mwisho wa mwaka wa jana ukatuongeza milioni 527; *expansion* ya mradi ule umefanyika kuelekea katika tenki ni nzuri lakini maji mara kwa mara yanakatwa. Sisi tuliamini kwamba kwa kupata hii milioni 800 tutapanua wigo wa mradi ule ili watu wengi wapate maji ili katika *multiplier effect* tunaweza tukapata fedha nyngi za kuendelea kuendesha ule mradi sisi wenywewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuombe sana katika muda huu uliobaki mtusaidie fedha hizi ili tuweze kukamilisha mradi ule na tuweze kusimama imara na kuendesha huu mradi vizuri. Hii itaondoa manung'uniko ya wananchi

ambayo yanakuwepo mara kwa mara hasa huduma ya maji inapokatwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni vizuri ikakumbukwa kuwa mradi huu pamoja na kwamba kuna mradi ule wa miji 24, 28 bado ni muhimu kuendelea kupanua mradi huu, ambapo tayari tutakuwa tumeanza kufanya kazi ya sehemu ya mradi ule mkubwa unaokuja. Kwa hiyo tunaomba hili tuweze kutekelezewa.

Mheshimiwa Spika, lakini tunashukuru sana, kuna miradi mingine ambayo imeweza kukamilika katika baadhi ya vijiji kule Robanda kuna miradi mingine Makundusi kule Kebancha na vijiji vingine vingi. Tunaona kuna miradi inaendelea katika vijiji 56. Kwa kweli ni *commitment* kubwa na fedha hii imetolewa lakini bado pamoja na miradi hii mingi inayoendelea bado kuna zaidi ya vijiji 24 ambavyo bado havina maji kabisa. Kuna vijiji vya Masinki, Magange kuna vijiji vya Nyamihuru kuna ukienda vijiji vya kule Bisalala kuna vijiji vya Robanda ambapo tayari tumepata kisima kimoja lakini bado sehemu ni kubwa sana ambayo inahitaji maji.

Mheshimiwa Spika, bado ukienda Bwitengi na vijiji vingine vingi kama vile Kebosongo vingi sana havina maji. Sasa katika ile 85% ambayo Wizara imekusudia kufikia *by 2025* naona Serengeti tunaweza tuka-lag *behind*, kwa hiyo tuwaombe sana Wizara tuone kila linalowezekana katika bajeti, hii kuona kwamba mmetutengea bilioni nne *point something* bado kungehitajika fedha nydingi zaidi ya kuongeza maana naona pale kuna vijiji kama vitano ambavyo vimewekewa fedha ambavyo ni Viji vya ijiji Ligicha, Nyiberekera Singisi pamoja na Nyamisingisi ambavyo viko jirani ambavyo mngeweza mkavi-connect na hiyo *project* havina maji bado.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niombe katika bajeti hii mpya 2022/2023 kuna mradi ule wa miji 28. Pale Serengeti tunahitaji mradi ule uweze kuwa mkubwa zaidi. Lile bwawa la Manchila wakati linajengwa lilikuwa kwa ajili ya kutafuta *temporary solution* ya maji katika mji wa Mugumu ambao ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Makao Makuu ya wilaya. Wakati ule Mugumu ilikuwa ni kijiji ilikuwa na watu wachache sasa watu ni wengi na ule mji bado unaendelea kuwa mkubwa; na hivi karibuni tunaendelea na maandalizi tukishirikiana na Serikali ya wilaya kwenda kwenye *project* kubwa sana ya *Smart City*.

Mheshimiwa Spika, *project* hii inaenda kujenga itahusisha ujenzi wa mahoteli makubwa kwa ajili ya huduma za kitalii tunaenda kujenga miundombinu mikubwa *facilities* nydingi sana ambazo zinahitaji maji. Maji katika lile bwawa ni lina *cover* kama ni *almost* mita *cubic* milioni 14.2 na wataalamu wanaonesha miaka 15 hadi 20 ijayo litashuka mpaka kufikia mita *cubic* 6,000,000 sasa hii na mategemeo yetu kwa miaka 10, 20 ijayo tunaweza tukawa tunahitaji zaidi ya mita *cubic* milioni 30.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna haja sasa huu mradi mkubwa badala ya kutumia bwawa la Manchila sasa mwende kuu-*connect* na ule mradi mkubwa unaotoka Mugango – Kyabakari – Butiama. Kutoka Butiama mpaka Mji wa Mugumu ni kilomita 90 tu. Tukifanya hivi tutapata maji ya kutosha na maji kwa muda mrefu. Ni vizuri tukafikiria kuwa na *solution* kuwa na matatizo ya muda mrefu kuliko kila siku ku-*invest* katika *mean solution* za muda mfupi, baada ya kusema haya naunga mkono hoja ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafatiwa na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara ya Maji.

Awali ya yote naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Maji kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Wizara kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. Sambamba na hilo nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwatua wanawake

ndoo kichwani. Ama kweli hakuna mwanamke anayeweza kutupa mtoto wake, na mama ametambua tatizo la maji ni tatizo la wanawake. Tuna mpongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nilisimama kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwaajili ya kuomba maji na Mheshimiwa Waziri akanihakikishia na akaniambia; ukiona mama mtu mzima analia ujue kuna jambo; nitahakikisha hili jambo linamalizika au kupungua kwa kiasi kikubwa; na ndiyo maana leo nimesimama kwa ajili ya shukran. Mheshimiwa Waziri amenipatia pesa takriban bilioni 12.5 kwa ajili ya mradi mkubwa kutoka chanzo cha Ng'apa kuja Mitwero hatimaye kusambaza mabomba katika Jimbo letu la Mchinga, ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa fedha hizo ambazo umenipatia. Sasa ninaamini lile tatizo la maji limeanza kupungua na baada ya muda si mrefu tatizo la maji litatoweka katika Jimbo letu la Mchinga ambalo liko katika Manispaa ya Lindi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kuna Tarafa ya Mipingo tayari maji sasa hivi yanatiririka. Mheshimiwa Waziri wanakusubiri tu uje uzindue kama ambavyo ulivyoahidi wakati ule tulipokuwa pale Mnyangara ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Haukuishia hapo tatizo la maji la Mchinga lilikuwa ni tatizo tete na ni tatizo kubwa; maji kulikuwa hakuna walikuwa hawajui maji ya bomba sasa hivi maji yanatiririka bombani.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo uknipatia visima vinne na tayari hivyo visima vinne vimeshakuwa katika harakati za kumalizika kuna kisima cha Kilolambwani tayari kimemalizika, Uleka kule kisima kimemalizika na maji yanabubujika hayana hata utaratibu jinsi yanavyobubujika ahsante sana. Sasa tuko kwenye kisima kile cha tatu Namkongo ambako Namkongo kulikuwa na shida kubwa ya maji; wakitoka Namkongo wanamalizia Nanjime. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia maji katika Jimbo langu la Mchinga.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna bilioni 1.5, na hii umetupelekea Mnyangara na tayari kazi inafanyika;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

umetupelekea Mputwa tayari kazi inafanyika; vile vile umetupelekea Kiwawa kazi zinafanyika, na ndio maana nimesema nasimama hapa kwa ajili ya kutoa shukrani zangu za dhati kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imefanyika. Mwaka 2022/2023 bado kuna miradi mipyä ambayo mmetupatia.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mpyä wa upanuzi kutoka Kilangala kwenda Mihamwe Sinde hatimaye kufika kule Mtumbikile. Mradi huu una jumla ya shilingi milioni 340. Sambamba na hiyo kuna mradi ambao utakuwa ni *Phase II* kutoka Moka kwenda Matimba; na maeneo haya yote yalikuwa na matatizo makubwa ya maji huku umetupatia milioni 250 jumla ya milioni 590. Hukutuacha hapo hivyo hivyo bado ukatupatia visima vitano ambavyo vitachimbwa katika Jimbo letu la Mchinga. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kila kwenye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto. Sambamba na mafanikio hayo makubwa ambayo tumeyapata kwa muda mfupi katika Jimbo letu la Mchinga bado tuna changamoto katika tarafa ya Milola kuhusiana na suala la ukarabati na mabomba ambayo ni chakavu katika ile kata ya Milola. Maji yapo lakini yanayomwagika ni mengi sana. Tunachoomba Mheshimiwa Waziri utusaidie kiasi cha fedha ili tuweze kufanya ukarabati wa mabomba yale ambayo yanavujisha maji kutoka kwenye chanzo hadi kwenye bomba kuu pale Nyirola.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwagine ambao nashauri huu mradi ambao ni wa bilioni 12.5 pesa ambazo tayari zimetoka ni bilioni 1.8 na ni mradi wa mwaka mmoja. Ombi langu kwa Serikali ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri mtufanyie kadri inavyowezekana kadri bajeti inavyoruhusu ili kutupatia zile pesa kwa wakati ili ifikapo tarehe 3 Mei, 2023 kama tulivyokubaliana mradi huu uwe umekamilika. Tulikubaliana kwenda kusaini ule mkataba na ulikuwa tayari. Mheshimiwa Waziri vile vile nitakuomba twende tukazindue ule mradi wakati huo huo kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. ninaipongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

unaifanya. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia na kwa kuwatua ndoo wanawake wa Jimbo la Mchingga. Mwenyezi Mungu akubariki Mwenyezi Mungu awabariki. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kabla hujakaa tusaidie Jimbo la Mchingga liko Mkoa gani hapa nchini? Washa kisemeo chako

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mchingga lipo Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Lindi ndiyo mkoa ambao Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatokea huko katika Jimbo la Ruangwa. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni muhimu sana kufahamu kwamba haya mambo yanayozungumzwa miradi mikubwa inayozungumzwa kwenye Jimbo la Mchingga liko Mkoa mmojawapo kati ya mikoa ya kusini na ndiko ambako jana hapa Mbunge alichangia kana kwamba kusini kuna jambo fulani hivi. Lakini mmesikia hapa Jimbo moja tu bilioni 590 zimepelekwa, Jimbo moja. Kwa hiyo sasa nadhani mnaanza sasa kupata picha.

Haya ahsante sana Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kwa mchango huo muhimu kutoka kwenye mkoa anaotoka Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Stella Simon Fiya atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Emmanuel Lekshon Shangai ajiandae.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Nitaanza kwanza kwa kuugusa Mkoa wa Songwe kwa sababu Mkoa wa Songwe tuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama. Mkoa wetu una kata zaidi ya 90 lakini hakuna kata yenye uhakika wa kupata maji safi na salama. Changamoto hii imepelekeea

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

baadhi ya maeneo kujikuta wana-share maji pamoja na mifugo; hasa ukienda katika Wilaya za Ileje, Mombasa na maeneo mengine changamoto kubwa ya maji wananchi wamejikuta wana-share maji pamoja na mifugo jambo ambalo ni hatari sana kwa afya za wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nitazungumzia sana changamoto kubwa pia iliyopo katika Jimbo la Tunduma iliyopatikana muda mrefu. Changamoto ya maji imekuwa ni kubwa sana ndani ya Jimbo la Tunduma na changamoto hii imepelekeea wananchi watumie muda mwingu sana kwenda kuyatafuta maji, badala ya kufanya masuala mengine yanayohusiana na maendeleo ya Taifa letu. Lakini pia ndani ya mji wa Tunduma kuna mradi mkubwa wa maji ambao ulikuwa umeshafanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 2013 na Kampuni ya *Networkers* ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, upembuzi huu ulifanyika kutoka Mto Songwe Ileje na kuja kuyaleta maji katika Jimbo la Tunduma, jambo ambalo mpaka leo halijatekelezeka na bado wananchi wa Tunduma wana kilio kikubwa cha changamoto ya maji.

Mheshimiwa Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja hapo atuambie ni lini mradi huu utaanza kutekelezeka ili wananchi wa Mji wa Tunduma waepukane na changamoto ambayo wamekuwa wakiipata kwa muda mrefu zaidi?

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mradi mwengine wa maji kutoka katika Wilaya ya Mbozi. Mradi huu unatoka katika Kijiji cha Ukwile na ulikuwa ukiwahudumia wananchi wa Kata ya Mpemba na Kata ya Katete. Mradi huu kutoptera na ubovu na uchakavu wa ile miundombinu, kwasababu miundombinu iliyopo kwenye ule mradi ni ya mwaka 1971, hivyo miundombinu hiyo imechakaa sana, na kupelekeea wananchi kushindwa kupata maji. Lakini nitaomba pia Waziri atakapokuwa anakuja atuambie ni lini watafanya mabadiliko wa ile miundombinu ili wananchi wa Kata ya Mpemba na wananchi wa Kata ya Katete waweze kuwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uhakika wa kupata maji safi na salama kutoka katika mto Ukwile. hii inaweza ikatusaidia sana kutokana na changamoto kubwa ambayo inawakuta wananchi wa mji wa Tunduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Lakini changamoto nyingine kubwa ni kwa wananchi kusomewa *bills* zisizo sahihi. Hiki ni kilio cha maeneo mengi sana ndani ya Mji wa Tunduma na ndani ya Mkoa wa Songwe kwa ujumla. Changamoto hii imekuwa ikiwakabili wananchi wanapewa *bills* kubwa ambazo ni tofauti na uhalisia wa maji ambayo wanakuwa wameyatumia kwa wakati huo; jambo ambalo limekuwa likiwaumiza sana wananchi wetu,

Mheshimiwa Spika, ningeomba kuishauri Wizara. Wana sababu ya kuhakikisha kila mwananchi wanae mhudumia kwenye suala zima la maji wafunge mita ili wawewe kupata uhalisia wa gharama ambazo wanakuwa wanawatoza wananchi wetu. Kwasababu hatimaye wananchi wetu wamebakia wakiumia, wanatoa kodi kubwa tofauti kabisa na ule uhalisia wa matumizi yao yam aji. Tunaomba hili lizingatiwe kwasababu linawaumiza sana wananchi wetu (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala zima la upotevu wa maji. Katika ripoti ya CAG ya Machi, 2022 inaonesha kabisa kwamba kuna tatizo kubwa ambalo linaikabili Wizara la upotevu wa maji; changamoto ambayo imesababisha Wizara kupata hasara kubwa. Ukisoma katika ripoti ya CAG inaonesha kwamba kwa mwaka 2020/2021 upotevu wa maji uliigharimu mamlaka kiasi cha Shilingi bilioni 175. Hii ni gharama kubwa sana ambayo pengine ingeweza kutusaidi hata kuendeleza miradi katika maeneo mengine ambako haiwezekani kabisa, kumekwama kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Iakini leo hii nazungumzia mradi wa kutoka lleje kwenda Tunduma pengine kusingekuwa na hizi changamoto fedha hizi zingeweza kutusaidia hata sisi wananchi wa mji wa Tunduma kuweza kutatua changamoto ya maji. Kwasababu ukirudi kule Tunduma huu mradi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ninaouzungumzia unagharimu kiasi cha Shilingi bilioni tatu tu. Sasa kama tunaweza kupoteza fedha Shilingi bilioni 175 Shilingi bilioni tatu inawezaje kutushinda. Hili tunaomba Wizara pia ilizingatie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini changamoto kubwa ninayoiona, Wizara ina sababu ya kuongeza watumishi katika eneo la maji ili waweze kufanya ufuatiliaji kwenye maeneo ambayo wanawahudumia wateja. Kwasababu sababu wanazozitoa hapa zilizosababisha kupata hasara hii kubwa ni kama vile wateja kujunganishia maji kinyume na utaratibu. Jambo hilo limepelekea Wizara kupata hasara kubwa sana. Jambo la pili ambalo wanalisema ni kuvuja kwa mabomba.

Mheshimiwa Spika, sasa, Wizara ikipata watumishi wengi katika maeneo ambayo wanawahudumia wateja hizi changamoto zinaweza kupungua na hatimaye hatuwezi kuwa na idadi kubwa ya upotevu wa maji kiasi ambacho tunapata hasara kubwa. Tuombe hili lizingatiwe. Wizara ione umuhimu wa kuongeza watumishi katika sekta ya maji ili waweze kufanya ziara na kutembelea yale maeneo ambayo wanatoa huduma kwa wateja...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Haya, ahsante sana kengele imeshagonga, ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah anatufatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau ajiandae. (*Makof*)

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya maji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu kwa namna ambavyo wanachapa kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza llani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuhakikisha kwamba huduma ya maji

inawafikia Watanzania. Tunawapongeza sana na Mungu aendeleee kuwabariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri kwa kuwasilisha bajeti yake ya utekelezaji ya mwaka 2022/2023, bajeti ambayo inakwenda kupunguza changamoto kubwa ya maji katika nchi yetu ya Tanzania na kuhakikisha kwamba maji salama yanaendelea kupatikana.

Mheshimiwa Spika, nimebahatika kupita katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania katika shughuli za Kamati ya P/C. Nimekwenda katika Majiji ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam na kuangalia miundombinu ya maji na shughuli mbalimbali za usambazaji wa maji na huduma za maji kwa wananchi; maji safi pamoja na maji taka; tumeona shughuli kubwa ambayo Serikali inafanya na tunawapongeza sana katika Mkoa wa Dar es Salaam, Arusha na Mwanza kwa namna ambavyo wanasimamia utekelezaji katika kuwashudumia wananchi kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ningependa kule kwetu Lindi kukawa na mabadiliko makubwa kama yaliyopo Dar es Salaam. Kuna siku nimeshawahi kukueleza Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso kwamba ningeomba Eng. Juma Meneja wetu wa Lindi aje kuja Dar es Salaam na timu yake kuja kujifunza namna ambavyo wanatoa huduma ya maji safi na maji taka ili kuhakikisha kwamba wananchi wa lindi wanaunganishiwa maji na kila mwananchi anapata huduma hiyo ya maji na kuweza kuchangia Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu. Katika Mji wetu wa Lindi tumepata fedha nyingi tangu mwaka 2021/2022 na utekelezaji wa miradi mingi unaendelea, miradi mingine imekamilika. Kwa mfano kama pale Ng'apa, Teleweni, Tandangongoro mradi wa Shilingi bilioni 2.8 umekamilika, na wananchi wanapata maji safi na salama. Pale Mingoyo pia tuna mradi wa tenki lenye ujazo wa litu 100,000 umekamilika na wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji. Fedha za *COVID* 19 kwa ajili Mradi wa ujenzi wa tenki la ujazo wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

lita 100,000 pale Kiduni zimetolewa na mradi unaendelea kujengwa; na hatimaye muda si mrefu utakamilika na wananchi wataendelea kupata maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunao mradi mkubwa sana pale Mitwero uliogharimu shilingi bilioni 3.5 ambaa umekamilika kwa asilimia 80. Bado mradi ule unaendelea kusambaza mabomba kutoka Mitwero kwenda Mbanja na Jimbo la Mchinga ambako mama yangu amezungumzia hapa. Kwa hiyo ninaamini mradi utakapokamilika utakuwa umetoa huduma nzuri katika majimbo haya mawili na wananchi wataendelea kupata maji safi na salama.

Kwa hiyo ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu kwa kazi hii na upendo mkubwa wa wananchi wake wa kuhakikisha kwamba wataendelea kupata huduma ya maji safi na maji salama kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwalinda wananchi wetu ili waendelee kuwa na afya nzuri na kupunguza gharama kubwa ya matibabu inayosababishwa na wananchi kunywa maji ambayo si salama. Kwa hiyo pamoja na mambo hayo mazuri ambayo yamefanywa katika jimbo la Lindi mjini bado tunazo changamoto mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba kila mwananchi anavuta maji nyumbani kwake. Kwa sasa tunayo changamoto mabomba yale makubwa ambayo wananchi wanataka kuvuta maji, lakini mabomba yamepita umbali mrefu na hivyo wananchi wanashindwa kuunganisha kwasababu gharama ni kubwa. Yawezekana mwananchi mwingine akaambiwa kutoka kwenye bomba kubwa mpaka nyumbani kwake analazimika kununua mita 300 au mita 400; sasa gharama ya kuvuta maji mpaka nyumbani kwake inakuwa kubwa. Kwa hiyo wananchi wengi wanashindwa kumudu kuhakikisha kwamba wanavuta maji nyumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, na suala hili tulishalizungumza na Mheshimiwa Waziri na nilishakueleza na ulisema kwamba miradi ikishakamilika basi utatuongezea mtandao wa maji

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuhakikisha kwamba wananchi wa Lindi wanaendelea kupata unafuu wa kuvuta maji nyumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, tunayo maombi mapya katika maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba mtandao wa maji unaendelea. Tuna eneo la Kitumbikwela upande wa pili wa Bahari. Tumeomba fedha Bilioni 1.95 ili kuwezesha kuweka mtandao huu kuititia Kijiji cha Mkundi, Mnengule, Iyato, Mtalala, Mwitingi Mwamoja na Nachingwea; tuhakikishe kwamba fedha hizi Mheshimiwa Waziri unatupatia ili kuhakikisha mtandao huu unakwenda kutekelezwa na wananchi wa upande wa pili wa bahari waweze kupata maji safi na salama. Tunajua kwamba maji yapo lakini bado hayajasambazwa kwenye mabomba katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna mradi mwagine wa usambazaji wa mabomba katika maeneo ya Mlandege, Muhimbili, Kipuri, Mmongo pamoja na Mnazi Mmoja; nayo tumeomba Bilioni 1.44. kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunategemea bajeti yetu itakapopita basi haraka uweze kutupatia fedha kwa ajili ya kwenda kuitekeleza hii miradi mipya kuhakikisha kwamba tunaweka wigo mpaka wa wananchi kufunga maji na kuweza kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna mradi mpya wa Angaza Sekondari ambao utagharimu Shilingi milioni 740, nayo ni maombi mapya kwako Mheshimiwa Waziri. Tunajua ya kwamba una kiu kubwa kuona kwamba Lindi kunakuwa na mabadiliko makubwa na mapinduzi makubwa ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Lindi wanapata maji na sisi tuweze kuchangia mapato ya ndani katika Wizara hii ya Maji. Kwa hiyo bado yapo maeneo ambayo hayapo kwenye mpango. Tuna Kijiji cha Ruaha Mtaa wa Ruaha tuna kaya takriban 400 wanakosa maji safi na salama. Tunaiomba Serikali kuhakikisha kwamba wana Ruaha japo kwa kuwachimbia kisima.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna eneo la Madingula...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde 30 Mheshimiwa Hamida, malizia.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: ...lakini bado tuna mtaa wa Mitonga kule Kata ya Mbanja ni mbali kutoka barabara kubwa, nao wanakosa maji. Tuhakikishe kwamba wananchi hawa tunawachimbia visima kwa haraka ili kunusuru maisha yao kwasababu wanatafuta maji umbali mrefu zaidi ya kilometra tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba wanatusaidia ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya hayo yote niendelee kumpongeza Jumaa Aweso kwa unyenyekevu mkubwa...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekisho Shangai atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru, nami nichangie hotuba ya Waziri wa Maji. Awali ya yote niwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngorongoro kwa kunichagua kwa kura nydingi sana.

Mheshimiwa Spika, nami niungane kuwapongeza timu nzima ya Wizara ya maji kuanzia Waziri Mwenyewe, Makatibu Wakuu, na Naibu Makatibu Wakuu, lakini pia nimpongeze Eng. Andrew ambaye ni meneja wa RUWASA Wilaya ya Ngorongoro. Pamoja na mazingira ya Wilaya yetu na kutokuwa na vitendea kazi kwasababu hawana gari kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sasa kwasababu gari yao waliyokuwa wanaitumia ni mbovu; na unavyojuwa Wilaya yetu ya Ngorongoro ukitoka Kata moja kwenda Kata nyingine unatumia zaidi ya kilometra 70 hadi 100. Kwa hiyo ni lazima tuwatafutie vitendea kazi ili waweze kufanya kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti iliyopita mwaka 2021/2022 Wilaya yetu ya Ngorongoro tulitengewa bajeti ya Shilingi bilioni 7.1 lakini mpaka ninavyozungumza tumepokea Shilingi 1,200,000,000 tu kwa ajili ya miradi ya maji. Sasa tumbakiza mwezi mmoja kwa ajili ya kukamilisha mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, tushukuru kwamba tumepata kiasi hicho, lakini kiuhalisia tukijaribu kuangalia, kwasababu tuna miradi 13 inayoendelea mpaka sasa hivi; lakini fedha zillizotengwa pia kwa mwaka 2022/2023 zimetengwa Shilingi bilioni 1.9; na kabla hatujamaliza mwaka huu bado tunadai zaidi ya Shilingi bilioni sita na fedha ambazo hazijaenda kwa ajili ya miradi ya maji inayoendelea kule Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, je, tunategemea nini? Kwasababu leo tunawadai Shilingi bilioni sita ya bajeti iliyopita maana yake sasa miradi inayoendelea pale kwenye Wilaya ya Ngorongoro ni miradi ambayo tutaenda kuiona kama ni *White Elephant Projects*. Kwasababu kama hatupeleki fedha kila siku labda tunapeleka kwa mradi wa Shilingi milioni 300 tunapeleka Shilingi milioni 50 itawezesha wananchi kupata maji? Na ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi inasema kwamba ifikapo mwaka 2025 vijiji tuwe na asilimia 85 ya watu wanaopata maji na mjini ni 95. Kwa mtindo huu wa kuweka bajeti halafu tunapeleka *a little amount of money* tutatekeleza kweli miradi hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine, ukijaribu kuangalia miradi mingi ambayo imetekelezwa; Mheshimiwa Aweso nikukumbushe tu na nikupongeze pia, kwamba umeweza kufika kwenye mradi wa vijiji nane ambao ni mradi maarufu sasa hivi Ngorongoro. Mradi huo umeanza tangu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwaka 2018 lakini mpaka leo bado tunajenga chanzo tu. Niombe tu, kwamba tutenge fedha za kutosha ili tuweze kumaliza mradi huo wa vijiji nane ambao ni maarufu kwa jina la mradi wa Mageri.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali, kama kweli tunataka kuwasaidia wananchi, akina mama kwenye vijiji na kwenye vitongoji kwenye kata za Enguserosambu, Tinaga, Digodigo na kata nyingine zilizopo karibu kwa ajili ya mradi huo akina mama wanateseka kwenda kuchota maji mtoni kila siku, wanateseka kufuata maji usiku na mchana; kama kweli tunawapenda wananchi wetu na ni kweli kwamba tunataka nao waondokane na umaskini tuwaletee maji ili muda wanaotumia kwenda kuchota maji mtoni watumie kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo linatokea, sisi wafugaji tunahitaji maji kwa ajili ya binadamu pamoja na mifugo. Kwenye llani yetu ya Chama Cha Mapinduzi inasema kwamba tutajenga mabwawa kwa kila Wilaya, lakini Wilaya yetu ya Ngorongoro hakuna hata bwawa moja, ukienda pia Longido hakuna hata bwawa moja. Tunahitaji kujenga mabwawa kwa ajili ya mifugo ambayo kwa sisi tunaweza kutumia yale mabwawa kwa ajili ya mifugo pamoja na binadamu. Sisi wakati wa mvua tunaweza tukapata maji, kuna maeneo mengi. Kwa mfano Kata za Malambo, Oloipiri pamoja na Maalon hawana maji; na kata nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wilaya yetu tuna vijiji 65 lakini vijiji ambavyo vinapata maji angalau ni 34, vijiji 28 vinapata maji ambayo si toshelezi na vijiji zaidi ya 13 havina maji kabisa. Kwa hiyo niiombe Wizara tuangalie namna ya kuwasaidia wale wananchi nao waweze kupata maji ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine, kule Loliondo wananchi wanapata maji *Unit* moja kwa shilingi 2,500, hicho ni kiasi kikubwa sana. Mama zetu na watu wengine wameamua kurudi kwenda kuchota maji mtoni kwasababu hawawezi kumudu gharama ya maji. Wakati mwingine

wanasema wasimamizi wanaweka bei ambazo wananchi hawajui. Kwa hiyo tuombe, kama ikiwezekana wizara ijipange zilete zile *pre-paid meters* ambazo zitawasaidia Watanzania kuibowi.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine mimi niombe na nisisitize sana. Fedha hizi ambazo zilitengwa kwa bajeti ya mwaka 2021/2022, nikucombe sana uweze kuangalia angalau hata tupate fedha kwaajili ya miradi inayoondelea. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, kengele imeshagonga, ahsante sana. Mheshimiwa Edward Olelekaita atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, ajiandae.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Utanisamehe sauti yangu leo si nzuri sana. Lakini kwanza kabla ya yote kabisa nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya kutatua kero za maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kiteto wakati tunachaguliwa Mkoa wa Manyara, nilishazungumza hapa mwaka jana, upatikanaji wa maji ni asilimia 58, *way below national average*. Lakini nafurahi sana kwamba kwa mwaka jana na mwaka huu bajeti ya mwaka huu, nilikuwa naongea na *Engineerwananiambia* kwamba mpaka Disemba tutakuwa tumefikisha asilimia 68 *well done*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao wote kwakweli kwa kazi kubwa wanayofanya kumsaidia Rais. Tunaona kila mahala wanapokwenda kusimamia miradi ya maji *big up*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mkurugenzi wa *RUWASA* na Meneja wa *RUWASA* Mkoa wa Manyara kwakweli kwa kazi kubwa wanayofanya. Ndiyo maana Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Makamu wa Rais wakati alipotembelea Simanjiro aliahidi fedha kwa Meneja wa RUWASA wa Mkoa kwa kazi kubwa anayofanya, hii ni kutambua kazi yake kubwa anayofanya. Meneja wa RUWASA Kiteto anafanya kazi nzuri sana. Kwa kweli timu hii mmejipanga vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nilishazungumza hapa, kwamba Kiteto ni jimbo moja kubwa sana, zaidi ya Mkoa wa Kilimanjaro. Meneja wa RUWASA Kiteto hana gari. Alishalala siku moja mpaka saa nane kwenye mapori yale. Mheshimiwa Waziri tunaomba *Landcruiser* moja nzuri sana ili huyu meneja apate kufanyakazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alituletea mradi mkubwa sana wa maji pale Mjini Kibaya Kata ya Kalorenzi wenyе thamani ya shilingi millioni 400; ni mradi mzuri sana. Lakini nilisema mwaka jana kwamba miundombinu ya mabomba pale mjini yamechakaa. Kwa hiyo, hata tukipata haya maji ya milioni 400 bila kufumua mabomba ya mjini pale, na nilikuomba milioni 100, hata huo mradi hatutafaidi sana itakuwa na *linkage*. Naomba milioni 100 ili tufumue mifumo ya maji pale ili wananchi wa-enjoy maji milioni yenyе thamani ya Shilingi milioni 400 ambayo yameletwa na Mama Samia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabwawa. Kiteto ni kame. Nilishazungumza hapa tarehe 10 mwezi wa pili mwaka huu, kwenye swali namba 84, kuhusu Mabwawa ya Dongo, Dosidosi na Kijungu. Mliniahidi kwamba mtapata fedha na mtajenga mabwawa haya.

Naomba kwakweli Mheshimiwa Waziri nikufahamishe kuwa ilikuja timu ya Dosidosi hapa wakifuatilia Bwawa lao la Dosidosi; na nimeshazungumza mara nyangi sana hapa, kwamba wilaya hizi ambazo ni kame tusipopata mabwawa kwaajili ya wakulima na wafugaji kwakweli changamoto za ukame hata mifugo imekufa sana mwakajana kwasababu ya ukame huo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi najua bajeti hii umetutengea karibu bilioni mbili tena, tunakushukuru sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tunayaomba sana Mabwawa haya ya Dongo, Dosidosi, Kijungu ili wananchi hawa wakapate kunufaika na maji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru wadau wa maendeleo wanaosaidia miradi ya maji Kiteto kama vile *OIKOS*. Juzi tu siku mbili zilizopita tumekwenda kuzindua mradi wa vijiji 16 miradi ya maji ninawashukuru sana *OIKOS*. Kwakweli Mheshimwia Waziri hili Shirika la *OIKOS* mlisaidie na muwape *support* nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maabara ya maji naambiya zilikuwa takriban 16 nchi hii lakini wameleta maabara ya maji Mkoa wa Manyara, Shirika hili la *OIKOS*.

Mheshimiwa Spika, mashirika mengine yanayojishughulisha na miradi ya maji kwenye Jimbo la Kiteto ni; Shirika la *PINGOS*, *ELEWA AFRICA*, *KINAPA* na *PICODEO*. Mashirika haya yanahitaji *support* sana; na ninawashukuru sana kwa kazi kubwa wanayofanya. Juzi tu Kata karibu 10 zimenufaika na mradi huu Kata za Makame, Ndodo, Engusero, Lengateri, Loolera, Matui, Ndiringishi, Magungu na Bwawani kata 10 vijiji 16 kwakweli wanafanyakazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulishazungumza mimi na Mheshimiwa Waziri na nilimualika aje Kiteto; na kat i ya maeneo ambayo nilimuahidi tutatembelea ni kwenda Dongo kuangalia Bwawa la Dongo. Naomba sana, baada ya bajeti hii ambayo mimi najua itapita kwa *speed* kubwa sana kwa kazi unayofanya; tupange utembelee Kiteto. Vilevile nilimualika na Naibu Waziri pia twende Kiteto. Mheshimiwa Waziri tutampeleka Dongo huku huyu tutampeleka umasaini huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kiteto kwakweli kwa kasi ya maji, alikuwa ananiambia meneja wangu wa *RUWASA*, kwamba mpaka Juni mwaka huu tutakuwa tumetoka asilimia 52 ya maji mpaka asilimia 68, ambayo ni nzuri sana. Tukiendelea na kasi hii ile *dream* ya mama yetu yakuleta maji asilimia 95 vijijini na 85 tutafikia bila shida yoyote.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri, atakapohitimisha bajeti yake nitataka baadaye atuambie, zile mashine ambazo Mama Samia alisema ataleta kila mkoa hebu mtuambie imefikia wapi? Kwa sababu sasa tunataka kujishughulisha na mambo ya mabwawa yetu. Akifanya hivyo kwakweli Mwenyezi Mungu atambariki sana.

Mheshimiwa Spika, kwakweli Wizara Maji kwa kazi wanayofanya kwakweli tuwasaidie wapate pesa hizi za bajeti ili miradi hii ikatekelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kuunga mkono hoja, ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimwia Daniel Awack Tlemai ajländae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kupata nafasi ya kuchangia. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwakutoa fedha ambazo zimetekeleza miradi mingi ya maendeleo ndani ya wilaya yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri ni mionganini mwa Mawaziri ambao ni wasikivu wanasiliza Wabunge na wasikiliza wananchi kwa ujumla. Kazi anayofanya pamoja na wasalidizi wake ni mfano mzuri wa kuigwa kwani anawatendea haki Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimuombe sana Mheshimiwa Waziri; Mkao wa Katavi, Mkao wa Kigoma, Mkao wa Rukwa wote tuna kilio cha aina moja. Sisi tuna chanzo cha uhakika cha maji cha Ziwa Tanganyika, ziwa ambalo linakina kirefu na ziwa ambalo lina maji safi ambayo ni mengi na yanaweza kutumika kwa mikoa yote na mpaka kutoa ziada kwenye maeneo mengine. Tunachoomba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kile chanzo kianze kupeleka maji kwenye mikoa hiyo mitatu ikiwemo Mkao wa Katavi ambao mimi ni sehemu ya jimbo na Mheshimiwa Waziri alishafika mpaka kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

eneo ambako chanjo kinachopendekezwa kutoa maji kuyatoa eneo la Karema kuyapeleka Makao Makuu ya Mkoa pale Katavi, Mpanda Mjini inaweza ikasaidia sana kupeleka huduma ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi bila kupata chanzo cha maji cha kutoka Ziwa Tanganyika tutaendelea kupata miradi midogo midogo ambayo haitasaidia sana. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kutupatia fedha kwaajili ya miradi midogo midogo lakini mwarubaini wa suluhisho la maji kwenye Mkoa wa Katavi ni kuyatoa maji Ziwa Tanganyika na kupeleka eneo la Makao Makuu ya Mkoa Mpanda Mjini. Niombe sana Mheshimiwa Waziri ninachokizungumza wewe mwenyewe ni shuhuda na unajua, na nikupongeze sana. Umefika kwenye eneo la chanzo cha maji na umetoa ushirikiano mkubwa sana kwa watendaji na niwapongeze Watendaji wa Mkoa kwa ujumla wa Katavi na meneja wa *MRUASA* wa Wilaya ya Tanganyika kwa ubunifu ambao na wewe mwenyewe ulishuhudia mpaka ukafika ukaona umuhimu wa yule meneja ukatoa fedha za kwako kumpa kama zawadi ambayo ni motisha kwa ufanyaji kazi mzuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni wakandarasi ambao wanateuliwa na Serikali kwaajili ya kujenga ile miradi ya maendeleo. Tunaye mkandarasi ambaye alipewa kazi ya kujenga Mradi wa Katuma mkandarasi huyu *Hema-Tec* anamuda mrefu toka amesaini mkataba ambao ultakiwa kuwa amekamilisha huu mradi ifikapo tarehe 21 mwezi wa sita. Wenzie ambao walisaini pamoja huu mkataba walishatekeleza miradi yao na imekamilika na maji yameanza kutoka; lakini huyu tangu aliposaini huo mkataba hata kwenda kwenye *site* hajafika na alishasaini huo mkataba.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri aingilie kati mkataba wa *Hema-Tec* usimamishwe ili tutafute mkandarasi ambaye anauwezo anayeweza kwenda kufanyakazi kuliko kuwarundikia kazi ambao hawana uwezo wa kufanya kazi. Eneo hili ni muhimu na naamini si Mpanda tu peke yake au Katavi kwa ujumla;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wapo wakandarasi wabovu ambaو wanapewa miradi ya Serikali wanashindwa kuitekeleza kwa wakati. Niombe muwapime na muangalie vigezo ambavyo mnapowapa kazi wahakikishe wanaenda kutekeleza kazi ambayo inaweze ikawasaidia wananchi kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo eneo lingine ambalo Serikali ilifanya kwa nia njema tulipoanzisha jumuiya za watumia maji. Jumuiya hizi zinafanya kazi nzuri, lakini kwa bahati mbaya sana kuna waraka ulitoka wa Serikali uliokuwa unataka kila jumuiya za watumia maji wawe angalau wana elimu ya kuanzia kidato cha nne, na huko nyuma Serikali iliwapa elimu ya mwanzo waliokuwa wanasisimamia ile miradi huko nyuma, ambaو waliokuwa ni vijana wazalendo wa kutoka kwenye maeneo husika ya miradi husika. Kwa bahati mbaya sana tangu mlipotoa ule waraka mkaleta vijana wengine wapya ukweli usimamizi umekuwa si mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe muwarejeshe wale ambaو mliwapa elimu, mliwasaidia mkaapa elimu na wakajitolea wamefanya kazi na ilikuwa na ufanisi. Na ukichunguza waliokuwa huko nyuma walisisimamia miradi vizuri na mapato ya jumuiya za maji yalikuwa yakijiendesha vizuri. Sasa hivi mmeongeza gharama kwa kuwajaza hao vijana ambaو ukweli miradi mingi imeshindwa kufanya kazi ile iliyokusudiwa ni eneo hilo ambalo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa sekunde 30 malizia.

MHE. SELEMANI KAKOSO:...ni eneo hilo ambalo tunashukuru, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafutaiwa na Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, ajiandae.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu, hoja ya Wizara ya Maji, Wizara yenye umuhimu mkubwa sana katika maisha ya watanzania. Nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu kwa kazi kubwa ya kutoa fedha kwenda katika wizara hii ili kuweza kumtua ndoo mwanamama lakini kuhakikisha kwamba maji ni uhai yanatekelezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Aweso msaidizi wake mama yangu Christina, *Engineer Sanga Mtendaji* Mkuu wa Wizara lakini kubwa zaidi Meneja wa RUWASA Mkoa wa Morogoro na Mhandisi Meneja wa Wilaya, Wilaya ya Morogoro Vijiji kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii katika kukamilisha kiu ya Watanzania katika kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ni mtu ambaye hana akili au asiyeona, lakini kwa yoyote anayeona kazi kubwa ya mapinduzi katika sekta ya maji ndani ya kipindi kifupi anakila sababu ya kujua kwamba kuna mambo mazuri yanafanyika. Nitumie nafasi hii cha kwanza mfano kwenye jimbo langu la Morogoro Kusini kuna mradi wa Bwakila juu tumepata milioni 680, kuna mradi wa Lundi tumepata milioni 492, kuna mradi wa Mvuha huu ni mradi kuititia *UVIKO* tumepata milioni 680, ukijumlisha kuna bilioni 1.772. Kwakweli tunakila sababu ya kuipongeza Serikali na kuipongeza Wizara kwa kuhakikisha kwamba haya mambo ambayo Serikali inataka yanafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kwenye jimbo langu kuna ukarabati wa mradi wa Singisa tumepata milioni 60 ahsante sana Mheshimiwa Waziri, lakini mradi wa Matombo - Lugeni tumepata milioni 100 kwaajili ya kukarabati, tunakila sababu ya kupongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi nimpongeze waziri kuititia mradi wa Bonde tumejengewa mabirika 10 na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

vizimba zaidi ya 20 kwa ajili ya kunyweshea maji mifugo lakini vile vile wale wananchi wa jamii ya wafugaji kupata maji safi na salama tuna kila sababu ya kupongeza. Tumechimbiwa visima viwili virefu Kata ya Milengwelegwe na Mngari tunakila sababu ya kupongeza, mimi kama mbunge wao napongeza kwa kazi kubwa nakupongeza ahsante sana mdogo wangu Aweso kwa kazi kubwa ambayo unaifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu pamoja na pongezi bado tunachangamoto za maji. Katika Kata ya Selembala, kuna Vijiji vya Kiganyira, Magogoni, Mji Mpya na Bwira Juu. Huko ndiko kwenye Bwawa la Kidunda tunapokwenda kujenga. Tumewatoa wananchi kwenye maeneo ambao walikuwa na maji yao sasa hivi wanakwenda mtoni kuchota maji wanakumbana na adha ya kukamatwa na mamba. Ninakuomba tupatiwe visima. Lakini vile vile Kata ya Bwakila chini kuna Vijiji vya Dakawa, Sesenga, Vigolegole, Kichangani Kata ya Kisaki na Nyalutanga tunaomba mtusaidie visima vya maji ili wananchi wetu wapate maji safi na salama na sisi tufikie azma ya Serikali ya kupata maji safi na salama tutakapofikia mwaka 2025 kama vile Serikali inavyosema.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Waziri wa Maji; kuna vijiji vya Mtombozi, Lugeni, Kisemu, Gozo Kibangile na Mtamba kuna matatizo makubwa ya maji. Idara ya Maji kuititia RUWASA na mkoa tayari walishafanya upembuzi yakinifu. Kuna mto unaitwa Kibana una uwezo wa kusababisha vijiji vyote hivi vikapata maji safi na salama. Tayari walishaandika *proposa/na ipo* kwenye Ofisi ya Mkoa inahitaji kama bilioni tatu tu. Nikuombe Waziri angalia kwa namna moja au nytingine unaweza kutusaidia vipi tuondokane na adha hii ya maji. Mimi naamini kabisa miradi hii ikikamilika wananchi wetu watapata maji safi na salama, lakini kubwa zaidi wataweza kutusaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nikuombe Mheshimiwa Waziri umetusaidia katika kuititia mradi wa UVIKO mradi wa mvua ambao ndio Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Morogoro Vijiji, pale tayari kuna mradi ambao unatakiwa ufanyike lakini kama mkiweza kutuongezea fedha

kiasi kama cha milioni 200 mradi ule kwa kujenga *tank* kubwa, ambapo lililokuwa *designed* ni dogo, utaweza kufanikisha maji kufika katika Kijiji cha Sangasanga, Tulo, Lukulunge na hapo tutaenda kuwasaidia wananchi wetu kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze mdogo wangu Aweso na Wizara kwa safari hii kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga Bwawa la Kidunda. Ni uhalisia suluhisho la upatikanaji wa maji wa Jiji la Dar es salaam, Pwani na hata baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Morogoro ni kujenga Bwawa la Kidunda. Bwawa la Kidunda lipo katika Jimbo la Morogoro Kusini katika Kata ya Selembali.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, tunakwenda kujenga mradi mkubwa ambao unatakiwa ulete matokeo chanya; sijui Serikali tumejipangaje katika uhifadhi wa mazingira ili kuruhusu vyanzo vyta mito ambayo inajaza maji katika Mto Mvua iendelee kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri katika hatua za muda mfupi na katika mabonde walivyoonyesha katika jitihada za kutengeneza mabirika ili mifugo isiende mtoni tungeweza kusaidia mkachimba mabwawa ng'ombe wakaenda kupata hifadhi ya maji kwenye mabwawa badala ya kwenda mtoni kuharibu kingo za mto, lakini wakati wa kiangazi wakapanda juu kwenda kwenye vyanzo vyta mito ambavyo wataenda kuharibu mazingira. Matokeo yake, nataka tu kuthibitisha, kama hatkuuangalia hili hata huu mradi tutakuwa tumepoteza fedha bure ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Waziri, nimetoa angalizo kwa sababu ya uzoefu wangu kama Mbunge katika eneo lile. Na ushuhuda wewe mwenyewe unajua; mwaka huu huu Dar es Salaam walikosa maji. Lakini walikosa maji si kwa sababu Mto Ruvu ulikauka, hapana, ni kwa sababu vyanzo vyta mito mitano ya Ngazi, Mto Mvua, Mto Dutumi, Mto Mgekakafa ilivamiwa na wafugaji juu kwa ajili ya kuokoa mifugo yao. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo Mheshimiwa Waziri nikuombe tu, katika huu mradi wa mabirika 10 karibu tunamaliza, ambao umejengwa na bonde, nikuombe wewe nawe ukipata muda twende tukazindue wote kwa pamoja ili kazi iendelee kuwa nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho zaidi kabisa nikushukuru kwa kazi kubwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajandae.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, awali nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wenzake wote Wizarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme katika Jimbo la Karatu tuna changamoto; na bahati nzuri sana Naibu Waziri alifika katika Jimbo la Karatu. Lakini vilevile Waziri alifika takribani miezi mitatu. Mwezi wa pili alifika katika Jimbo la Karatu. Lakini pale Karatu maji yanapatikana kwa asilimia 33 katika taasisi ya Serikali. Lakini kuna taasisi binafsi ambazo upatikanaji wa maji unapatikana kwa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, shida kubwa katika Jimbo ka Karatu ni bei kubwa ya maji. Bei ya maji Karatu kwa *unit* moja inapatikana kwa Shilingi 3,500. Katika taasisi ya Serikali inapatikana kwa Shilingi 1,750. Lakini Mheshimiwa Waziri alifika katika Jimbo lile na akasema ndani ya siku 30 bei hii inaweza na ikawa uwiano. Hili haihitaji hela ya Serikali, inahitaji kauli ya Waziri kusema bei iuzwe kwa bei fulani katika Jimbo la Karatu. Na mimi siombi niongezewe fedha, mimi ninachohitaji ni kauli ya Waziri kusema bei ya maji ambayo inatokana na maelekezo ya EWURA katika Jimbo la Karatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, alisema jambo hili lingeckukua ndani ya siku 30 lakini takribani leo ni miezi mitatu na siku tano. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, hii pia ni sehemu unapofutilia, unapozunguka nchi hii maamuzi magumu unapofanya maeneo mengine. Sijajua kwa nini Karatu inashindikana bei ile kuwa ya aina moja; kwa sababu kuna wengine wanauza kwa Shilingi 3,500, wengine wanauza kwa Shilingi 1,750. Na ulifika katika Jimbo la Karatu ukasema hata hao wa chini wanaouza Shilingi 1,750 bado wanawaibia wananchi wa Jimbo la Karatu.

Mheshimiwa Spika, napenda sana uweze kutoa kauli katika Jimbo la Karatu, wananchi wale waweze kupata fursa ya kuweza kupata kulingana na bei katika maeneo mengine katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naamini ukiwa katika Jimbo la Karatu ulisema kwamba uliweza kushusha bei ya hapa Dodoma, kama sikosei ilikuwa Shilingi 1,200 au Shilingi 1,300 kwa *unit* na Arusha na maeneo mengine yaliyoko ndani ya nchi hii mpaka Dar es Salaam. Naamini hilo kwako wewe si kitu kigumu, unaweza kulifanyia kazi kwa muda mfupi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo lile kuna mradi ambaao unaendelea, naamini Serikali ilitoa fedha za kutosha Shilingi zaidi ya Milioni 800. Lakini kuna eneo la Ayalabee limetoa Shilingi Milioni 800 na kuna eneo la Bwawani limetoa zaidi ya Shilingi Milioni 400, lakini mradi ule unahitaji kama zaidi ya Shilingi Milioni 700. Lakini na katika eneo hili la Ayalabee imefika mradi asilimia kama zaidi ya 80 lakini mradi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Bwawani asilimi ni 34. Asilimia hizi zote 80 zikikamilika asilimia 100 na ile asilimia 34 ikikamilika asilimia 100 tunaweza kupata zaidi ya asilimia 70 katika Mji wa Karatu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri najua alitembelea maeneo mengi katika Jimbo la Karatu wakati umetembelea mwezi wa pili. Tulifika Bonde la Easi ambako upatikanaji wa maji ni wa asilimia zaidi ya 60. Lakini vilevile tulifika katika maeneo mengine katika Jimbo la Karatu, upatikanaji wa maji haujazidi asilimia zaidi ya 60 katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwake, na kipindi kile wakati umetembelea Jimbo la Karatu ultiuhidi sisi wananchi wa Jimbo la Karatu. Ulisema upatikanaji wa maji Karatu ili shida hii iishee kabisa ilionekana kwamba tunahitaji zaidi ya Shilingi Bilioni 4.5. Na mimi naamini katika Serikali na Wabunge wengi wamesimama katika ukumbi huu kwamba kuna maeneo mengine wapeleke Shilingi Bilioni 10, kuna maeneo mengine wapeleke Shilingi Bilioni 15; na mimi naomba katika eneo hili la Karatu tuweze kupata Shilingi Bilioni 4.5 na Mheshimiwa Waziri uliahidi katika Jimbo la Karatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na uliahidi wananchi wa Jimbo la Karatu kwamba Shilingi Bilioni 4.5 kwa Serikali si kitu kikubwa sana na ulisema Serikali haifanyi biashara. Kazi kubwa ya Serikali ni kutoa huduma na wananchi wa Karatu walikunukuu vizuri. Na mimi nikuombe umekuja Karatu na wananchi wa Karatu wamekusikiliza vizuri na wamekuelewa vizuri. Nakuomba sana usinitengenezee ajari katika Jimbo lile tuweze kupata huduma ili wananchi wale waendelee kuniamini Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwamba tumepata katika maeneo kata mbalimbali katika Jimbo la Karatu. Kwa mfano; katika eneo hili la Mang'ola Juu tumepata Shilingi Milioni 191, Kata ya Daa lakini pale Kata ya Kansay tumeweza kupata Shilingi Milioni 225. Vilevile mradi mwengine katika eneo la Mang'ola Balasani tumepata Shilingi Milioni 360. Kuna eneo lingine Kata ya Rotya tumeweza kupata Shilingi milioni zaidi

ya 360. Maeneo mengine ya Barai tumeweza kupata Shilingi Milioni 360.

Mheshimiwa Spika, kazi imefanyika na sisi tunashukuru sana Wizara. Nami pia kama Mbunge wa Jimbo wakati naingia kama Mbunge wa Jimbo lile fedha ilikuwa ya Wizara ya Maji kidogo ni changamoto lakini tangu mwaka jana, mwaka huu fedha katika Jimbo lile imepatikana kwa asilimia kubwa. Hata katika hizo hela za UVICO - 19 tumeweza kupata shilingi milioni 500 na mradi unaendelea na unasambaa katika Mji wa Karatu kwa zaidi ya kilometra 45. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba sasa tumesambaza ule mradi kwa eneo la mabomba tu kwa kilometra 45 ili maji yale yasambae vizuri nahitaji mradi ule ukamilike ambao unahitaji zaidi ya shilingi milioni 800. Na sasa imeshatolewa kama shilingi milioni 600. Kinachohitajika pale ni shilingi milioni 250 na eneo hili la Bwawani hela zimeshaenda zaidi ya shilingi milioni 300. Kinachohitajika pale zaidi ya shilingi milioni 300 ili iweze kufikia shilingi milioni 700. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nakuomba hili kwako siyo kubwa na kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Chama cha Mapinduzi naamini siyo kitu kikubwa. Naomba, eneo hili likikamilika katika Jimbo la Karatu tutakuwa tumesogea sana katika eneo hili la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba kazi imefanyika, tunashukuru kwa hili ambalo limefanyika na japo naamini katika mwaka huu wa fedha miradi mingi ile ya mwaka jana wanaimalizia. Naamini hii miradi mkimalizia tutapata maji, kwa sababu katika Jimbo la Karatu kuna changamoto kubwa. Kuna miradi mingine ilikuwa ya miaka zaidi ya name, saba ilikuwa imemelala lakini baada ya Waziri kuingia na Serikali ya Awamu ya Sita kuingia miradi mingi imefufuliwa na wananchi wetu wanaendelea kupata maji katika eneo la Jimbo la Karatu. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi na pia naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima lakini pia nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake, ndugu zangu Aweso na Injinia Maryprisca kwa kazi nzuri sana mnayoifanya kwenye Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Sumve tulikuwa tunahangaika kwa muda mrefu, na tulikuwa tuna kilio chetu, kwamba katika Mkoa wa Mwanza na Majimbo yake tisa, Jimbo la Sumve ndilo lilikuwa Jimbo pekee halina maji ya bomba kutoka Ziwa *Victoria*; na kimekuwa ni kilio chetu humu. Tulikuwa kila mara tunajiuliza, hivi tatizo letu sisi ni nini? Hawa wenzetu kwa nini wanayo sisi hatuna mpaka yanataka kuleta Dodoma? Kumbe tulikuwa hatufahamu siri ya urembo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siri ya urembo ni Mama Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais Samia Suluhu Hassan ndiye amekuja kutuletea maji ya bomba kutoka Ziwa *Victoria* kwenye Jimbo la Sumve. Nafikiri ingekuwa tunaruhusiwa kujenga sanamu, alitakiwa ajengewe sanamu na watu wa Sumve. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa jambo hili lilihofanyika ambalo nimeliona kwenye bajeti hii, kwa sababu tumeshajua siri ya kupata maji ya bomba kutoka Ziwa *Victoria*. Tumeshajua siri ya maendeleo ya uhakika sisi watu wa vijijini, naamini wenzangu kule vijijini ikifika muda wanahitaji kuchagua, hawataacha kumchagua Rais Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso mimi nimekuwa nikilalamika na Wizara ya Maji kuhusu vijiji vyat

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Sumve kupata maji ya Ziwa *Victoria* lakini leo nikiangalia kwenye bajeti ninaona kwamba kuna maji yanatoka Hungumalwa yanapitia Mwankulwe yanaenda mpaka Malampaka kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mashimba Ndaki, halafu kutoka Malampaka yanakuja Malya yanaenda kwenye vijiji vyote vya Kata ya Malya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu wa Talaga, Mwitambu, Kitunga, Mwamembo na watu wa Kijiji cha Kiminza kwenye Kata ya Lyomo wanapata haya maji. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo la Sumve maji ya bomba kutoka Ziwa *Victoria* hayaishii hapo yanatokea Ukiliguru yanakuja kupita kwenye Kijiji maarufu cha Kolomije yanaenda kwenye Kijiji cha Mantale yanaenda kwenye Kijiji cha Ishingisha yanaenda kwenye Kijiji cha Sumve yanaenda kwenye Kijiji cha Bungulwa na Kijiji cha Isunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili jambo kwa watu wa Sumve huu ni muujiza walioustubiri tangu dunia iumbwe. Kwa hiyo, nashukuru sana Serikali ya CCM kwa kazi kubwa walioifanya. Mheshimiwa Waziri amefikia kiwango akawaambia watu wa RUWASA wabadili *design* ili Jimbo la Sumve lipate maji. Walikuwa wanapeleka bomba lenye nchi nane lakini baada ya sisi kusema humu amewaambia wabadili *design* na tenda imechleweshwa kutangazwa ili waweke bomba la nchi kumi na wiki ijayo Mheshimiwa Waziri wamesema wanatangaza hiyo tenda ili watu wa Sumve tupate maji ya bomba kutoka Ziwa *Victoria*. Hii kwetu ni neema na ni jambo la kujivunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Lakini Mheshimiwa Waziri sisi watu wa Sumve bado tunakushukuru. Upo mpango pia wa kupeleka maji ya Ziwa *Victoria* kutokea Nyamilama kwenda kwenye Kata ya Lyoma kwenye vijiji vya kina Mweli, Kunguru, Lyoma na Busule. Hili ni jambo la heshima sana kwa wananchi wa Sumve. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tukiacha haya mambo, Jimbo la Sumve lina kata 15. Hizi kata tunazozizungumzia ni kata tano. Kata 10 ili zipate maji ya bomba kutoka Ziwa *Victoria* inabidi yatokee Magu. Naomba Wizara isiusahau mradi wa maji ya bomba kutoka Ziwa *Victoria* kuja kwenye kata 10 zilizobaki za Jimbo la Sumve kutokea Magu.

Mheshimiwa Spika, mbali na kuwakumbusha hilo bado tunashukuru. Mimi kwa kweli leo Mheshimiwa Waziri utanisamehe, itabidi leo niwe chawa, yaani nishukuru tuu kwa kiwango kikubwa kwa sababu umefanya kazi ambayo nilikuwa ninaililia kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna miradi kwenye karibu kila kata ya Jimbo la Sumve. Kuna mradi unaendelea kwenye Kijiji cha Ibindo Shilingi Milioni zaidi ya 500. Kuna mradi unaendelea kwenye Kijiji cha Mulya, kuna mradi umeshatangazwa tenda kwenye Kijiji cha Lyoma, kwenye Kijiji cha Wala, Kijiji cha Nkalalo, Kijiji cha Ligembe, Kijiji cha Mulula na Kijiji cha Ng'undya; vyote hivi vinaenda kutengenezewa mradi wa uhakika wa maji ya bomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri watu wa Sumve umetupa heshima kubwa. Wewe ni Waziri pekee ambaye umekuja tumeanza kunywa na sisi maji ya kutoka Ziwani. Tunategemea tutaanza kuyanya wa maana yake zamani ilikuwa ukitaka kuyanya inabidi ubebe ndoo uende Mwaloni. Sasa hivi tutakuwa tunafungua kwenye mabomba yanatoka.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho nataka kukuomba Mheshimiwa Waziri. Uhakikisho wa hii miradi kufanyika na kusimamiwa vizuri. Tumekuwa tuna shida sana kwenye miradi ya maji. Sisi Sumve kuna mradi unaitwa Waisunga - kadashi na mwabalatulu. Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kuja mwanzoni kabisa. Siku ile unakuja Mheshimiwa Naibu Waziri walifungua maji yakatoka, ulipoondoka wakafunga. Wakasema watamalizia kuweka mabomba kule Isunga ili yaanze kutoka, hawajamalizia Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa hiyo, bado kunashida. Kuna watu baadhi hawako *serious*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kuna mradi wa Mwabilanda maji yanatoka kwa msimu. Kuna Kamati za Usimamizi wa Maji wanaiba pesa kama hawana akili nzuri. Inafika wakati wanashindwa hata kulipia bili za umeme. Kwa hiyo, iko miradi chechefu ambayo mnatakiwa mtusaidie. Hata hii miradi inayokuja bila kuwa na usimamizi wa uhakika inaweza isiwe na tija.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri najua wewe ni mchapakazi, Jimbo la Sumve sisi tunataka tukuone tu, tukushukuru lakini tukuoneshe pia ambapo panavuja. Kwa hiyo, nikuombe sana ukipata nafasi uje Sumve tukushukuru, tukuoneshe panapovuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daud Protas. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anachapa kazi katika kuiendeleza nchi yetu ikiwemo katika Sekta hii ya Maji. Iakini pili nawapongeza pia Mheshimiwa Waziri rafiki yangu Mheshimiwa Aweso pamoja na dada yangu Maryprisca kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii na kuhakikisha kwamba wanaisimamia vizuri miradi ambayo inatekelezwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi katika Jimbo langu nimenufaika sana. Tangu nimeingia madarakani miezi 18 iliyopita tayari miradi zaidi ya 11 imekuwa ikitekelezwa yenye

thamani ya jumla ya Shilingi Bilioni 2.18. Kwa hiyo naipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ndani ya jimbo langu na nchi nzima kwa ujumla. Kwa mfano kuna vijiji nya njia nne tayari kuna mradi umeshakamilika pale. Somanga kuna mradi umekamilika, Mtumbeni Mpopera kuna mradi umekamilika, Kipatimu kuna mradi unaendelea kutekelezwa. Vilevile kuna ukarabati wa visima vifupi unaendelea kufanyika katika vijiji mbalimbali. Kipindimbi kuna mradi wenyewe thamani ya Shilingi Milioni 497 wa UVIKO-19. Lakini pia kuna Vijiji nya Malendego, Chumo, Chapita, Kinjumbi kuna miradi inaendelea kutekelezwa iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna uchimbaji wa visima unaendelea kufanyika katika Vijiji nya Mitole, Zinga Kibaoni Namayuni pamoja na Kisima Mkika. Pia nina furaha kubwa kusikia katika mpango wa bajeti wa mwaka ujao katika Kitongoji cha Nasaya, Kijiji cha Mtekimwaga pamoja na Kijiji cha Miteja, Kitongoji cha Masaninga Serikali imepanga kuchimba visima virefu ili kuweza kuwashudumia wananchi waweze kupata huduma ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufanisi huu uliopatikana bado kuna baadhi ya maeneo takribani vijiji visivyopungua 15 vina changamoto kubwa sana ya maji. Wamekuwa wakitumia majitope wakati wa masika, wakati wa kiangazi wanapata tabu sana kusafiri mbali kutumia visima nya asili kupata maji; navyo ni Vijiji nya Nandete, Nandembo, Namatewa, Ngarambi kwa Kinjeketile Ngwale huko, Nambondo, Bugo, Kinywanyu, Namakoro, Ngorongoro, Lyombanga, Somanga Simu, Handa, Mtende pamoja na Mwegei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ulizungumza hapa, kuna kauli zilitolewa na baadhi ya Wabunge jana na leo zinagongana kidogo. Lakini mimi niseme katika baadhi ya maeneo yetu ni kweli kuna hali fulani yakutoeleweka. Kwa sababu mgao wa fedha katika baadhi ya Majimbo au Wilaya umekuwa ni mdogo sana. Kwa mfano, tarehe 14 mwezi Machi mwaka 2022 mimi pamoja na Kamati yetu ya *PAC* tulitembelea katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mradi mmoja wa maji kule Manyara katika Kijiji cha Hydom kuna mradi pale wa bilioni 12 umewekezwa lakini unahudumia kata tatu tu.

Mheshimiwa Spika, lakini katika jimbo langu miradi yote iliyowekezwa pamoja na UVIKO-19 ina gharimu shilingi bilioni 2.18 tu, haifiki hata robo ya mradi mmoja tu ule ambao umewekezwa kule Manyara. Kwa hiyo kwa kweli jambo hili ni lazima Wizara ilifanyie kazi ili kuhakikisha hii keki inayopatikana iweze kugawanywa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimesema hapa kuna vijiji 15 bado vina shida ya maji. Kwa hiyo tukiigawa vizuri ile keki ni wazi kabisa kwamba mambo yatakwendwa vizuri. Na mimi katika kuzingatia hilo ningependa kusema kwamba nimefuatilia kuhusu utekelezaji wa maji kutoka Mto Rufiji kwa karibu sana kupitia DAWASA na RUWASA Wilaya ya Kilwa. Kule DAWASA tayari wameshapata *designer* wa mradi wa maji kutoka Mto Rufiji. Tayari walitanga zabuni wameshapata, na tayari wako katika hatua mbalimbali za kuelekea kutekeleza ule mradi ambapo wataweka chujio pale katika Kijiji cha Mloka kule Rufiji.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande wa Kilwa wao walikuwa nyuma kidogo tarehe 19 mwezi huu wanatarajia kufungua zabuni ya kumpata *designer*, yule Mhandisi mshauri kwa ajili ya ku-*design* mradi wa maji kutoka Mto Rufiji.

Kwa hiyo ombi langu na ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba hii miradi miwili iunganishwe. Inawezekana kwenye ku-*design* mradi ikawa wametofautina, lakini kwenye utekelezaji wa mradi ningeomba basi iuanganishwe ili apatikane mkandarasi mmoja ambaye atajenga huu mradi wa maji kutokea kule Mloka Rufiji, bomba basi kama litapita Ikwiriri au litakwenda kule Kibiti, likifika pale linagawanyika lile lingine linakwenda Kusini kuanzia wilaya ya Mheshimiwa Mchengerwa pale Rufiji inaendelea mpaka wilaya yangu linakwenda mpaka kwa mama Kikwete kule Mchinga Liwale, Nachingwea, Newala na maeneo mengine yote ya kusini. Lakini pia na hawa wa Kaskazini kwa maana ya Mkoa wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Pwani, Bungu Mkuranga mpaka Dar es salaam nao waweze kupata maji mengi yanayotokana na maji ya Mto Rufiji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna hii miradi ambayo inatekelezwa na Mfuko wa Maji, imekuwa na tatizo sana kwenye ulipaji. Pale mimi ninao ule mradi wa Kinjumbi pale ambao una gharimu shilingi milioni 326 za Serikali Mkandarasi hivi sasa ana miezi miwili ali-*rise claim* lakini mpaka leo haulipwi. Sababu ukifuatilia unaambiwa shida ni kwamba mlolongo mrefu kwenye hii miradi ambayo inatekelezwa na mfuko wa maji.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ijaribu kuona namna ya kupunguza mlolongo ili tusije tukaangukia kwenye changamoto ya kulipa riba ikaigharimu zaidi Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza jioni ya leo. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko atafuatiliwa na Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasamu ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa fursa ya mimi kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya maji sote tunajua kwamba maji ni uhai lakini zaidi maji ni uchumi.

Mheshimiwa Spika, nimeduwa nikishauri hapa, na sote tunajua kwamba Tanzania nzima tatizo la maji ni kubwa kwa kweli, kwamba tuje na suluhisho la muda mfupi wa kati na mrefu. Mathalani kwa Mkoa wetu wa Mara majimbo yote takribani asilimia 40 ya wakazi wa kule ndio wanapata maji, tena hapo nimeweka kiwango cha juu sana. Lakini ukiangalia *target* ya Wizara sasa hivi kwa maji vijijin ni *almost* asilimia zaidi ya asilimia 70 na mijini zaidi ya asilimia 85 na *target* kufikia mwaka 2025 wanataka maji vijijini yawe asilimia 85 na mjini yawe asilimia 95.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, na hii inatokana na uhalisia kwamba tunakuwa na takwimu ambazo tunazingatia tu miundombinu ya maji liliyotandikwa pale bila kujua uhalisia, kwamba maji yanatoka au la unakuja una-*count* kwamba maji yanapatikana kwa kiasi hicho. Hii inakuwa ni adha kubwa sana na inasababisha kwa kweli tuendelee kushuhudia Watanzania wakitembea muda mrefu kutafuta maji, na wengine wakiliwa na mamba na kadhalika

Mheshimiwa Spika, kwenye miradi ya miji 28 mwanzoni Mji wa Tarime ulikuwepo, lakini nimesoma Ibara ya 122 ya hotuba ya Waziri hapa anaeleza kwamba ule mkopo wa kutoka India miji 24 tu ndiyo inaenda kutelelezwa na kuanzia mwezi Aprili na kuendelea. Ambapo Mji wa Tarime Songea na Mafinga na kwingine imeondolewa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 allyekuwa Rais Hayati Maguful alivyokuwa amezuru Mkoa wa Mara akiwa kwenye viwanja vya *TTC* aliwatamkia bayana wananchi wa Tarime kwamba maji yanakwenda kutoka Ziwa Victoria kuja pale, 2017, miaka mitano sasa hivi. Na tumekuwa tukiuliza hii miradi tukifua tilia mnatauhidi hapa kwamba mradi unaenda kuanzishwa. Leo mnasema Tarime Mji itapata maji baada ya Serikali kutafuta vyanzo vya ndani. Leo tunavyozungumza Tarime Mji chini ya asilimia 40 pia pamoja ni kwamba mijini hawana maji na haya maji yanatoka Ziwa Victoria tu, ambapo mngekuwa mnavuta pale Rarya wangefaidika Tarime pia ingefaidika.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri hapa; kwa sababu kuanzia mwanzo hii miji 28 ilikuwa inahesabika hizo fedha ambazo zina uhakika zinapatikana kuanzia Aprili mradi unaanza kutekelezeka ianze yote miji 28 wakati huo mkitafuta hivyo vyanzo vya ndani mtakuja ku-*supplement* huko mbele wakati miji hii 28 yote mmei-*take on board*, kinyume cha hapo kwa kweli hatutawaelewa, na mtabidi mtuambie ni vigezo vipi ambavyo mnatumia ambavyo vinakuwa na *bias*, yaani mmeefikia vigezo vipi ku-*arrive* kwamba Tarime isiwepo kati ya miji 24 ambayo mmeamua kuiweka lazima mtueleze

wananchi wa Tarime na hiyo miji mingine minne ambayo mmeamua kuiacha ni kwa nini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiangalia, nimejaribu kupitia jedwali la IIIA; Mheshimiwa Waziri ameainisha baadhi ya miradi ambayo inaenda kutekelezeka ya maji vijijini. Kuna mikoa inapewa zaidi mpaka bilioni 16. Kwa mfano Mkao wa Katavi bilioni 16, Kagera bilioni 14, nimeona Mwanza bilioni 13, Mara tunapewa bilioni 1.6 tu miradi ya vijijini. Nimerudia kusema hapa, nimepitia hiyo tatu A, Mara wanapata bilioni 1.6 miradi ya vijijini, majimbo yote 10, kweli! *Is this fair?* Mnatumia vigezo vipi wakati mnagawanya hizi rasimali za nchi kuhakikisha kwamba tunatatua matatizo katika mikoa yote au majimbo yote ambako tunajua kote kuna matatizo ya maji haya? Mnatumia vigezo vipi? Au ndiyo *biasness* Mara nayo muinyime hela Tarime muiondoe mradi wa maji na Rarya, ambayo ingefaidika yani mnatumia vigezo vipi ni kwa nini wanakuwa wanabagua.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji. Tumekuwa tukishuhudia kuwa vyanzo vya asili vya maji havitunzwi. Mfano Mto Mara ambao unasaidia vijiji kadhaa na kata kadhaa; vijiji vya Korurya Kibusyo kule tunasaidika, lakini vyanzo hivi havitunzwi, Serikali pia hajajenga hata basi visima vya kuweza kusaidia. Wale walioenda kufanya utafiti walisema wakati wanaangalia haya maji, walikuwa wanatembea zaidi ya KM 30 wanakutana na *source* ya maji, sasa yale maji yakichafuka pale hawa wananchi wanakuwa hawapi *alternative* ya maji ya kutumia. Sasa tunashindwa kuweka maji ya muda mfupi ya visima, tunashindwa kuchimba mabwawa tunashindwa pia hata kutunza haya maji ambayo Watanzania wanaendelea kutumia wakati huo tukijikongoja kuweza kuwasaidia kupatia maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa nashauri Serikali iweze kuangalia vyanzo vya asili ambavyo tunavyo, ivitunze wakati huo ikitafuta mbadala wa kuhakikisha kwamba inapeleka maji, tena miradi ya muda mrefu kutoka Ziwa Tanganyika, Victoria. Tuamue na tu-*prioritize once and for*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

*all; kwamba tunaamua kujenga miundo mbinu ya maji tutatue matatizo ya maji kwa Watanzania. Kama vile ambavyo tumeamua kuwekeza kwenye Wizara ya Uchukuzi na Ujenzi hata hapa tuweke *trillions of money* ili tuhakikishe kwamba tunachukuwa maji kutoka sources zote ili kuwezesha Watanzania kupata maji.*

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa na maji safi na salama Watanzania wanaugua, nchi inapata hasara kwa kuwatibu hawa Watanzania ambao wanaugua kwa sababu hatuna maji safi na salama; lakini pia Watanzania wanashindwa kufanya kazi za kuzalisha uchumi wakitembea kutafuta maji. Kwahiylo hii Wizara tuipe kipaumbele cha dhati, fedha zitengwe za kimkakati hii miradi mikubwa mikubwa yote iahakikishe imejengeka ndani ya muda mfupi ili ile hata ilani yenu ya CCM ambayo mmeisema 2025 muweze kuwa mmeifikisha asilimla 95, 85 iweze kuflikika, vinginevyo inakuwa hatufanyii chochote kile.

Mheshimiwa Spika, mwisho nikuhusiana na maji taka...nitaliandikia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

SPIKA: Haya ahsante Mheshimiwa Esther Matiko Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea utafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasamu Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi ajiandae.

MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kabla sijaongea vitu vyangu vyaya jumboni naona Mheshimiwa Esther mchango wake uliopita amegusia kidogo kitu ambacho nilitaka kushauri Wizara. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesisitiza na wakaonesha kama upo uwezekano wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Dodoma; kwa ajili gani tusifikirie kuchukuwa maji kwenye vyanzo vyote vikubwa nchi hii tukavisambaza nchi nzima? Kwa ajili gani tuendelee na vyanzo vidogo vidogo ambavyo havina uhakika nilikaa chini nyumbani

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwenyewe nikaanza kufirika na kupiga mahesabu? Nikahisi tufanye kitu kimoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba hili ulichukuwe Katibu Mkuu wetu yupo aandike hiki kitu ninachotaka kukishauri Serikali Mheshimiwa Waziri naomba uandike kaka yangu tukae chini tutengeneza *business proposal*/kiasi gani kitatu-*cost*/kuchukuwa maji kutoka vyanzo vyote vikubwa nchi hii, kusambaza nchi nzima kiasi gani kitatutosha kutengeneza *treatment plant* ambazo zitatosha nchi nzima na kiwango gani cha pesa kitaweza kusambaza mabomba nchi nzima kumaliza ili tatizo kwa wakati mmoja (*at once*)?

Mheshimiwa Spika, nafahamu hatuna fedha hizo, lakini *business proposal*/hiyo i-identify *source of fund*, twende tukakope. Nina imani kabisa tukikopa fedha hizo namba moja tutaweza ku-repay ule mkopo kwa kuwa watu watakuwa nchi nzima wanalipa bili za maji na *revenue* kutoka kwenye maji zitaongezeka, nimepiga mahesabu zitaongezeka mara tano.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa hapa kuna upotevu wa maji asilimia 30 mpaka 45. Kwenye huo mfumo mpya ninaamini kabisa tutakuwa na upotevu wa maji chini ya asilimia 10, kana kwamba tutaweza kuokoa *revenue* tutaweza kulipa mkopo huo.

Mheshimiwa Spika, nimepiga mahesabu, kwa mfano mwaka huu tumetenga milioni 700. Nina imini bajeti ya Wizara ya Maji kuanzia kipindi hicho ambacho kila Mtanzania atakuwa na maji tutatumia sasa hiyo bajeti ya maji kulipa mkopo na tutakuwa tumeondoa tatizo la maji kabisa nchi hii, na inawezekana Mheshimiwa Waziri. Mimi niko tayari kama utanihitaji. Unafahamu mimi ni mtalaam wa masuala ya fedha, nitashirikiana na wewe au wataalam wengine wa Wizara yako tuweze kutengeneza hiyo *business proposal*, tuiuze ili tutatue tatizo la maji nchi nzima kwa wakati mmoja. Nakushukuru sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi jimboni kwangu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa miradi mikubwa ambayo ameileta jimboni kwangu. nimshukuru Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kipindi kifupi ambacho ni Mbunge umenipatia milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa maji kwenye Kata ya Bagamoyo, umenipatia fedha kwa ajili ya kumalizia ule mradi ambao unaitwa chechefu wa Longela Relini na Darajani na mwezi huu maji yatatoka. Pia mradi ambao una thamani wa 1.6 *bilion* uko kwenye hatua za manunuzi tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado zipo changamoto chache kwenye Kata ya Kwamsisi, maji yapo lakini ya chumvi Kata ya Manundu Majengo mabomba ni chakavu sana ni yale mabomba ya chuma ambayo yametengezwa tangu mwaka 70; ni chakavu yanavujisha maji sana mjini watu wanakosa maji. Kwenye Kata za Masuguru, Magunga, Mtonga *Road* Korogwe Mgombezi na kwa Mndolwa wanapata maji kwa shida sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ninafahamu, ni imani yangu, na ni imani ya watu wote wa Korogwe kwamba huu Mradi wa Miji 28 ambao ulioasisiwa miaka nane iliyopita nakumbuka kwenye jumbo langu Mbunge alikuwa kaka yangu Nasri; lakini leo baada ya miaka nane tunaenda kuufanya kazi mradi huo. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pia nimshukuru Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutuhakikisha mradi huo unafanyika.

Mheshimiwa Spika, imani yetu, imani ya watu wa Korogwe, tunaamini mradi huo utaleta maji Korogwe, utaenda kutengeneza matenki sehemu zote zinazohitajika kupelekwa maji, utasambaza mabomba kwenye kata zote na vitongozji vyote na mitaa ya mji wetu. Ninaamini pia mradi huu utatengeneza vizimba vya kuchotea maji kwa wale wananchi wetu ambao hawana uwezo wa kuvuta maji nyumbani mwao.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumeambiwa mradi huu utatuletea tu maji kusambaza tutajua wenyewe lakini ndugu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yangu juzi umenihakikishia, kwamba mdogo wangu si kweli mradi utaleta maji Korogwe na utasambaza na kihistoria ya changamoto ya maji Korogwe itakuwa imeishia hapo. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana, nilikuwa na hayo mawili machache nataka kuunga mkono hoja, Mungu akubariki sana endelea kuchapa kazi na kupambana sisi ndugu zako tuko nyuma yako. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi mtoa hoja ajiandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa Aweso kwa kule Mwanza sisi wewe ni bado *green guard* tu, lakini maskini wa Mungu sasa umezeeka, yani unaota upara kwa ajili ya maji, lakini Mungu atakulipa. Dada yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mungu atawalipa; kazi ya maji ni sadaka. Msione Wabunge humu ndani wanalia maji, Mheshimiwa Rais yeye mwenye anajua kabisa kazi anayokuja kufanya ni sadaka kwa wananchi wa Tanzania na Mwenyezi Mungu atamlipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi kwetu katika Mkoa wa Mwanza hakuna mahali popote ambapo haufanyiki mradi wa maji. Magu kuna mradi mkubwa wa zaidi ya mabilioni, ambao unakamilika sasa hivi; Misungwi kuna mradi wa bilioni 45; sasa hivi hapa tunapiga hesabu mradi wa Majimbo ya Sumve na Kwimba pekee yake tu wana bilioni 41; Sengerema mimi hapa sasa hivi katika miradi iliopo kuna mradi mkubwa wa bilioni 21 na sasa hivi kuna mradi wa bilioni 17, huyu mama tunataka tumpe nini? Na bado anahikikisha tena tunapata mitambo 25 kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ninachoshauri tu ni kwamba hii mitambo Mheshimiwa Waziri Aweso muhakikishe

wataalam wanaokwenda kuihudumia mitambo hii tusije tukashindwa kufika 2025 hatujamaliza kero ya maji kwa nchi hii; hakuna mtu ambaye atakosa maji. Hawa wanaosema wanakosa maji kutoka Ziwa Victoria kuna mitambo itachimba.

Mheshimiwa Spika, na mimi ninachotaka kukuambia ni kwamba badala ya kuigawa hii mitambo kwa mikoa, iende kwenye kanda ili tufanya kazi kwa pamoja. Wilaya moja inaweza ikashambuliwa na mitambo mitatu au minne ionekane kazi ya Mheshimiwa Rais. Haya ndiyo maono yake, yaonekane kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hakuna mbadala wa maji kama unavyosema. Na hii Wizara yako mara nyingi nakusikia unasema siyo Wizara ya ukame, na mama ameshatuhakikishla kwamba suala la maji katika nchi hii litakuwa historia. Waheshimiwa Wabunge, kubalini mipango Mheshimiwa Rais anayoifanya sasa hivi kuititia Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso, ushauri wangu ni kwamba kwa kutumia magari haya ambayo uyatumia sasa hivi kuendelea na safari, kutembea nchi nzima unaweza ukachoka kuiflikia miradi yote kuikagua. Sasa hivi duniani watu wanakwenda katika mabadiliko. Gharama za kutumia helikopta Watanzania wanatakiwa waambiwe; kutumia helikopta ni gharama ndogo sana, mafuta lita 400 ukitoka na *jet* kutoka Dar es salaam unaweza ukakagua miradi 10 mpaka kufika Sengerema.

Mheshimiwa Spika, mnashindwaje idara kama hii, Wizara ya Maji mna miradi mikubwa ya mabilioni, kutoa pesa bilioni moja na nusu mkanunue helikopta. Na unakagua miradi yote kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nimekuona juzi unaangalia bwawa unadaganywa bwawa lilikuwa hapa; bwawa linaweza likapotea? Hawa watu wengi wanakuwa sio waadilifu. Sasa unakuja kuambiwa kwamba mara paipu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zilipaa. Paipu zinaweza kupaa namna gani zimechimbiwa chini? Sasa hii yote ni kwa sababu unachelewa kufika katika yale maeneo. Jitahidi Mheshimiwa Aweso, wewe ni mdogo wangu, na Mwenyezi Mungu atakulinda na sisi tunakuombea dua.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu, ninachotaka kuwaambia ni kwamba kazi ya kusimamia miradi hii ya Serikali siyo mchezo. Hii miradi ya maji ni mingi sana katika nchi hii. Tuwe waadilifu, sisi wenyewe Wabunge twende tuka-*visit* hii miradi, tuisubiri kuja kulaumu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, tuchukuwe majukumu yetu. Wabunge tuchukukuwe majukumu yetu jamani, tuhakikishe tunamsaidia Waziri kutoa taarifa. Na bahati nzuri ile Wizara yake nimekwenda kule mara nne, unafika unapewa chai unapewa na korosho.

Juzi nilipewa korosho nikashangaa mimi, nimekwenda na shida ya maji nikapewa korosho na kukaribishwa chai, nikapewa na maji ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ma-*tank* Sengerema, nakushukuru sana. Umeweka *tank* Sengerema lita milioni 5; siyo mchezo. Tunaweka kwenye chanzo cha Nyamazugo, Nyamkurukano kuna lita kama milioni mbili; haya maji yaliyoko Sengerema yanaweza yakatosha kuilisha Geita, Boshosa na kila mahali tukamaliza miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso, karibu Sengerema, dada yangu karibu Sengerema, mmekuja mmeona ile hali iliyopo, endeleeni kuwa waadilifu na Mwenyezi Mungu atawalinda.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu Sanga, najua unafanya kazi kwa niaba ya nchi. Unatoka hapo *DUWASA*, mimi nakukuta pale mpaka saa sita za usiku, mimi nipo jirani pale Sanga, Mwenyezi Mungu atakulipa. Hii kazi ni ya sadaka, wananchi wanakuona wala usiwe na wasiwasi. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, na wakati mwingine hawa watu wawe wanapewa hata zawadi hapa Bungeni kwa kazi wanayofanya ya maji. Lakini Mheshimiwa Rais tumuombee kwa Mwenyezi Mungu; Wabunge hapa tumuombee, kazi ya maji siyo mchezo katika nchi hii. Tusiwe tunalaumu tu muda wote.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni kubwa, hii nchi siyo ndogo kama Burundi au Rwanda hapana. Kuna wananchi zaidi ya milioni 60 wote wanataka maji; siyo mchezo. Mheshimiwa Aweso, endelea tu kutusikiliza hivyo hivyo, lakini tunalia kwako na miradi yetu iweze kwenda. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na Viongozi wote wa Wizara ya Maji, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maji kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa Kimataifa (*national competitiveness*). Bajeti hii inaenda sambamba na dhima

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni *Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya bajeti ya mwaka 2021/2022, Serikali kuititia Wizara ya Maji imetekeleza miradi mingi ya maji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya inatekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya vijiji vya Ruanda, Illembo, Inyala, Igoma, Iwalanje, Galijembe, Tembela, Pashungu, Shigamba, Santilya, Inyala Illembo, Mshewe, Muvwa, Njelenje, Mapogoro, Mjele, Chang'ombe, Iwizi, Ikukwa, Simboya, Itimba, Utengule, Ihombe, Idugumbi, Iwala, Ilota, Ikhoho na pia mradi mkubwa katika Mji Mdogo wa Mbalizi. Miradi yote hiyo imetekelezwa kwa ufanisi mkubwa, ingawa kunahitajika uboreshaji wa miundombinu ya mabomba hasa katika mradi wa Mbalizi kuna upotevu mkubwa wa maji kutokana na uchakavu wa mabomba yaliyokuwepo awali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya bado kuna changamoto kubwa ya maji salama kwa wananchi. Pamoja na kuwepo kwa vyanzo vingi vya mseleleko (*gravity*), asilimia kubwa ya vijiji havina maji salama. Nashukuru kwa kuwepo bajeti ya *mradi mkubwa wa Mto Kiwira* ambao utakuwa mkombozi wa maeneo mengi ya Mkoa wa Mbeya na hata Songwe. Napendekeza Serikali iendelee kutekeleza miradi ya maji kwa mpango wa *force account* ambao umeonesha mafanikio ya kupunguza gharama za miradi na pia utekelezaji ni wa haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iweke msukumo mkubwa wa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliyomo kwenye mradi wa Bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Development Programme - SRBDP*), wenyе ofisi zake Kyela, Tanzania. Mradi huu unaotekeliza kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Malawi ni muhimu sana kwa sasa kutokana hasa na ujenzi wa mabwawa ambayo pamoja na manufaa mengine, yatasaidia kupunguza mafuriko ya Bonde la Kyela. Mabwawa haya yamelenga kuzalisha umeme,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na hata utalii ambao unahitajika sana katika Wilaya ya Mbeya na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za tabianchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji mkaa na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo wa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Kama ilivyo kwa athari za mafuriko ya Kyela, hata Ziwa Rukwa linaathirika sana na kujaa mchanga na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya na kuhakikisha anawatua kina mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na timu yake yote kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya, kwa hakika Mwenyezi Mungu atawalipa.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika ya kuwa maji hayana mbadala, naishukuru Serikali imenipa miradi ya maji yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili, lakini kama unavyojua changamoto ya maji bado ni kubwa sana katika jimbo la Lushoto na naomba niorodheshe maeneo yenye changamoto; Kata ya Gare, Kata ya Kwai, Kata ya Migambo, Kata ya Malibwi, Kata ya Ubiri, Kata ya Ngulwi, Kata ya Kwekanga na Kata ya Makanya.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kata hizi zote nilizoorodhesha hapo juu hazina mradi hata mmoja na zina hali mbaya sana kwa wananchi kukosa maji safi na salama. Kwa hiyo niiombe Serikali katika bajeti hii iangalie kwa jicho la huruma ili tuweze kuokoa maisha ya wananchi wanaoishi katika kata hizo hasa kina mama, wao ndiyo waathirika wakubwa wa huduma hii maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na baadhi ya kata ambazo zina miradi ya maji lakini bado kuna uhitaji mkubwa wa maji, kwani wananchi ni wengi kuliko upatikanaji wa maji yenye, kata hizo ni hizi zifuatazo; Kata ya Lushoto, Kata ya Mlola, Kata ya Kilole, Kata ya Kwemashai, Kata ya Mbwei na. Kata ya Magamba.

Mheshimiwa Spika, Kata hizi zina miradi kama nillivyosema, lakini bado mahitaji ni makubwa sana, kwa hiyo niiombe Serikali iongeze miradi katika kata hizi ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niishauri Serikali yangu tukufu, Jimbo la Lushoto lina vyanzo vingi nya maji, lakini katika vyanzo hivyo kuna chanzo ambacho kina sifa zote yaani hakikauki hata wakati wa kiangazi, lakini pia ni chanzo chenye maji mengi, safi na salama na chanzo hicho kipo kileleni, hivyo basi kinawenza kupeleka maji kwenye kata 13 kati ya kata 15 za Jimbo la Lushoto, na chanzo hicho kikifanyiwa kazi na kwa kuwa kipo juu, maji yake hayatahitaji *pump*, ila maji yake yatakuwa ya mserereko mpaka yafike kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, chanzo hicho kipo katika Kata ya Magamba eneo la chanzo linaitwa, Mstari Namba Tisa na mradi huu ukitekelezeka utakuwa ndiyo suluhisho la kudumu katika Jimbo la Lushoto. Kwa hiyo niiombe Serikali itumie chanzo hiki ili kuondoa kero ya maji katika Jimbo la Lushoto na ile dhana nzima ya Rais wetu pamoja na Waziri ya kumtua mama ndoo kichwani itakuwa imetekelvezeka kwa vitendo pamoja na kumaliza tatizo la maji safi na salama na yenye kutosheleza kwa wananchi wa Lushoto.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii ya Maji kwa asilimia mia moja.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuwapongeza kwa mtiririko na mpangilio mzuri wa hotuba ya bajeti hasa katika viambatisho vinavyoonesha miradi iliyokamilika, inayotekelawa na ile ambayo itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, aidha nawashukuru kwamba baada ya mkandarasi wa kwanza wa kuchimba visima katika Viji^ji vya Itimbo na Matanana kutokomea, leo kwa maelekezo ya juzi ya Waziri Mheshimiwa Aweso na Katibu Mkuu *Engineer Sanga*, magari ya kuchimba visima yamewasili leo tarehe 12 Mei, 2022 katika Kijiji cha Matanana na baadae wataenda Itimbo.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha maombi kwenu, kwamba baada ya kuchimba na kwa kurejea mazungumzo yetu kwamba Mafinga *as of now* ukiacha mradi wa UVIKO katika Kijiji cha Ulole, hakuna mradi ambao unatekelezwa au umetekelezwa. Utakumbuka hata Mradi wa Viji^ji vya Ugute na Ulete wanasema vilikuwa vimesahaulika, mmetumia neno *oversight*. Kwa sababu hiyo, naomba mtusaidie baada ya kuchimba visima hivi vya Matanana na Itimbo, *design ifuaties* ili tukamilishe katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kifupi ninaomba mradi au mwendelezo uingie katika bajeti hii tunayoipitisha sasa. Mkitusaidia maana yake tutakuwa tumemaliza viji^ji hivi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili; baada ya mazungumzo yetu katika Kikao (Mheshimiwa Aweso, Mheshimiwa Chumi, Katibu Mkuu - *Engineer Sanga*, Ndugu Bwire na *RM Joyce*), nilifahamishwa kwamba kwa kuwa kulikuwa na jana nashukuru sana kupitia Ndugu Bwire nimefahamishwa kuwa tangazo la *tendertayari*. Hata hivyo, katika kitabu chenu viji^ji hivi viwili vya Ugute na Ulete havipo, ninapata shaka kuwa isije ikafika wakati wa utekelezaji ikaonekana viji^ji havipo katika kitabu cha bajeti, hivyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nashauri izingatiwe ili vijiji hivi ambavyo kimsingi ni mwendelezo wa miradi ya mwaka huu wa fedha wa 2021/2022 viweze kuwa *reflected* kwenye kitabu cha bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ombi la gari; nafahamu kwamba kuna uhaba mkubwa wa magari, hata hivyo ninaomba kwa jicho la kipekee, mtusaidie kupata gari la uhakika ambalo litaweza kusaidia *RUWASA* na *MAUWASA*, kwa sasa gari la *RUWASA* Mufindi ni kuukuu na *MAUWASA* hakuna gari kabisa. Kwa kasi ya ukuaji wa Mji wa Mafinga ikiwa ni pamoja na viwanda vya mazao ya misitu na vijiji vinavyozunguka, upo umuhimu mkubwa sana kutusaidia kupata gari.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa dhati ya moyo wangu nawapongeza sana kwa namna ambavyo miradi inafuatiliwa kwa ukaribu na ushirikishwaji sisi Wabunge, walau sasa miradi inafanyika kwa *speed*, naamini hata Mradi wa Miji 28 utatekelezwa kwa *speed* na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa hongera kwa utekelezaji wa majukumu yao na nashauri yafuatayo:-

Kwanza *pump* kwa ajili ya Mradi wa Kazilankanda, Wilayani Ukerewe ni suluhisho la changamoto ya maji vijiji. Kupitia pesa za UVIKO tulikubaliana na *MD RUWASA* sehemu ya pesa hizo kununua *pump* mpya lakini jambo hili limechukua muda mrefu. Naomba *pump* hii ipatikane mapema kuondoa adha ya maji Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu Mradi wa Maji Mjini Nansio, pamoja na jitihada kubwa zinazoendelea, lakini bado wananchi wengi Mjini Nansio hawana maji kutohana na gherama kubwa za kuunganisha maji.

Nashauri Wizara kuikopesha mamlaka iweze kusogeza maji maeneo ya jirani halafu wananchi wakiunganishiwa basi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mamlaka iweze kurejesha pesa hizo. Hii itasaidia jamii kupata maji safi na salama.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza Taifa letu kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Maji pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya katika sekta hii ya maji. Pia naipongeza Wizara kwa miradi mikubwa ya maji katika Jimbo la Babati Vijiji ni hasa miradi ya Darakuta - Magugu hadi Mwada; Mradi wa Mayoka - Minjingu, Vilima Vitatu, Madunga na maeneo mengine. Fedha za UVICO zimesaidia mradi wa maji wa Bashnet na Secheda.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya mradi wa maji wa Darakuta-Magugu-Mwada hadi Minjingu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Dareda; mradi mkubwa wa Ziwa Manyara ambao utahudumia kata zote za Tarafa ya Bashnet.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Kata za Gidas, Duru, Riroda na Endadosh na Ayasanda.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza tena Wizara hii kwa kazi nzuri na naunga mkono hoja.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa kuwatumikia Watanzania.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Pia niwapongeze Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa makao makuu ya Wizara ya Maji pamoja na *RUWASA* kwani wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwapongeze *Engineer* Walter, Meneja wa *RUWASA* Mkoa wa Manyara na *Engineer* Idd Msuya - Mkurugenzi Mtendaji wa *BAWASA*, wanafanya kazi nzuri sana. Naomba sana watumishi hawa waendelee kutusaidia ili kukamilisha miradi inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutupatia fedha kwa ajili ya maji ya mji wa Katesh wa shillingi 2,300,000,000 ambapo mabomba yameanza kupokelewa ili kusambaza maji, pia mradi wa maji Gehandu na visima 24 ambavyo vinaendelea kuchimbwa kwa fedha za mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani nilizotoa hapo juu Wilaya ya Hanang ni kubwa, ina kata 33, vijiji 96 na maeneo mengi hayana maji, naomba mtuangalie kwa jicho la kipekee kwa kukamilisha miradi inayoendelea ya Ziwa Bassotu (mradi wa vijiji 12), mradi wa Gehandu; pia miradi mpya ifanyiwe usanifu kwenye chanzo cha Mto Duru-Masakta, maji ya Bwawa Bassotughang iliyopo kijiji cha Bassotughang, kata ya Hidet ili yatumike kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaimani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri na timu yake, ila atusaidie Wilaya ya Hanang kwani Meneja wa Wilaya tuliyanaye kweli hafanyi vizuri na Mheshimiwa Waziri alipokuwa Kongwa alitamka kumfukuza kazi na analalamikiwa sana kwa kufanya kazi chini ya kiwango. Hivyo ili meneja huyu asiharibu kazi nzuri inayofanywa na Serikali apangiwe majukumu mengine atakayomudu vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu naomba kuunga mkono hoja.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mungu, kwa zawadi ya uhai na amani katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa juhudzi za kumtua mwanamke ndoo kichwani, na ninahimiza kazi iendelee. Pia pungezi kwa Waziri Mheshimiwa Aweso na timu yake yote, kwa utekelezaji wa viwango vya hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kufikisha kilio cha wananchi wa Same, Mkoani Kilimanjaro. Mradi wa kimkakati wa Mwanga, Same, Korogwe umekuwa hadithi ya abunuasi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha aseme neno moja tu kuhusu mradi ya hapo juu na roho za wananchi husika hapo juu zitapata amani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Pili, naungana na wezangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimae kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na hali ya upatikanaji wa maji vijijini; napenda kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mikakati ya kumtua mama ndoo kichwani. Hili ni jambo zuri sana na la kupigwa mfano katika nchi yetu.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha kuwa upatikanaji wa maji vijijini unaongezeka kila mwaka. Mwaka 2021 hali ya maji vijijini ulikuwa asilimia 74.5, mwaka huu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

imepanda kwa asilimia mbili. Naipongeza Serikali yetu kwa rekodi hii ya manufaa kwa wananchi.

Ushauri wangu katika upatikanaji wa maji vijiji ni kuendelea kuwasogezea vyanzo vya maji karibu na maeneo yao ili kuwapunguzia masafa marefu ya kufuutilia maji kwa matumizi yao.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji; vyanzo vyetu vya maji vinahitaji kuhifadhiwa sana. Vyanzo vingi vya maji viko katika hali ya kuweza kuhatarisha maisha ya wananchi. Utakuta chanzo cha maji hakina uzio wa kukihifadhi, wanyama wanaweza kuingia kwenye chanzo cha maji na kuhatarisha maisha. Aidha, kutokana hali ya dunia sasa hivi watu ambao si wazuri wasiopenda maendeleo inakuwa ni rahisi kuweza kufanya uharibifu wa chanzo cha maji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuendelea kuchukua hadhari ya kuviwekea uzio vyanzo vote vya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vibali vya kuchimba maji; naipongeza Wizara ya Maji kwa kuweka utaratibu huu wa kuruhusu wananchi kuchimba visima vyao kwa matumizi yao binafsi. Hili ni jambo zuri sana litaisaidia Wizara kwa sehemu kubwa.

Ushauri wangu katika jambo hili ni kuweka udhibiti kwa kuwapa maelekezo ya kitaalam namna ya kuchimba visima hivyo ili kuepuka hatari ya miripuko ya maradhi yanayotokana na maji yasiokuwa salama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote, kwani tunajivunia kwa jinsi alivyotuvusha kwenye majanga mbalimbali kwa mfano corona na ustawi katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyanja za kisasa, kiuchumi, kidplomasia, kisasa, amani, mshikamano wetu kitaifa, hongera sana mama.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Mbulu Mjini kutoa pongozi nydingi sana kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kwa jinsi anavyoiongoza nchi yetu na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM yam waka 2020/2025.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara na Mheshimiwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi mnavyoitendea haki Wizara hii kwanza kutusikiliza sisi wawakilishi wa wananchi na kutatua tatizo la maji kwa nchi nzima, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya Wizara hii, Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako nzima naomba kukueleza masikitiko yangu kwa kuwa katika mpango wa bajeti mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Mji wa Mbulu ilikuwa mionganoni mwa miji itakayonufaika na mradi wa miji 28. Binafsi mimi nasikitika kwa sababu hata wakati tunaondolewa mimi kama mwakilishi wa wananchi sijashirikishwa, wakati Jimbo la Mbulu Mjini kuna kama 17 kata 10 eneo la vijiji 34 na kama saba yenye mitaa 58, hadi sasa ni kisima kimoja tu cha Bargish Antsi kilichimbwa 2016/2020. Hivyo basi kupitia kauli yako ya wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani. Tunaomba mturudishe kwenye miradi ya P4Rkutokana na eneo hilo la vijiji 34 na kutuongezea fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tuliwasilisha maombi yetu ya nyongeza ya fedha za miradi kutoka milioni 700 mpaka billioni 1.5 lakini kiasi hicho hakipo kwenye mapendekezo bajeti ya mwaka 2022/2023 na *documenthizo* ninazo kwenye *tablet* yangu. Ninapata wakati mgumu sana kushika shilingi yako, hivyo kwa heshima kubwa ninakuomba mdogo wangu kaa na timu yako kuona njia mbadala ya kunusuru hali hii, chonde chonde.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara yetu hii iagize makusanyo ya mapato ya bili za maji katika maeneo yote ambayo tayari kuna *DPS* za maji nchini kwani hali hii itasaidia kudhibiti upotevu wa fedha za mauzo ya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji itazame utaratibu wa mapendekezo ya majina ya bodi za maji kwani kwa sasa mchakato wa wajumbe wawili wa bodi mpya kwa kila nafasi kwenye ngazi za Kata, Baraza la Madiwani na baada ya hapo Meneja wa *RUWASA* ngazi hiyo kuwasilisha ngazi ya Mkoa na Wizara kwa ajili ya kupata wajumbe mahiri katika kusimamia utoaji wa huduma bora za maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuwasilisha na naunga hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Mdunduwalo, Kata ya Maposeni hawajawahi kupata maji toka wapate Uhuru. Kijiji hiki watu hutumia maji ya kisima na wana-share na vyura na mijusi. Naomba Serikali mwaka huu wamalize adha hiyo.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mbunge na Waziri wa Maji na Naibu wake Mhandisi Maryprisca Mahundi, Mbunge kwa kazi nzuri ya kuwashudumia wananchi kupitia Wizara wanayolongoza.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga na Naibu wake Mhandisi Nadhifa Kemikimba pamoja na watendaji wote wa Wizara akiwemo kijana mdogo *Engineer* Maduhu anayekaimu Wilaya yangu ya Nyasa.

Nawashukuru kwa miradi ya maji inayoendelea jimboni kwangu, hata hivyo nina maombi yafuatayo; kwanza ni kuhusu ukanda wa chini (mwambao wa Ziwa); Wilaya yangu ina milima na ni kubwa sana. Gari iliyopo ni chakavu sana. Tunaomba gari ili kufuatilia vizuri utekelezaji wa miradi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Pili, kutatua kero ya changamoto ya maji, utekelezwe mradi wa Ngumbo na Liwundi, kukarabati mradi wa Kihagara, kuongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Mbamba Bay na vijiji vyake.

Mheshimiwa Spika, tatu, kupeleka maji kijiji cha Mtupale hadi Chiwindi.

Kwa upande wa ikanda wa juu; kupeleka maji Kijiji cha Malayalam, Kimbango, Litindo Asili na Luhangalasi (Kata ya Luhangalasi); kupeleka maji Kijiji cha Luhindo; kupeleka maji Kijiji cha Uhuru na Mipotopoto na kupeleka maji Kijiji cha Mitomoni.

Mheshimiwa Spika, tunasisitiza matumizi ya maji ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru na naomba kuwasilisha.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi katika Wizara hii muhimu sana kwa maisha ya wananchi wangu wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuhakikisha anakwenda kumtua ndoo mama kichwani. Katika mwaka mmoja sasa Mheshimiwa Rais ameonesha njia nzuri ya jinsi ya kupambana na kutatua changamoto ya maji katika nchi yetu na sisi kama wawakilishi wa wanawake tutaendelee kumpatia ushirikiano wa dhati ili kutimiza azma yake ya kuwatua ndoo kinamama wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Juma Aweso, Waziri wa Maji kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha huduma ya maji inapatikana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, lakini nimpongeze Mheshimiwa Katibu Mkuu wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wizara ya Maji kwa kazi kubwa wanayoifanya, ukweli kazi inafanyika na inaonekana. Pia nimpogezo Naibu Waziri mwanamama shupavu Mheshimiwa Maryprisca kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasaidia akinamama wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpogezo Mheshimiwa Waziri lakini bado kuna changamoto ndogo ndogo zilizopo katika Mkoa wa Katavi. Lengo la Serikali ni kufikisha maji kwa mijini asilimia 85 na vijijini kufikia asilimia 60, lakini kwa Mkoa wa Katavi bado ile azma ya Serikali bado hajafikia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha changamoto za maji katika Mkoa wa Katavi, kumekuwa na kukatikakatika kwa maji, inafikia hatua mwezi mzima maji hayapatika katika baadhi ya maeneo, lakini wananchi wamekuwa wakiletewa *bill* kubwa za maji na kubambikiwa *bill* za maji kutokana na mita kutokuwa za uhakika. Nashauri Mheshimiwa Waziri zifungwe mita za uhakika na ziwe na uwazi mkubwa ili wananchi wetu wawe na uelewa kusoma *bill* zao.

Mheshimiwa Spika, ilikutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Katavi lazima mradi wa ziwa tanganyika ufanyike kwa haraka ndio utakuwa mkombozi mkubwaa wa wananchi wa Mikoa Kigoma,wakatavi na Rukwa. Naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu kwa azma yake ya kumtua mama ndoo kichwani. Pili nampongezo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kujitoa kwao kuhakikisha miradi ya maji inakamilika tena kwa ubora kabisa.

Namuomba sana Waziri kuwachukulia hatua watendaji wasio waaminifu na wakandarasi hovyo hovyo ili kuhakikisha miradi ya maji inakamilika kwa wakati tena kwa ubora unaotakiwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, napongeza uamuzi wa Wizara kwa kutaka kuanza kutumia mita ya malipo ya awali, hili litaondoa malalamiko kwa wananchi kwa kubambakiziwa *bill* kubwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri vijiji na vitongoji vitakavyopitiwa na mabomba ya miradi ya maji basi navyo vipatiwe maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMINA DAUDI HASSAN: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi katika Wizara ya Maji ili kuhakikisha maji yanapatikana na kumtua mama ndoo kichwani katika kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Waziri wa Maji na Naibu wake kwa kuaminiwa na Rais kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuendeleza malengo ya Rais wetu kuwa wanahakikisha maji yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, mimi nijikite katika suala la uchimbaji wa mabwawa na visima nchini, naishauri Serikali iongeze fedha katika uchimbaji wa mabwawa na visima ili kutatua tatizo la maji katika maeneo ambayo hayana vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, lingine kuna maeneo ambayo maji yanaharibika kwa kuwa hakuna usimamizi katika maeneo ya vyanzo vya maji. Niiombe Serikali isimamie na kulinda maeneo hayo kwa kuweka walinzi ili kulinda maji ambayo ni uhai.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo nikianza na sualalal ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji. Kuna uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji nchini. Wizara imewe ka nguvu nyingi na fedha zaidi kwenye miundombinu na kuliacha suala la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa sekta nyingine hussusan za maliasili. Ni vyema kuanzisha uratibu na miradi ya pamoja na sekta za misitu ili kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji. Tuweke mikakati ya pamoja na sekta za kilimo, mifugo na misitu ili kizitafutia suluhisho la kudumu changamoto zinazotishia uendelevu wa vyanzo vya maji.

Pili ni kuhusu upotevu wa maji; tuongeze fedha zaidi kwa kushirikiana na TAMISEMI ili kukarabati miundombinu ya maji iliyochakaa. Aidha, tuendelee kutoa elimu kwa jamii kujenga tabia ya kutumia maji kwa nidhamu zaidi na kulinda miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu mabadiliko ya tabianchi sambamba na makazi holela inachangia sana upoteaji wa maji na uharibifu wa vyanzo vya maji. Tufanye kazi kwa karibu na sekta za misitu na ardhi ili kupanga makazi katika hali bora zaidi itakayozingatia uwepo na uendelevu wa vyanzo vya maji. Aidha, tuimarishe dawati la mazingira na mabadiliko ya tabianchi ili kuweza kupata ushauri na kuzingatia athari za mabadiliko ya tabianchi katika shughuli zote za sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji na ninaomba nianze kwa kumpogeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kumtua mama ndoo kichwani kwa kuipatia shilingi 709,361,607,000 kwa maendeleo ya miradi ya maji katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada kubwa za kuchimba visima maeneo oevu ili kuboresha hali ya upatikanaji wa maji. Ninaiomba Serikali iongeze fedha kuitia bajeti hii ili visima vingi vichimbwe nchini ili kuzidi kutatua changamoto ya maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina miradi mingi ya maji ambayo hajakamilika, niombe Serikali ikamilishe miradi yote

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambayo imeshaanza ili kuweza kuwatua akimama ndoo kichwani katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwa jitihada zake za kuhakikisha tatizo la maji linamalizika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, mradi wa maji kutoka Nungwe kwenda Mgodini *GGM*unatoa maji ghafi katika kata ya Nyamwilolelwu hususani Kijiji cha Kayenze, naiomba Wizara iyatibbu maji haya kabla ya kutumiwa na wananchi. *Please establish a treatment plant before human consumption.*

Mheshimiwa Spika, mradi unaoendelea wa kuleta maji katika miji midogo ya Katoro na Buselesele toka chanzo cha Chankorongo uongezewu kasi ya utekelezaji, lakini kutokana na ukuaji wa kasi wa miji hii Wizara iongeze pesa katika kupanua mtandao wa maji kila mwaka katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Busanda linayo miradi ya visima vya maji iliyo kwenye utekelezaji, niombe itakapokamilika tupate pesa ya mtandao wa maji kwenye vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *RM* na *DM* kwa ushirikiano wao kuhakikisha Jimbo la Busanda wananchi wanakunywa maji safi na salama.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunipa ari ya kuifanya kazi hii muhimu kwa ustawi wa nchi, pia nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajikita katika kusisitiza utekelezaji wa yale ambayo Wizara imejipangia. Lakini pia kuiomba kutoa kipaumbele kwenye maeneo yenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uhitaji mkubwa wa maji. Mkoa wa Mtwara ni mfano wa maeneo yenyé uhitaji mkubwa wa maji, mwaka jana Mheshimiwa Waziri alitembelea na kujionea yeye mwenyewe ambapo maeneo yote bei ya dumu la lita ishirini ilifika shilingi 2,500. Hali hii inajitokeza kila mwaka wakati wa kiangazi.

Naishauri Wizara kwamba Jimbo la Lulindi lina chanzo cha uhakika cha maji cha Mto Ruvuma, hivyo Mradi wa Mbangara - Mchoti naomba uwekewe pesa ya kutosha kwa sasa umepewa shilingi billioni 1.3 pekee licha ya kuwa ni mradi unaoweza kutatua changamoto ya maji kwa karibu ya nusu ya jimbo; Kata za Lupaso, Lipumburu, Sindano, Mchauru, Mpeta na Chiungutwa na maeneo hayo yako ndani ya kilometra 50 kutoka kwenye chanzo hivyo kuwa ni mradi mkubwa wenye tija unaoweza kutekelezwa kwa gharama ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Maji na nianze kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuititia Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya kuhakikisha anamtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika Wakala wa Maji Safi na Mazingira Vijiji (RUWASA); niongelee tatizo la maji katika Wilaya ya Same Jimbo la Same Mashariki katika Vijiji vya Maore, Kadando na Muheza. Vijiji hivi vimekuwa na tatizo la maji kwa muda mrefu sasa baada ya *intake* kusombwa na mafuriko ya mvua yaliyotokea Desemba, 2021. Mradi huu wa maji ulijengwa tangu mwaka 1967 idadi ya watu ikiwa ndogo sana, hivi sasa idadi ya watu imeongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ipeleke pesa za ujenzi wa *intake* na kukarabati miundombinu ambayo imekuwa chakavu kutokana na muda mrefu tangu ilivyojengwa.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia kuhusu uchimbaji wa visima nchini. Maji ni uhai; kutokana na kauli hiyo niipongeze Serikali kwa kuchimba visima vyta maji kwa maeneo ambayo hayana vyanzo vyta maji. Ni naishauri Serikali iongeze bajeti katika eneo hili la uchimbaji wa visima ili kupunguza changamoto ya maji na kuwafanya wanawake wafanye kazi za uzalishaji badala ya kutumia muda mwingi katika kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake wa kujitoa kuwatumikia Watanzania.

Pili, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa uzalendo wake wa kusimamia vizuri Wizara ya Maji kwa uwajibikaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kufikisha maji ya Ziwa Victoria pale Ushetu ni ya msingi sana kwa sababu utaalami umedhihirisha bayana kuwa Ushetu haina chanzo mbadala baada ya jitihada za kuchimba maji chini ya ardhi kushindikana.

Mheshimiwa Spika, suluhisho pekee la kutatua changamoto ya muda mrefu ya ukosefu wa maji kwa wananchi wa Ushetu ni maji ya Ziwa Victoria kutoka bomba la *KASHWASA* kuanzia Kahama. Kwa kuwa Serikali kuititia Wizara ya Maji tayari imefikisha maji ya Ziwa Victoria kuititia bomba la *KASHWASA* katika miji ya Ngudu - Kwimba, Muhunze - Kishapu, Kagongwa, Isaka, Nzega, Igunga na sasa maji yatafika Tinde, Shelui - Singida na Miji ya Sikunge na Urambo, hakuna sababu ya msingi ya maji ya *KASHWASA* kufika Ushetu ambapo kata ya kwanza kufaidi maji hayo ipo kilometra 12 tu kutoka bomba la *KASHWASA* ikilinganishwa na kilometra nyingi zilizojengwa kwenda maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu iundwe timu maalum ya wataalam wa ndani ikijumuisha *RUWASA* na *KASHWASA* ili ifanye tathmini na uchambuzi wa kina kuhusu mradi wa kufikisha maji Ushetu na kusanifu mradi kwa ujumla. Aidha, nashauri ujenzi wa mradi huo ufanye kwa *force account* kama ilivyofanyika katika miradi mingine mikubwa. Pia nashauri kama hali ya kifedha haitaruhusu kutekeleza mradi wote, ujenzi ufanywe kwa awamu ukianzia na kata ilio karibu na Kahama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama yetu mpendwa, mama msikivu na mwenye huruma Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi makini na uwazi wenyewe kujali maslahi ya wananchi, nampongeza sana.

Pia nampongeza sana Waziri wa Maji Mheshimiwa Juma Aweso, Naibu Waziri *Engineer Maryprisca Mahundi* na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na mafanikio yaliyopatika katika utekelezaji wa miradi ya maji katika mkoa wangu wa Singida bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama katika mkoa wangu wa Singida hususan maeneo ya vijijini na hii ni kwa sababu wananchi wengi wanatumia visima virefu na vifupi katika kupata maji kwa matumizi yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, jiografia ya mkoa wa Singida ni kame hivyo ni lazima kuwa na chanzo cha uhakika wa maji ambacho kitawezesha wananchi wa mkoa wa Singida na viunga vyake kupata maji safi na salama wakati wote kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uhakika, hivyo naiomba Serikali iangalie Mkoa wa Singida kwa jicho la kipekee katika suala zima la upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana mkakati wa Serikali wa kutoa maji kutoa chanzo cha Ziwa Victoria ambaao kwa sasa maji hayo yamefika Wilaya yangu ya Iramba katika Mji wa Shelui, naishukuru Serikali na kuipongeza sana lakini niiombe Serikali iyafikishe maji hayo Makao Makuu ya Wilaya ya Iramba, Mji wa Kiomboi ambaao una changamoto kubwa ya upatikanaji wa vyanzo vya maji endapo maji hayo yatafika Kiomboi itakuwa ni faraja kubwa kwa wananchi wa Vijiji vya Urughu, Mntenkente na Kizaga, lakini maji hayo pia yafike hadi Wilaya nyingine za Singida zikiwemo za Singida Vijijini, Mkalama, Ikungi, Singida Mjini na Manyoni ili ziweze kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni mradi wa visima ishirini kwa Wilaya ya Ikungi ambavyo kwa sasa vimekamilika lakini visima hivi havina miundombinu. Ombi langu kwa Wizara kwa kuwa visima hivi vimechimbwa kwenye vijiji na vijiji hivyo vina vitongoji ambavyo vipo mbali na sehemu kisima kilipochimbwa uwepo wa visima hivyo hautakuwa na maana endapo visima hivyo havitawekewa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana watendaji wa *RUWASA* ambaao wamekuwa wakifanya kazi nzuri katika mkoa wangu wa Singida. Nawapongeza sana lakini pamoja na pongezi hizo *RUWASA* Mkoa wa Singida inakabiliwa na uhaba mkubwa wa watumishi, kuna uhaba wa watumishi 42 pamoja na vitendea kazi, magari yaliyopo katika Wilaya zangu zote ni mabovu, ni gari moja tu ambalo ni zima. Je, kutakuwepo vipi na ufanisi wa utekelezaji endapo vitendea kazi muhimu kama magari hakuna? Hakutakuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ituongezee wataalam na vitendea kazi vya kutosha ili kazi za utekelezaji wa miradi ya maji hususan maeneo ya pembezoni ufanyike kwa ufanisi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Mkalama ipo miradi ambayo utekelezaji wake uliana mwaka 2014 lakini miradi hii mpaka leo hii haijakamilika na miradi ambayo imetumia fedha nyingi za walipakodi. Miradi hii ni mradi wa Gumanga wa vijiji vitano, mradi wa maji wa Nyaha ambao umetumia shilingi milioni 900 lakini nao haujakamilika, hapa niishauri Serikali nikiamini Serikali yangu ni sikivu, iundwe kamati kutoka Wizarani ili kubaini ni kwa nini miradi hii mpaka sasa haijakamilika? Pia ili kubaini nini changamoto ya kutokukamilika kwa miradi hiyo wakati wananchi wanaendelea kuteseka kwa kukosa huduma ya maji?

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuendelea kutenga fedha katika Mradi wa Maji Kintinku - Lusilile wa vijiji kumi na moja na kwa kuwa mradi huu ni wa muda mrefu na wananchi wamesubiri kwa muda mrefu kupata huduma hii muhimu ya maji na kwa kuwa maeneo ya kata ya Kintinku, Maweni na Makutopora maji yake ni ya magadi na hayafai kabisa kwa matumizi ya binadamu na kwa kuwa wananchi hutembea zaidi ya kilometra tano kufuata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, niiombe na kushauri Serikali itenye fedha za kutosha katika mradi huo ili umalizike na wananchi wafurahie uwepo wa Serikali yao ya Awamu ya Sita ambayo ni sikivu sana!

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi na naunga mkono hoja

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Juma Aweso na Naibu wake *Engineer Maryprisca Mahundi* pamoja na wataalamu wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, Waziri na timu yake wamekuwa mfano wa kuigwa kwenye kutatua changamoto za maji na kuwatua akinamama ndoo kichwani, kwani maji ni haki ya msingi kwa binadamu wote. Kwa ujumla, inatia faraja kuona upatikanaji wa maji vijijini unaongezeka, kama alivyoonesha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa kina katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka huu wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu la Moshi Vijiini kuna changamoto ya upatikanaji wa maji ya bomba katika maeneo yafuatayo; Kata ya Kibosho Kirima yenze vijiji vya Kirima Juu, Kirima Kati na Boro ina wakazi 10709 na kaya 2,332. Kata hii inahudumiwa na *RUWASA*. Miradi ya Maji ya Boro na Kirima ina changamoto kubwa ya upungufu wa maji kwenye mifumo. Upungufu huu umeleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi na taasisi zikiwemo Chuo Kikuu cha Kilutheri cha Masoka, shule za sekondari zenye mabweni (Kirima na Masoka), shule za msingi na taasisi za dini zilizopo kwenye kata.

Mheshimiwa Spika, kwenye taasisi hasa zile zenye mabweni, wanafunzi wameishia kutumia maji yasiyo salama kutoka miferejini na mtoni na kusababisha magonjwa mbalimbali ya tumbo na ngozi. Tunaishukuru Serikali kwa kutenga fedha za kuboresha mradi huu.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kata za Kibosho Kati na Okaoni zenyе jumla ya vijiji 14 zinahudumiwa na Mradi wa Maji Otaruni ambao ulijengwa miaka ya 1980. Eneo hili linahudumiwa na *RUWASA*. Kwa sasa watu wameongezeka sana na mifumo ya usambazaji maji imechakaa. Kwa hiyo, kuna uhitaji wa kuupanua na kuukarabati. Tunaishukuru Serikali kwa kutenga shilingi 200,000 katika mwaka huu wa fedha unaoishia ili kufanya ukarabati. Tunaomba Serikali iangalie miundombinu ya eneo hili kwa jicho la pekee na kuongeza bajeti ili mradi huu ukamilike.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya upatikanaji maji ya uhakika katika baadhi ya vijiji kumi vya kata ya Kibosho Magharibi. Vijiji hivyo ni Manushi Sindé, Manushi Ndoo, Mkomongo, Kifuni, Umbwe Onana, Umbwe Sindé, Manushi Sindé, Manushi Mashariki, Manushi Kati na Umbwe Kati. Kata hii ina wakazi 20,291 na baadhi ya maeneo haya yanaunganishwa na chanzo cha maji toka Jimbo la Hai,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwenye mradi wa Makeresho - Lyamungo - Umbwe na inahudumiwa na *RUWASA*.

Mheshimiwa Spika, maji ya mradi huu huelekezwa zaidi kwenye Jimbo la Hai. Ili kutatua kero hii, kuna umuhimu wa Wizara kutenga fedha za kusaidia kununua mambomba na kuunganisha wananchi wa maeneo haya na chanzo kingine cha maji kilicho karibu katika eneo la *Moshi DC* na kuachana na kile cha Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Spika, katika kata ya Mabogini kuna mradi unaoitwa mradi wa vijiji vitano; vijiji hivyo ni Muungano, Chekereni, Maendeleo, Mtakuja na Mserekia. Mradi huu umeanza na umekwishaombewa fedha na *MUWSA* na unangoja utekelezaji na kukamilisha.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine kubwa iko katika kijiji cha Mabogini. Tunaomba miradi hii ipewe kipaumbele, kwani wakazi wa Kata ya Mabogini ni wengi (28,992) na kuna changamoto kubwa ya maji ya kunywa. Hili ni eneo la kimkakati ambalo wahamiaji wengi toka mlimani wameanzisha makazi huko na hawana vyanzo mbadala vya maji. Tunashukuru kwa kupatiwa shilingi milioni 500 ili kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali itutengee pesa za kutosha ili maji yafike mpaka Remiti Umasaini kwani maeneo haya yana uhaba mkubwa wa maji. Tunashukuru kwa kupatiwa shilingi milioni 500 ili kutekeleza mradi huu. Tunashukuru kwa kupatiwa shilingi milioni 500 ili kutekeleza mradi huu. Tunaiomba Serikali itutengee pesa za kutosha ili maji yafike mpaka Remiti Umasaini kwani maeneo haya yana uhaba mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Old Moshi Mashariki, *MUWSA* ilikabidhiwa mradi wa maji ya kunywa wa Old Moshi Mashariki unaohudumia vijiji vinne vya Kikarara, Tsuduni, Mahoma na Kidia takribani miaka miwili iliyopita. Eneo hili lina wakazi wapatao 9,528. Tunaishukuru Serikali kwani wameanza kuweka mabomba ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hayajasambaa kata nzima. Tunaiomba Wizara iwawezeshe *MUWSA* wakamilishe huu mradi.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Uru Shimbwe yenye vijiji vya Shimbwe Juu na Shimbwe Chini, wananchi wana changamoto kubwa ya maji na wamejiongeza na kuanza kujenga miundombinu katika vyanzo vyao vya maji vilivyo mlimani kwa kutumia nguvu za wananchi. Kuna Mradi wa Maji Kimangara (kilometra nne) na mradi wa maji Mofuni (kilometra nne).

Mheshimiwa Spika, baada ya ujenzi, wana Shimbwe wanakabiliwa na changamoto ya mabomba ya kusafirisha maji kwenye kila mradi kwenda vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kimochi ina zaidi ya wakazi 13,000. Kata hii ina vijiji vya Mowo, Sango, Shla, Miami, Lyakombila na Kisaseni. Eneo lote linahudumiwa na *MUWSA*. Tunaishukuru Serikali kwa jitihada za awali kuwafikishia wakazi wa eneo hili maji. Ila bado kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji maji katika maeneo mengi hasa Kijiji cha Sango. Tunaiomba Serikali itutenggee pesa za kutosha ili maji yafike maeneo yote ya kata hii vikiwepo vijiji vya maeneo ya tambarare.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Uru Kusini yenye vijiji saba (Okaseni, Kimanganuni, Rua, Kariwa, Longuo A, Kitandu na Shinga) ina takribani wakazi 22,904 na ina miradi mitatu ya Mang'ana, Kisimeni na Mbora. Changamoto ya miradi hii ni maji kidogo katika mifumo ambayo hayatoshelezi na mara kwa mara huwa ni machafu sana. Hata ripoti ya Mkaguzi Mkuu yam waka huu imeeleza kwamba maji hayo hayafai kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Arusha Chini katika vijiji vya Mikocheni yenye wakazi 4,378 na Chemchem yenye wakazi 2,140 kuna uhaba wa maji. Sasa hivi ni watu wa Kirua Kahe wanatoa huduma ya maji ya kuza katika maeneo haya. Maji huuzwa kwa bei ya juu na si salama kwa matumizi ya binadamu. Kata hii inahudumiwa na *RUWASA*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kujenga mradi wa Ochai Ngoma katika Kata ya Uru Mashariki unaohudumia vijiji vinne kati ya saba, tenki liliopo ni dogo na halitoshelezi. Kuna umuhimu wa kujenga tenki kubwa la kuhifadhi maji ili lihudumie vijiji vyote saba (Materuni, Mruia, Mwasi Kaskazini, Kishumundu, Mwasi Kusini, Mnini na Kyaseni) yenye wakazi 14,78. Kata hii inahudumiwa na MUWSA.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Uru Kaskazini, MUWSA hajiatekeleza ahadi ya kuunganisha vijiji vya Msuni (wakazi 2,272) na Njari (wakazi 3,327). Chanzo cha maji haya kiko Uru Kaskazini na maji haya yamepita maeneo ya Uru Kaskazini na kwenda Kata ya Uru Kusini na Kata ya Pasua ya Jimbo la Moshi Mjini.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Old Moshi Magharibi kuna mradi wa maji wa Tela Mande ambao umekamilika. Mradi huu una maji mengi sana na ya ziada ambayo kwa sasa yanahudumia wananchi wa ukanda wa milimani. Vijiji na vitongoji vya kata hii vilivyopo ukanda wa tambarare kama kile cha Mandaka Mmono havina maji ya bomba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea changamoto zilizopo hapo juu, naishauri Wizara ya Maji itekeleze yafuatayo; kwanza naishauri Serikali itenye fedha za kutosha ili watafute na kujenga vyanzo vipya vya maji na kuyapeleka kwenye miundombinu ya miradi ya maji ya Boro na Kirima Kata ya Kibosho Kirima ili kutatua changamoto ya uhaba wa maji.

Mheshimiwa Spika, pili naishauri Serikali itenye fedha za kutosha kukarabati, kupanua na kujenga upya mradi uliopo katika Kata za Kibosho Kat i na Okaoni kwa kutumia vyanzo vilivyojengewa tokea miaka ya 1980.

Mheshimiwa Spika, tatu naishauri Serikali kupitia Wizara ya Maji itenye rasilimali pesa ya kutosha ili kujenga miundombinu mipyga kwa ajili wa wananchi wa Kata ya Kibosho Magharibi yenye vijiji 14 kwani maji kutoka mradi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Lyamungo - Umbwe kutoka Jimbo la Hai hayafiki kwa uhakika katika Jimbo la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nne, naishauri Serikali ipeleke fedha za kutosha kukamilisha mradi ulioanza na kuhakikisha maji yanafika Umasaini, eneo lenye uhaba mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, tano naishauri Serikali itenye rasilimali fedha ya kutosha kukamilisha mradi wa maji uliopo Kata ya Old Moshi Mashariki.

Mheshimiwa Spika, sita naishauri Serikali kuitia Wizara ya Maji isaidie juhudhi zilizoanzishwa na wananchi wa Kata ya Uru Shimbwe kwa kuwanunulia mabomba ya kusafirisha maji na kuyafikisha kweye vijiji vya Uru Shimbwe Juu na Chini.

Mheshimiwa Spika, saba naishauri Serikali kuitia Wizara ya Maji iwekeze vya kutosha na kuhakikisha wakazi wa Kata ya Kimochi wanapata maji ya kutosha kuanzia ukanda wa juu na tambarare.

Nane, naishauri Serikali kuitia Wizara ya Maji iwekeze na kutatua kero ya maji kidogo kwenye mifumo ya miradi na ile ya maji machafu iliyolalamikiwa katika kata ya uru kusini, kwani mkaguzi mkuu ameeleza hayafai kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, tisa ninaishauri Serikali iangalie kwa jicho la pili na kuwapatia maji wananchi wa vijiji vya Mikocheni na Chemchem vilivyoko Kata ya Arusha Chini.

Mheshimiwa Spika, pia kumi ninaishauri Serikali ije na mkakati wa kujenga tenki kubwa la kuhifadhi maji na litumike kuhudumia Kata saba za Uru Mashariki.

Kumi na moja, nanaishauri Serikali iwaunganishe kwenye mfumo wa maji wananchi wa vijiji vya Msuni na Njari vilivyopo Kata ya Uru Kaskazini kwani vyanzo vya mradi huu viko kwenye kata yao. Kwa kufanya hivyo, wananchi watakuwa walinzi bora wa miundominu na vyanzo vya maji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaishauri Serikali ipeleke maji ya mradi wa Tela Mande uliopo Old Moshi Magharibi katika maeneo ya tambarare huko Mandaka Mnono na vitongoji vyake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, jana nilichangia bajeti yako na kwa msisitizo, nimesikitika sana kuona Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Kata za Gwanseli, Magata Karutanga, Muleba, Bureza, Kikuku na Kagoma. Mradi huu ullanza kuasiisa mwaka 2009. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulikamilika mwaka 2020. Nimeulizia mara mbili juu ya mradi huu majibu yalikuwa ni ya kutia moyo kwamba mradi huu utakuwa kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023. Mradi huu, haupo kwenye bajeti yako. Nimesikitika sana, Muleba imesikitika sana. Nakuomba uangalie kwenye bajeti yako, mradi huu ni muhimu sana kwa Muleba.

SPIKA: Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, atafuatiwa na mtoa hoja.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nampenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametufanikisha kujadili mjadala huu muhimu sana kwa mustakabali wa maisha yetu kwani maji ni uhai na ni haki ya msingi kwa mwanadamu ye yote yule.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ameweza kutuheshimisha Wizara ya Maji. Kwa mara ya kwanza tayari tumeweza kufikia asilimia 95 za kupata fedha za mwaka wa fedha tunaoelekea kumaliza, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, na tunasema hatutaacha kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

dhamira yake njema ya kumtua mama ndoo kichwani inakwenda kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nipende kukushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo umeweza kutuongoza vyema na hata leo hii ndani ya Bunge lako tukufu bajeti hii imeweza kujadiliwa kwa mapana.

Mheshimiwa Spika, nipende kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa umoja wetu, mmeweza kutupongeza, tumepokea pongezi zote; mmeweza kutupa changamoto, yote tumeweza kuyapokea. Tunaahidi haya yote ambayo mmeweza kuyajadili kwa siku mbili ndani ya Bunge hili Tukufu ni deni kwetu.

Mheshimiwa Spika, mmetupongeza tumepokea kama deni. Kazi ambayo tumeweza kufanya kwa mwaka mmoja ambao tunaelekea kuimaliza tunaahidi tutaongeza ushirikiano kwenu kuhakikisha majimbo yote tunayafikia na huduma ya maji inakwenda kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, michango ni mingi na tunashukuru sana kwa michango yote. Ninakwenda kuongea tu kwa uchache kwa sababu Mheshimiwa Waziri ataongea kwa marefu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuongea kwenye Jimbo la Chemba; Mheshimiwa Monni ameongea mengi lakini nipende tu kusema kwamba Wizara inatambua changamoto zote ambazo Wilaya ya Chemba inaishi nazo.

Mheshimiwa Spika, lakini changamoto hizi kulingana na upendo wa Mheshimiwa Rais ambavyo ameweza kutupatia fedha za kutosha tutaendelea kuhakikisha changamoto iliyoko chemba tunakwenda kuifanyia kazi. Tayari tunakwenda kuchimba Bwawa la Farkwa ambalo maji yatakwenda mpaka Chemba, hiyo nayo itasaidia kwa sehemu kubwa sana kuwa na chanzo cha uhakika na mradi kuwa endelevu kwa sababu tunatamani mradi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

utakapokamilika basi mradi huo uwe na manufaa kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitaongelea pia kidogo kwa Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mbunge wa Mkinga. Naye pia tumepata hoja yake kuhusiana na matumizi ya Mto Zigi. Tumezingatia, tumepokea, na tutakwenda kuhakikisha tunatumia Mto Zigi ili uweze kupeleka maji Mkinga katika maeneo yale ambayo imeshindikana kupatikana mabwawa yakiwa yanakauka, sasa Mto Zigi utakwenda kuwa suluhu.

Mheshimiwa Spika, pia nitaongelea kidogo Mbeya Mjini; hili ni jimbo lako wewe. Umetuongoza hapa Wabunge wote tunafanikiwa, ni kwa sababu ya umahiri wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale Mbeya Mjini tunafahamu tatizo la maji suluhu yake ni Mto Kiwira. Tayari Mhandisi Mshauri ameshaleta andiko lake la awali sasa hivi tunamsubiria aweze kukamilisha andiko ambalo litatupatia gharama nzima ya mradi na tayari sisi kama Wizara tunaendelea kufanya *shortlisting* ya kupata wakandarasi ili tuweze kumpata mkandarasi sahihi ambaye atawea kumudu mradi ule mkubwa, mradi ambao Mbeya Jiji unautegemea.

Mheshimiwa Spika, mradi ule hautakuwa kwa ajili ya Mbeya Jiji tu, ni mradi ambao maeneo ya pembezoni mwa Mbeya Vijijini pia yanakwenda kunufaika; maeneo ya Chunya tunarajia yaje yanufaike na mradi huu; maeneo ya Mbalizi yanakwenda kunufaika; maeneo ya Rungwe pia yatakwenda kunufaika. Ni mradi ambao una tija hivyo, kwa heshima kubwa sana tunaliyonayo juu yako tutakwenda kufanya hili na wananchi watakwenda kunufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Mbeya, nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Suma Fyandomo, jana amechaniga kisomi sana, naamini sote tunesikia. Mradi wa Tukuyu Mjini nao pia tutakwenda kuuzingatia; ushauri tumepokea na tutaufanyia kazi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lengo la kuona kwamba *force account* huenda inachelewesha mradi, tutazingatia kuona namna tutaweza kushirikiana labda ya wakandari ili kuona mradi ule unakamilika. Na maeneo yote ambayo uliyataja kwa Tukuyu Mjini pamoja na kule alikotokea Mheshimiwa Spika wetu, basi yatakwenda kupata maji. Na haya tunayaongea siyo kama siasa, ila tunasema tunakwenda kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mungu katika hoja zote zilizotolewa zipo ndani ya uwezo wa Wizara na tunaweza kuongea haya yote kwa sababu Mheshimiwa Rais yupo tayari kuwa begabega na sisi. Tumejionea wenyewe kwa matendo, mliongoea hapa bajeti iliyopita lakini matendo na utekelezaji wa miradi sisi sote ni mashahidi. Hivyo, haya yote ambayo ninayaongea tutakwenda kuyafanya kazi kadri Mungu atakavyotuongoza na namna ambavyo Mheshimiwa Rais ataendelea kutuwezesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nihamie Jimbo la Magu kwa kaka yangu, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga. Jana ameongelea hapa kuhusu maji katika eneo lake. Sisi kama Wizara tunesema miradi ambayo inaendelea na utekelezaji ndani ya jimbo lake tutaisimamia kuhakikisha inakamilika; lengo ni kuona maji yanatoka bombani.

Mheshimiwa Spika, tunaposema mradi ukamilike tunahitaji kuona akina mama wanapata maji bombani yakiwa safi na salama na yakutosha na katika umbali rafiki. Tunahitaji kuona kwamba dhamira njema ya Mheshimiwa Rais inakwenda kuokoa ndoa za akina mama wengi.

Mheshimiwa Spika, akina mama wamekuwa wakiamka usiku wa manane na hii sasa tunaelekea ukingoni. Akina mama watapumzika nyumbani mpaka kunapambazuka, shughuli za nyumbani zitakamilika na maji yatakwenda kupatikana karibu na makazi ya wananchi. Na hili tatalitekeleza kuendana na mradi wake wa Butimba na miradi yote ambayo ipo ndani ya jimbo lake. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia basi pia naomba niongelee kidogo kwenye Jimbo la Biharamulo, Mheshimiwa *Engineer Ezra* ameweza kutuelekeza hapa hitaji la matumizi ya maji ya Ziwa Victoria. Sisi kama Wizara tumesema Biharamulo inakwenda kupata maji kuititia Ziwa Victoria. Na hii tutaifanya, tutafika kuhakikisha tunaleta msukumo mkubwa ili maji yaweze kupatikana na ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi nipende tena kuwashukuru Wabunge wote. Wabunge tunaomba mtusaidie kuitisha hii bajeti, lengo ni kwamba tuweze kukutana *site*, Sisi ombi letu kwenu ni kuitisha bajeti tuje tusimamie miradi, kama ambavyo tumefanya tuna uhakika tutafanya zaidi na zaidi kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, aje ahitimishe hoja yake. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa sababu maandiko yanasema yapaswa kushukuru kwa kila jambo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini kuwa kwenye dhamana ya Wizara hii ya Maji kuwapatia wananchi maji, kwa imani yangu ukiwapatia wananchi maji basi unapata baraka. Na nipo tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kuendelea kupata baraka hizi za kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nikushukuru wewe binafsi kwa mijadala tangu mwanzo mwisho mmeusimamia mpaka leo tunafika katika suala zima la kuhitimisha; nimshukuru pia Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna walivyozi simamia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

shughuli zao katika Bunge mpaka leo hii tunakwenda katika hitimisho.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, Makamu pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wizara yetu ya maji yawezekana kipindi hicho nyuma sikuwahi kuwa Mbunge lakini kuona Wizara inapongezwa, sijawahi kuona. Wizara ya Maji ilikuwa ni Wizara ya lawama, lakini leo hii Waheshimiwa Wabunge mnatupongeza; mmetutia moyo sana. Ahsanteni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naninachotaka kukisema tu mbele ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kama ni betri basi iko *fully charged*. Sisi viongozi wa Wizara ya Maji; mimi pamoja na Naibu wangu, Maryprisca Mahundi; Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, *Engineer Anthony Sanga*; Naibu Katibu Mkuu, Nadhifa Kemikimba, na watumishi wote kwa maana ya wataalam wa Wizara ya Maji, tutafia kwenye matenki katika kukahikikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa maoni na ushauri waliolenga kubadili mitazamo na fikra na kuboresha namna tutakavyofanya kazi Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotolewa ushauri ni pamoja na upatikanaji wa fedha, uvunaji wa maji ya mvua, upatikanaji wa misamaha ya kodi, ujenzi wa miundombinu ya majitaka, matumizi ya maji kutoka katika vyanzo toshelevu kwa maana ya ziwa na mito, umuhimu wa matumizi ya dira za maji za malipo kabla ya matumizi, masuala ya takwimu pamoja na maji kwa ajili ya wananchi na mifugo yao katika maeneo yanayopitiwa na mabomba makuu. Nataka niseme tu yote tumeyachukua na tutayafanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 65, wamechangia kwa kuongea na kwa maandishi. Kwa dhati kabisa nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo kwa kiasi kikubwa inalenga kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu yetu ndani ya Wizara ya Maji na taasisi zake na sekta kwa ujumla. Itoshe tu kusema Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa wachangiaji ni wengi sana nitaomba nijibu hoja kwa ujumla wake. Lakini kwa kweli nawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza kwa ujumla, michango ilivyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni mingi na yote inalenga kuleta tija kwenye sekta yetu ya maji. Hata hivyo, michango kadhaa imerudiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na mingine imechangiwa kwa hisia kali. Kwa kuwa muda uliopo hautoshi kujibu hoja zote, moja baada ya nyingine, naomba nitumie fursa hii kujibu hoja chache kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hoja moja wapo ambayo imezungumza ni juu ya upotevu wa maji; ni aibu na hatuwezi kukubali kuona Serikali inawekeza fedha nyingi wananchi wapate huduma ya maji halafu zije taarifa kwamba kumekuwa na upotevu mkubwa sana wa maji.

Mheshimiwa Spika, na mimi kama Waziri wa Maji nilishawahi kufanya ziara katika baadhi ya mamlaka zetu za maji. Niliwahi kupata taarifa kwamba hapa kuna upotevu wa maji wa asilimia 40, nilihoji kama kuna upotevu wa maji wa asilimai 40 kwa akili yangu tu ya kawaida kwamba ninategemea kuona mabwawa ya Samaki mtaani.

Mheshimiwa Spika, kwa akili yangu ya kawaida nilitegemea nione chemichemi za mito. Asilimia 40 ya upotevu wa maji si jambo dogo Waheshimiwa Wabunge. Kwa bahati nikamwambia hebu nипитиhe baadhi ya mitaa sasa nione maji yanayopotea; tumeピta baadhi ya mitaa sikuona hiyo asilimia 40 ya maji inayopotea.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ukweli wa dhati kabisa ni kwamba maji tunayosema yanapotea asilimia kubwa au kwa kiwango kikubwa yanaibiwa. Baadhi ya viwanda wanaweza wakajunganishia kinyemela pasipo kulipa halafu mamlaka ya maji inadai kwamba au inatoa taarifa kwamba maji yale yamepotea, lakini yule ni mteja ambaye ametumia maji lakini hahesabiki katika taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ni maelekezo ambayo tumetoa kwa baadhi ya mamlaka zetu za maji kuwajua wateja wao wakubwa na wadogo katika kuhakikisha wanadhibiti ili maji na malipo yaweze kupatikana na wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Na viro baadhi ya viwanda tulishawahi kukamata na tumeweza kuchukua hatua, lakini Waheshimiwa Wabunge hili jambo lazima tukubali kushirikiana. Serikali inawekeza fedha nyingi kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna nyingine sisi kama Wizara tumejipanga kutoa fedha na kukarabati maeneo ambayo yamekuwa na miundo mbinu chakavu ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mathalani, eneo la Mtwara pale mjini. Mahitaji ya Mji wa Mtwara ni lita milioni 15, uzalishaji wa vyanzo vyetu ni lita milioni 13, lakini changamoto ya pale Mtwara ni miundombinu chakavu tangu ukoloni. Kupitia bajeti hii tunatoa fedha kwa eneo la Mtwara kuhakikisha wanakwenda kutengeneza miundombinu ile na wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kikubwa ni kwamba hili tumeliona na tutahakikisha kwamba kila mtumiaji anakua na dira bora ili kudhibiti upotevu huu wa maji na tuweze kuuweka katika asilimia ambayo inakubalika, asilimia 20. Sasa hivi kinchi tupo asilimia 36, lakini maelekezo ya Wizara ambayo tumewapa mamlaka zetu, na ndiyo kipimo, katika kuhakikisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwamba lazima wasimame hapa na kwa kushirikiana na *EWURA* tunaendelea kudhibiti mamlaka zetu kuhakikisha kwamba tunakuwa katika hiki kiwango cha asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili lilizungumzwa ni tatizo la bei za maji mijini na vijivjini; ni haki ya mwananchi kupatiwa huduma ya maji lakini mwananchi naye asisahau ana wajibu wa kulipia bili za maji. Ili gari liende lazima liwe na mafuta.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mwananchi kupatiwa huduma hii ya maji lazima atambue maji kutoka mtoni hayana miguu useme yatafika nyumbani lazima tuweke pampu na umeme ili kuhakikisha kwamba maji yale yanafika. Kwa maana hiyo, pale kutakuwa na gharama zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na wajibu wa mwananchi kulipia bili za maji, sisi kama Wizara ya Maji tunasema bili hizo zisiwe bambikizi. Haiwezekani mwananchi ametumia maji ya 15,000 unamwambia alipe 120,000; haiwezekani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, moja, tumetoa maelekezo kwa wasomaji mita wetu kwamba lazima wawe waamini na waadilifu juu ya usomaji. Lakini tumekwenda mbali sisi kama Wizara ya Maji kwa maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, sisi lazima tutumie teknolojia ya sasa kuhakikisha tunafanya mageuzi katika Wizara yetu ya maji.

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha *Unified Billing System*. Kabla mteja hajasomewa mita zake au hajachajiwa bili anayotakiwa kulipa, anapokea *message* kwamba bwana fulani umetumia maji *unit* 30 unadaiwa kiasi fulani, thibitisha, anathibitisha mwisho wa siku tunaweza *kum-charge* bili ili aweze kulipa.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubali kwamba sisi Wizara ya Maji si kisiwa, lazima tukubali kubadilika. Na kizuri huigwa. Tunaona wenzetu wa *TANESCO*wana mita za LUKU. Ni muda muafaka, na tumeshatoa maelekezo kwa Wizara. Na nimshukuru sana Katibu Mkuu wetu wa Wizara ya Maji, kaka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yangu, *Engineer Anthony Sanga*, mimi nasema anatosha mpaka chenji inabaki, tumpigie makofi mengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wadau mbalimbali wameshakuja, tunajifunza hizi mita kabla hatujaenda kumfungia mwananchi, zile changamoto ambazo tunaziona basi tuweze kuzitatua. Lakini eneo ambalo tunaweza kuondokana na changamoto ya bili za maji lazima tukubali mwarobaini wake ni *prepaid meter*, lazima twende katika katika uelekezo huo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo naomba tusaidiane katika hili ili kuhakikisha kwamba tunafanya mageuzi katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo kama Waziri wa Maji nimejifunza, inakuwaje mwananchi Jijini Dar es Salaam *unit* ya maji analipa 1,600, lakini ukienda kijijini mwananchi anatumia maji ndoo ananunua kwa shilingi 50. Unaposema *unit* moja maana yake nini; *unit* moja maana yake ni lita 1,000. Lita 1,000 maana yake nini; lita 1,000 maana yake ndoo za lita 20, ziwe 50.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa mwananchi wa kijijini akinunua ndoo shilingi 50 maana yake ndoo 50 analipa shilingi 2,500 ilihali pale *DAWASA* Dar es Salaam mwananchi ananunua *unit* moja kwa shilingi 1,600 tena anapata nyumbani; hilo haliwezekani. Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, ametupa maelekezo Wizara ya Maji; wananchi watumie maji kwa bei rahisi na nafuu na wanufaika na matunda ya Serikali yao ya Awamu ya Sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Maji kupitia *RUWASA* tumetoa maelekezo mahususi kupitia bei zote za maji vijijini. Baada ya Bunge hili tutatoa bei elekezi kwa vijijini ili kuhakikisha wananaufaika kwa kazi kubwa na maoni mazuri yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wao hapa katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, nataka nizungumze jambo moja; lazima tukubali Rais wetu tangu ameingia ni mwaka mmoja tu. Hatuwezi kusema kwamba tumemaliza matatizo ya maji kabisa. Lakini tunachotaka kusema ni kwamba jithada za muda mfupi ambazo amezifanya Rais wetu Mama Samia Suluhu si za kubeza hata kidogo, anatakiwa kuungwa mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi katika Wizara yetu ya Maji, haijawahi kutokea bajeti kutekelezwa kwa asilimia hata 80, leo tunaitekeleza bajeti asilimia 95; haijawahi kutokea. Yapo maandiko ya dini yanasema *Waama "Bi-Neemat Rabbika Fahadithi"*, zielezeeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru; tumshukuru sana Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *actions speak louder than words*, matendo yanaongea kuliko maneno. Leo tunaona Mheshimiwa Rais kwa mwaka mmoja kwa namna ya fedha hizo zilizotoka, achana na hilo tu la fedha, ye ye kama Mama maelekezo ambayo ametupa sisi Wizara ya Maji, mimi ndio Waziri pekee ambaye niliwhati kusimamishwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka alisema Waziri wa Maji uko wapi nikasimama. Akasema ye ye ni Mama na anatambua asilimia kubwa ya wanaoteseka ni akina mama Vijiji. Akina mama wanatembea umbali mrefu kwa kukosa maji kwa maana ya kutafuta maji, wengine wamepoteza ndoa zao. Hataki kusikia, hataki kuona akina mama wakiteseka juu ya tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, nataka niwaambie baada ya maneno yale mimi sikuwhati kulala, lakini nilikaa na nikajitafakari na Waheshimiwa viongozi wenzangu kwa maana watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hakuna sikio lolote duniani lisilosikia vinywa vingi vikisema pamoja; tumewasikia.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ilikuwa na changamoto nyingi sana lakini mpaka hapa tulipofiki, tulipotoka ni mbali. Moja ya changamoto kubwa sana ambazo zilikuwa zinaiathiri Wizara yetu ya Maji ni miradi illyojengwa chini ya kiwango ya vijiji 10. Ni miradi ambayo imejengwa matenki lakini haitoi maji.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kwanza ambayo tumejipa – na tuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kuona haja ya kuanzishwa Wakala wa Maji Vijiji (*RUWASA*), hayo ni maoni yenu Waheshimiwa Wabunge. *RUWASA* ina miaka miwili hadi mitatu sasa tunakwenda, kama ndama, amezaliwa na kwenda. Ameikuta miradi 177. Kwa muda huu mfupi nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge miradi 127 tumekwishaikwamua katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa tunaona nuru na mwendo wa Wizara yetu ya Maji, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha; Mheshimiwa Rais anatus-support. Tumezungumza hapa, Wizara ya Maji, kwa maana kama nchi, hatuna uhaba ama umasikini wa vyanzo vya maji, tuna maji juu ya ardhi zaidi ya mita za ujazo bilioni 105, maji chini ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 21 kwa maana ya *total* ya bilioni 126; hatuna sababu ya kulalamika juu ya matatizo ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto zilizokuwa zinatuathiri sisi Wizara ya Maji ni vitendea kazi. Leo kwa Mheshimiwa Kuchauka, pale miaka yote watu wamefanya tafiti pamoja na tunatambua rasilimali za maji tulizokuwa nazo, ni mita za ujazo bilioni 21 lakini hatupati maji na tulishaaminishwa kwamba hapa maji hakuna. Lakini nashukuru sana wataalam wetu kwa *mind set* ambazo tunazigeuza, leo wamekwenda Liwale tumepata maji ya kutosha, na Mheshimiwa Mbunge ni shahidi, tunakwenda kupeleka fedha sasa kutatua tatizo la maji Liwale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nini maana yake; wakati mwingine tunashindwa kujua maji chini ya ardhi yapo au hayapo kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sababu ya ukosefu wa vifaa vya kisasa. Uking'ang'ania vifaa vilivyopitwa na wakati utakuwa umepitwa na wakati. Samia Suluhu Hassan ndio suluhu ya matatizo ya maji hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ametupatia fedha, tunakwenda kununua mitambo 25 kwa ajili ya kuchimba visima. Na kila mkoa utakuwa na mtambo wake wa kuchimba; haijawahi kutokea, tumpigie makofi mengi sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, achana tu na mitambo, anatambua kwamba siyo maeneo yote ukichimba unaweza ukapata maji; siyo maeneo yote. Yapo maeneo ambayo tukichimba tunapoteza fedha za Serikali. Ametupatia fedha kwenda kununua seti tano kwa ajili ya kuchimba mabwawa, siyo tu kwa wananchi kupata maji, bali hadi mifugo yao nayo iweze kupata maji. Haya ni mageuzi makubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mitambo kwa ajili ya utafiti, zaidi ya minne, fedha ameshatupa. Ndani ya mwezi huu wa Sita tutapokea vifaa vile katika kuhakikisha watu wanakwenda kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, na ninataka niwaambie wakandarasi na wahandisi wetu wa maji – nilishazungumza kwenye bajeti – sisi viongozi wa Wizara ya Maji tutacheka kwa kuona maji bombani, lakini kwa mhandisi ama mkandarasi ambaye atatuchelewesha juu ya upatikanaji wa maji, ukicheka na nyani utavuna mabua, sisi hatupo tayari kucheka na mtu yejote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la miji 28. Tulikuwa na viporo ama miradi ambayo ilikuwepo tu kwenye makaratsasi Waheshimiwa Wabunge. Suala la miji 28 lilikuwa likizungumzwa tu, halitekelezeki. Samia Suluhu Hassan ndiyo amekuja kuwa-*unlock* mradi huu wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, amefanya mazungumzo na Viongozi Wakuu wa India, amemuita Balozi Ofisini kwake. Leo nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tumalize Bunge, Mheshimiwa Rais tumemuomba ashuhudie utiaji saini wa miradi hii kwenda kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, na narudia hapa; tuisidanganyane, tunakwenda kutekeleza Mradi wa Maji HTM kwa maana Handeni, Korogwe, Muheza, Pangani; tunakwenda Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Chunya, Rujewa, Waking'ombe, Makambako, Njombe, Kiomboi, Singida, Manyoni, Chemba, Chamwino, Mugumu, Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kayanga, Geita, Chato, Mafinga, Makonde, Rorya, Tarime na Songea. Hizi ni jitihada kubwa zinazofanywa na Rais wetu Mama Samia Suluhi Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, jana kaka yangu, Mheshimiwa Katani – hapa naona ameondoka – nataka nimueleze yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Maji maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais ametupa hajatueleza kwamba sehemu fulani peleka maji, sehemu nydingine usipeleke. Ametupa maelekezo kuhakikisha asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijiji na asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mjini.

Mheshimiwa Spika, tumetenga kiasi cha shillingi bilioni 29 kwenda kutekeleza miradi ya maji 44 katika Mkoa wa Mtwara. Lakini katika Jimbo la Mheshimiwa Katani tunakwenda kutekeleza mradi ambao unajumuisha zaidi ya vijiji 15 ambao unaoitwa Mradi wa Nanyuwila – Maundo. Mradi ambao utakwenda kutatua matatizo ya maji kwa Vijiji 15 vya Nakayaka, Mnyawa, Mchichira, Mkwajuni, Shangani, Pachani, Mnarani, Namahonga, Maundo, Chiumo, Chang'ombe, Kunanundu, Lukokoda, Ghanajuu na Ghanachini; hizi ni jitahada za Mheshimiwa Rais.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna Mradi ambao tunauita wa Mkwiti ambao unakwenda kutatua shida ya maji katika vijiji 17, Kijiji kimoja sasa hivi cha Mangombya kimeshaanza kupata huduma ya maji. Mkandarasi yuko *site* anaendelea na ujenzi wa matenki matano ili kuhakikisha wananchi hawa wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tumesikia maombi ya Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara juu ya ujenzi wa Mradi wa Makonde. Mimi binafsi Mheshimiwa Rais alinituma kwenda zangu Newala nimekwenda kujiona hali ya mradi ule.

Mheshimiwa Spika, mradi ule ni chakavu, mradi ule tangu Baba wa Taifa, mradi una umri mkuwa kuliko mimi Waziri wa Maji na hamna namna nyingine zaidi ya kujenga mradi mpya. Nataka nimpe taarifa baba yangu, Mheshimiwa Mkuchika, na Mheshimiwa Katani, waandae futi. Mheshimiwa Rais ametupa maelekezo na tumekwishapata mkandarasi, kilichobaki tunakwenda kusaini mradi wa zaidi ya bilioni moja kuhakikisha Wanamakonde, Tandahimba pamoja na Nanyamba wanakwenda kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ipo miji tunasema kwamba imeachwa. Lakini pia moja ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezijenga ni kuhakikisha kwamba Serikali inatumia rasilimali toshelevu kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaanza; ukienda Lindi pale Mjini tuna mradi wa bilioni 33 umekwishakamilika. Mradi ule wa bilioni 33 tumetoa bilioni tatu kwa ajili ya kupeleka maji Mitwero. Sasa hivi tumetoa bilioni 12 kwa ajili ya kupeleka maji Mchinga kwa mama yetu, Mheshimiwa Salma Kikwete. Hizo ni jitahada kubwa sana za Serikali.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukaenda zako Musoma kwa dada yangu, Mheshimiwa Esther Matiko, Mkoa wa Mara, tuna

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mradi wa zaidi ya bilioni pale, tumeshaukamilisha. Lakini tumekuja na Mheshimiwa Rais katika Mradi wa Mugango – Kiabakari – Butiama, zaidi ya bilioni 70. Tumekwishautekeleza. Sasa hivi tumeshaukamilisha mradi pale Bunda Mjini zaidi ya bilioni 10; hivi Mheshimiwa Rais awape nini au awape donda mfukuze nzi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kikubwa sisi tunachotaka ni kumuunga mkono Rais wetu. Tumeona ameyatoa maji Ziwa Victoria tumeuyaleta Tabora, tumeyapeleka Igunga, tumeyapeleka Nzega, zaidi ya bilioni 600, na vijiji 100 vinapata huduma ya maji safi na salama. Mradi ule sasa unakwenda Kaliua, unakwenda Sikonge hadi Urambo kwa Mheshimiwa Mama Sitta, katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ukienda Arusha tuna mradi wa zaidi ya bilioni 520 hii; hii yote ni katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ukienda zako pale Sumbawanga Mjini tuna mradi wa zaidi ya bilioni 35; hizi ni jitihada kubwa. Kwa hiyo kikubwa Waheshimiwa Wabunge tunakubaliana kwamba rasilimali toshelevu kwa maana ya maziwa na mito tuliyokuwa nayo, ikitumika itakwenda kutatua matatizo ya maji. Na mimi Waziri wa Maji naamini hilo kupitia Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, leo tunakwenda kutatua mradi mkubwa wa maji pale Mbeya kwa kutumia Mto Kiwira kwa maelekezo tu. Sisi Waheshimiwa Wabunge maelezo na maoni mliyotupa tumeyapata tutayafanyia kazi katika kuhakikisha watanzania wanapata maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho; Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan lazima tumuunge mkono. Kama nilivyotangulia kusema awali, kuna mambo ambayo ni magumu kufanyika lakini Rais wetu ana uthubutu. Tumeona Dar es Salaam namna tulivyopitia kwenye changamoto ya *crisis*ya Mto Ruvu kukauka, leo tunakwenda kujenga Bwawa la Kidunda. Huu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni uthubutu wa hali kubwa sana, na tumpigie makofi sana Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofi*)

Lakini tunaona eneo hili la Jiji la Dodoma tangu Serikali ihamie hapa kumekuwa na uhitaji mkubwa sana wa maji. Kwa muda mfupi Mheshimiwa Rais ameingia, kutohana na mahusiano yake mazuri, tumeputa fedha kupitia *African Development Bank*, zaidi ya *USD* milioni 125 kwa ajili ya kwenda kuanza kujenga Bwawa lile la Farkwa; hizi ni jitihada kubwa sana. Bunge limeshauri kwa muda mrefu lakini utekelezaji wake ulikuwa wa kusuasua, leo tunakwenda kulitekeleza hili jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, ahsante sana na Waheshimiwa Wabunge Mwenyezi Mungu Awabariki sana. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa kabla hatujaendelea na utaratibu wetu, nimuite Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi kwa Wizara ya Maji, Fungu 49, ukurasa 327.

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 49 – Wizara ya Maji

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 3,973,088,226

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri. Wako Waheshimiwa Wajumbe wawili ambao wanataka ufanunuizi, na kwa mujibu wa Kanuni zetu hawa wanaotaka kupata ufanuzi kwenye kifungu chenye mshahara wa Waziri wanapaswa kuomba ufanuzi kwenye jambo mahususi la kisera. Tutaanza na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kutaka kupata ufanuzi kwenye jambo la kisera kwamba miradi mingi ya maji inakwama kutokana na uagizaji wa vifaa kutoka nje ya nchi ambavyo vinakwenda kukwama pale Bandarini na kusababisha wakati mwingine kuchelewa kulipa ushuru ambapo inasababisha wananchi kukosa miradi ile ya maendeleo ambayo walikuwa wameahidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaomba kupata ufanuzi katika jambo ambalo nilieleza hapa Bungeni wakati nachangia hoja hii ya Wizara ya Maji. Lakini bahati mbaya sikuona Waziri analitolea ufanuzi kwa hiyo natarajia kuchukua shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwenye mshahara wake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Nashon, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya pale. Lakini kubwa ambalo nataka nimuhidi na nimhakikishie ni kwamba moja ya changamoto kubwa za Wizara ya Maji katika utekelezaji wa miradi ya maji ilikuwa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama viongozi wa Wizara tulishakaa na viongozi wa Wizara ya Fedha, kwa kweli tumeona mwanga. Na tumekuwa na mahusiano makubwa sana na *TRA*, niombe tu kwa hiyo changamoto ambayo tumeipata tunakwenda kuifanyia kazi kwa haraka kuhakikisha kwamba tenki lile linapatikana kwa wakati. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, naona amesimama.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, bado sijamuelewa vizuri kwa sababu nilitaka atoe *commitment* ya Serikali. Kwamba ni lini tenki hilo litaondoka litatoka pale bandarini na ni lini litafika pale Kazuramiba?

MWENYEKITI: Sasa hilo linahusu tenki mahususi lakini hoja yako ile ya msingi ya kwamba miradi inachelewa kwa sababu ya mizigo kubaki bandarini ndiyo iliyomfanya Mheshimiwa Waziri asimame kutoa ufanuzi.

Lakini sasa kwa hilo jambo mahususi la tenki la kule kwako hilo inabidi litolewe majibu siyo kwenye kifungu hiki kwa sababu hilo ni jambo mahususi lakini siyo la kisera, lile la mwanzo ni la kisera. Kwa hiyo kwa sababu tunaendelea kuifunza, nakupa nafasi kwenye hoja yako ya kisera, kama umeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri au kama hujaridhika ndiyo hapo unaposhika shilingi ili watu wakuunge mkono.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nimeridhika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nakushukuru. Na mimi naomba ufanuzi kwenye suala la upotevu wa maji; nikiwa nachangia nimelizungumza hili kwa *data kabisa*, na Mheshimiwa Waziri amelizungumza akionesa na yeche hakubaliani na upotevu huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kama Wabunge tuna wajibu wa kuisimamia Serikali. Kwa mwaka mmoja tu Serikali imepata hasara ya bilioni 175. Kwa mazingira haya, kupitia Ripoti ya CAG, kwa miaka mitatu mfululizo Mamlaka za Maji 24; 22 zote zimekuwa na upotevu wa maji. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ambao umeshatolewa mara kadhaa, Dar es Salaam peke yake tumepata hasara ya bilioni 94.6. Sina haja ya kuondoka na shilingi ya Waziri; tunataka mkakati wa Serikali ili fedha hizi zikawasaidie wananchi maskini, hasa kwenye mito na maziwa, likiwemo na Ziwa Tanganyika. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri nadhani hilo lilikuwa ni pendekezo, kwamba Serikali iwe na mkakati. Haya maelezo kwa pendekezo hilo liliotolewa na Mheshimiwa Mjumbe.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Aida; ni ushauri mzuri sana na tumekwisha upokea na tumeshaanza kuufanya kazi.

Moja ya vipimo vyta watendaji wetu kwa maana wakurugenzi, tumewasainisha mikataba ya utendaji kazi; lakini pia kwa maelekezo mahsus iuu ya ukarabati wa miundombinu yetu ya maji ili kuhakikisha maji hayapotei hovyo hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, lazima twende na kutoa elimu kwa wananchi. Wakati mwingine maji yanapotea tu, mtu anaweza akasema kwamba maji yanapotea kwa sababu tu ya matumizi; leo hii mtu anakwenda kupiga mswaki tu amefungulia bomba. Kwa hiyo, tutakwendana sambamba na elimu lakini pia utoaji wa dira za maji ambazo zitakuwa bora kwa wateja wetu ili kudhibiti upotevu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkakati mahsus i maeneo ambapo tunaona miundombinu chakavu ni kuhakikisha kwamba tunakarabati miundombinu ile, na pia utoaji wa taarifa eneo gani linakuwa linavuja ili wataalam wetu waweze kufika kwa wakati ili mwisho wa siku waweze kudhibiti mivujo hiyo. Ahsante sana. (*Makofii*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.1,547,769,238
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh.1,127,916,365
Kifungu 1004 – <i>Government Communication Unit</i>	Sh.493,546,394
Kifungu 1005 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh.523,140,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh.1,017,624,279
Kifungu 1007 – <i>Management Information System Unit</i>	Sh.537,349,503
Kifungu 1008 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.638,618,800
Kifungu 1009 – <i>Project Prep., Coord. and Delivery Unit</i>	Sh. 733,454,182
Kifungu 2001 – <i>Water Resources</i>	Sh. 6,656,481,325
Kifungu 2003 – <i>Water Laboratory</i>	Sh. 2,515,482,087

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 3001 – <i>Water Supply and Sanitation Division</i>	Sh. 28,448,858,601
--	--------------------

MWENYEKITI: Mheshimiwa Assa Makanika.

MHE. ASSA N. MAKANIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nimejaribu kuitia Kitabu cha Maendeleo, hii *Volume Number IV*, kifungu hicho kilichotajwa 3001 kwenye vifungu vidogo 3342 nimeona pale kuna miradi mingi na Mheshimiwa Waziri ametaja kutoka Ziwa Victoria na kwenda maeneo mengine, ninaomba Bunge lako tukufu liweze kuridhia ili tuweze kufanya *re-allocation* ili tuweze kugawana hii miradi sawa; maana imekuwa mingi lakini sisi watu wa Rukwa, watu wa Katavi...

MWENYEKITI: Hebu ngoja kwanza; Mheshimiwa Assa Makanika hicho ni Kitabu cha Maendeleo au ni hiki cha Matumizi ya Kawaida?

MHE. ASSA N. MAKANIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sorry Matumizi ya Kawaida.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Hicho kifungu umetaja 3000 na ngapi?

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Mwenyezekiti, 3001, Kifungu kidogo 3342.

MWENYEKITI: Aah hicho ni cha maendeleo, siyo kitabu hiki tulichopo sasa. Umeelewa Mheshimiwa Assa Makanika? Kwa sababu kitabu tulichopo sasa hakuna hicho kifungu kidogo unachokitaja, hakipo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 5001 – *Water Development and Management Institute*.....Sh.3,248,940,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 49 – Wizara ya Maji

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh.3,690,000,000

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh.10,050,000,000

Kifungu 2001 – *Water Resources*Sh. 29,870,000,000

Kifungu 2003 – *Water Laboratory*Sh. 5,068,000,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 3001 – *Water Supply and Sanitation Division*Sh. 609,221,338,000

MWENYEKITI: Hapa ndiyo nadhani Mheshimiwa Assa Makanika ulikuwa na hoja yako; sasa ielezee hoja yako.

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ndiyo, nashukuru. Hoja yangu ilikuwa ni katika kufanya re-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

allocation katika Kifungu hiki. Nimeona Kifungu kidogo 3342 kimeonesha kutoa maji katika Ziwa Victoria na Mheshimiwa Waziri ameweza kuelezea miradi wanayofanya inayotoka katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi watu wengine huku ukingalia na sisi tuna mradi wa kutoa maji kutoka katika Ziwa Tanganyika, hatujatazamwa hata kidogo. Tunaomba kupata maelezo ya Waziri ili ikiwezekana na Bunge lako lilitidhie tuweze kufanya *re-allocation*. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Assa Makanika unataka *re-allocation* kutokea kifungu gani kwenda kifungu kipi?

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kutazama Kifungu hiki 3342 na Kifungu kingine 3403 vyote vinaonesha kabisa vinælekeza mradi huu kwenye mkoa mmoja. Kwa hiyo, hoja yangu ilikuwa ni katika kufanya *re-allocation* ya hii Keki ya Taifa kwa maana ya Vifungu hivi tuweze kuki-*reallocates* kimoja ili tuweze kugawana Keki ya Taifa sawa, na hata sisi wa Ukanda wa Magharibi tuweze kupata haki hiyo. Hii ni kutokana na kwamba hata mradi wetu ambao unatoa maji kutoka *Lake Tanganyika* haujawekwa kabisa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, Kanuni ya 121(1); "121.-(1) Katika Kamati ya Matumizi, Mbunge ye yeyote anaweza kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadaliko kwa Makadirio ya Matumizi ya Serikali iwapo mabadiliko hayo hayatabadili madhumuni ya Fungu.

(2) Endapo hoja iliyotolewa kwa ajili ya kupunguza kifungu fulani katika Fungu lolote hajapitishwa, hoja nyingine bado inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kupunguza kifungu kingine cha Fungu hilo hilo."

Maana yake ni kwamba unapotaka fedha zihame kutoka kifungu fulani zielekee Kifungu kingine, hicho kifungu lazima kiwepo hapa, ndiyo maana ya hii Kanuni. Yaani huwezi kutoa fedha kwenye kifungu ukataka kuanzisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kifungu kipyा kwenye ngazi hii. Sijui Mheshimiwa Makanika umenielewa?

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MWENYEKITI: Umenielewa enhee?

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, hoja yako itakuwa imesikika kwa upande wa Wizara, kwamba yapo na maeneo mengine ambayo yana maziwa au yana vyanzo vikubwa vya maji ambavyo ni muhimu sana Wizara kuanza kuangalia mikoa ya hayo maeneo, waanze kuiwekea miradi, ili sasa ikifika mahali kama hapa tuanze sasa kusema fedha zimekwenda nyingi huku, zipunguziwe huku, ziende huku na mambo kama hayo. Hayo ndiyo madhumuni ya Kanuni ya 121.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwa mujibu wa utaratibu wetu; kwamba Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2022/2023 – Wizara ya Maji
yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hii ni moja kati ya bajeti ambazo zimeafikiwa na Bunge zima. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote; niwapongeze kwamba Bunge limeafikiana na yale ambayo mmesema mnakwenda kuyafanya na wamekubaliana na yote mliyoahidi. Na sisi tunawatakia kila la heri kwenda kutekeleza hayo yote mliyosema mnakwenda kuyafanya.

Waheshimiwa Wabunge, nitumile fursa hii kuwashukuru sana Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa kazi nzuri wanayoifanya, mpaka tukifikia hapa kuipongeza hii Wizara maana yake Kamati yetu inafanya kazi nzuri ya kuisimamia Wizara hii. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri kwenye sekta hii muhimu kabisa ambayo inazungumzia uhai wetu sisi kama wanadamu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo, sasa niseme rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri na watendaji kazi wako wote tunawatakania kila la kheri katika utekelezaji wa yale yote mliyosema mnakwenda kuyafanya.

Na jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri umelizungumzia hapa – lakini kwa msisito, kwa sababu kuna hoja ilijitokeza tukiwa kwenye Kamati ya Matumizi – ni hoja ya Wizara kuwa na mkakati maalum. Hizi sifa hapa zote zinatokana na ule utekelezaji wa hii miradi ambayo ipo kwenye maeneo mahususi na kwamba inawaletea tayari watu maji, na kuna matumaini hayo ya kupata maji kwa miradi ambayo inaendelea kujengwa.

Lakini ni muhimu sisi kama Taifa kutengeneza mkakati maalum kwa ajili ya kutumia vyanzo vyetu vikubwa vyta maji ili upatikanaji wa maji uwe endelevu maeneo yote nchini. Kwa hiyo tunaposikia Ziwa Victoria, ni hivyo hivyo utawasikia wa Ziwa Tanganyika, watazungumza hayo; wa Ziwa Nyasa watazungumza hayo; wa Mto Ruvuma watazungumza hayo; na mito yote iliyopo hapa nchini.

Kwa hiyo ni vizuri kama Wizara kuwa na huo mkakati, pamoja na kwamba hii ni miradi mingine kwa sasa inatusaidia maeneo mbalimbali wananchi kuendelea kupata maji. (*Makof*)

Kwa hiyo tunawatakania kila la kheri katika hayo na tunaamini lile ambalo limejitokeza sasa mwakani tutaweza kuona namna ambavyo maeneo mengine pia yanatazamwa kama ambavyo maeneo yale ambayo yatapitiwa na Mradi wa Ziwa Victoria utafanya, basi tutaanza kusikia sasa Ziwa Tanganyika litapeleka maji wapi na wapi, Ziwa Nyasa litapeleka wapi na wapi; na mito ile mikubwa itapeleka maji wapi na wapi. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kuyasema hayo pia niwashukuru Wabunge ambao siyo Wajumbe wa Kamati hii ambao wamepata nafasi ya kutoa mawazo yao kwa ajili ya kuishauri Serikali. Ni jambo jema kwa sababu mtu anapochangia hapa ndani ni kwamba anakuwa amejandaa. Kwa hiyo niwapongeze pia Wabunge ambao

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wametoa mawazo yao ili Wizara inapokwenda kutekeleza ikaendelee kuangalia na mambo mengine ambayo hayakuwepo kabisa katika mpango wao katika mwaka 2022/2023. (*Makofi*)

Nileta matangazo niliyonayo hapa Mezani: -

Kwanza ni tangazo la wageni; wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambaao ni wakandarasi na wadau kutoka Moshi Mjini, Mkoani Kilimanjaro; Mhandisi Jonas Mshiu na Mhandisi John Benedict; karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wageni 50 wa Bunge *Sports Club* ambaao ni viongozi na wachezaji wa Iringa *All Stars Veterans*, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndg. Abdusufiani Silia. Karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Katika kikosi hicho naambiwa yupo mchezaji wa zamani wa Yanga Ndg. Ally Msigwa; karibu sana, karibu sana. (*Makofi*)

Sasa nimewaona humu ndani na Simba pia wamepiga jamani, na Simba pia wamepongeza, kwa hiyo Yanga mmepongezwa na Simba pia. (*Makofi/Vicheko*)

Waheshimiwa Wabunge mlitangaziwa asubuhi kuhusu michezo siku ya kesho, kwamba kesho tarehe 14 Mei, 2022, kutakuwa na mechi za kirafiki za mpira wa miguu (*football*) na mpira wa *pete (netball)* kati ya *Bunge Sports Club* na *Iringa All Star Veterans*.

Mechi hizi zitachezwa katika viwanja vifuatavyo; kwanza ni mpira wa miguu Kiwanja cha *Fountain Gate Academy* kilichopo Mlimwa C. Kwa hiyo, jamani wale mnaokwenda kucheza mpira wa miguu mjiandae, yupo mchezaji wa zamani wa Yanga humu ndani.

Lakini pia wale watakuokuwa wanakwenda kutazama mpira wa *pete* utakuwa Uwanja wa Jamhuri, na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wenyewe watakuwa wanacheza na wachezaji kutoka Iringa. Pia michezo yote itachezwa kuanzia saa 10.00. Na mimi nilikuwa namtafuta kati ya wale wachezaji wanawake sijui ni yupi nitakayekuwa namkaba kesho lakini tutaonana uwanjani bila shaka. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni 250 ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndg. Jamal Adam; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 4 kutoka kutoka Kampuni ya *Afrizania Building Materials (ABM)* ya Mkoani Dar es Salaam, wakiongozwa na *Business Development Manager* Ndg. Suleiman Hassan; karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge hawa ndio wageni tulionao, japo kuwa kule juu naona wageni zaidi, ila hayo ndiyo majina ya wageni nilionayo hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine na hili ni tangazo la kazi; Wajumbe wa Kamati ya Uongozi mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge tukutane hapa nyuma kwenye *Lounge* ya Spika kuna kikao muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kwa sababu leo tunahitimisha hotuba hii ya bajeti, nizungumze mambo mawili ambayo yamejitokeza wakati wa mjadala wa hii bajeti.

Kwanza kabisa, upo mjadala ambaao Waheshimiwa Wabunge huwa tunakumbushwa siku zote, tumeapa sisi kuilinda Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo ni muhimu sana kuzingatia kwamba michango yetu isiwe kwa namna yoyote ile inaashiria kuvunja Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wapo Wabunge hapa, kwa nia njema kabisa, wamechangia kwa kuonesha kwamba maeneo yao ni kama ya nchi jirani na hizo nchi jirani zimetajwa humu ndani,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwamba pengine sisi tunaonekana ni wa nchi fulani, na pengine sisi tunaonekana wa nchi fulani.

Sasa tukumbuke nchi yetu hii ilishawahidi kupigana vita kwa nchi fulani kutangaza eneo fulani la nchi yetu kwamba ni sehemu yao; na kwa sababu vita hii ilikuwa ya wazi kabisa, siyo siri, hiyo inaweza kutajwa humu ndani. Tuliingia vitani na Uganda kwa Uganda kutangaza kwamba Kagera ilikuwa sehemu yao. Kwa hivyo, msiyachukulie mambo haya kiurahisi mnapozunguza hapa Bungeni.

Kulitaja eneo la nchi yetu kama sehemu ya nchi nyiningine ni kama unataka sasa nchi ile ichukue hilo eneo ili tuingie vitani ama unataka kusemaj? Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge, hata kama una hisia kali sana tujizui kutoa michango ambayo inaashiria sisi wenyewe ni kama tunakuwa hatufahamu mpaka ya maneno yetu.

Changamoto ni kwamba Kanuni zetu haziruhusu kusoma unapochangia, lakini yapime yale maneno yako unayoyazungumza wewe kama Mbunge na kama kiongozi wa nchi hii. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuzingatie hilo. (*Makofi*)

Lakini pia, tunapozungumza tusichanganye mambo mpaka tukatuma ujumbe kwa wananchi tunaowaongoza kana kwamba wapo watu wa eneo fulani wanapendeleva sana na wengine wanaonewa sana. Ninyi ni mashahidi hapa, na ilitajwa mikoa kama mitatu hivi, lakini mikoa miwili ilitajwa kwa namna, kwa kweli ngumu sana.

Ndiyo maana wakati Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete anachangia hapa, nikamuuliza zile bilioni alizokwuwa anazitaja yeye anatoka mkoa gani? Na huu ni Mkoa wa Lindi Waheshimiwa Wabunge; kama jimbo moja limepelekewa zaidi ya bilioni 500 maana yake ni kwamba nia njema ipo ya kupeleka maendeleo kila mahali. (*Makofi*)

Wewe ni Mbunge na una jimbo lako; kwanza wewe ni kiongozi wa jimbo hilo, wale wananchi wanataka wasikie

kwenye jimbo lako unataka miradi gani? Usipoisema ya jimbo lako ukawazungumzia watu mkoa mzima; haya Mtwara kuna Mheshimiwa Mhata pale, jana alieleza kwake mambo gani yamefanyika na mambo gani anapenda yafanyike. Sasa ukieleza kwa namna ya jumla jumla kuashiria kwamba huko mahali hakuna chochote si sawasawa. Zungumza ya jimbo lako.

Labda kama umefanya ziara ya mikoa yote ukazijua changamoto zote, basi eleza yaliyofanyika halafu eleza na changamoto. Usijaribu kuonesha kwamba hii nchi imegawanyika kwa namna ambayo kuna sehemu fedha zinakwenda kwingine haziendi kabisa. Haipendezi kwa sababu sisi wote lengo letu ni moja, tunataka maendeleo nchi hii yaende kila mahali. Sasa tusileté picha hiyo ya kuleta mgawanyiko kana kwamba kuna sehemu ambayo inaonewa kuliko nydingine.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza leo na ninaamni Waheshimiwa Wabunge tutakuwa tumeelewana vizuri; mara nydingi tunayahuishisha maendeleo kwenye maeneo yetu na uchaguzi. Naistikia hii michango mara kadhaa. Kimsingi maendeleo yanapofanywa na Serikali yanatazama Ilani ya Chama kilichochaguliwa.

Sasa Serikali inapofanya ule utekelezaji inaleta maendeleo kulingana na ile Ilani, siyo Serikali kwamba inafanya maendeleo illi ije ipate kura, hapana. Wala wewe usifikie mahali ukawa unachangia kana kwamba likifanyika jambo fulani ndiyo utarudi humu ndani, hapana. Kuna maeneo mengi sana ambayo watu hawajarudi humu ndani na Serikali imefanya kazi kwenye hayo maeneo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, siyo kwamba kwa wewe kusema nitapata wakati mgumu sana kuchaguliwa mambo yasipofanyika, kwamba pengine kuna jambo fulani hivi linaongezeka la ziada; halipo. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ninachotaka kusema ni kwamba, Serikali inapopeleka maendeleo mahali haitazami kura, ukitaka kuhusianisha hivyo basi sehemu ambazo zina watu wachache zitakuwa hazipati maendeleo kwa sababu mtu hapati kura nyangi. Na pia maana yake sehemu zile zenyewe Wabunge wa Upinzani basi maendeleo yangekuwa hayaendi huko kwa sababu Serikali ni ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwaombe sana, tunapochangia tuwe makini na zile kauli zetu kwa sababu sisi wenyewe zinaturudisha hatua nyuma. Mheshimiwa Rais anapopeleka fedha kwenye majimbo yetu, haangalii Mbunge wa hapa ni yupi, Mbunge wa hapa anaafananaje; anaangalia Watanzania, ahsante sana. (*Makof*)

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, hli habari ya kuhusianisha maendeleo na uchaguzi, tutazungumza hizo habari za uchaguzi nje ya hapa; na wenzetu wale ambao huwa wanakaa upande wa kushoto ndiyo wengi walikuwa wanatuambia namna hiyo. Kwa hiyo, tusiambiane sisi wenyewe sasa wakati huu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 16 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*